# MAENDELEO YA KISWAHILI TANZANIA

Neno asili lina maana kuwa jinsi kitu au jambo lilivyotokea au lilivyoanza na tunapozungumzia asili ya lugha ya Kiswahili ina maanisha tunachunguza namna lugha hiyo ilivyoanza. Wataalamu mbalimbali wa lugha wamefanya uchunguzi juu ya asili ya lugha ya Kiswahili.

Uchunguzi huo umejenga nadharia mbalimbali zinazoelezea chimbuko la lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla historia kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili ina matatizo mengi na ndiyo maana kuna nadharia mbalimbali zinazoelezea juu ya asili ya lugha ya Kiswahili.

Miongoni mwa matatizo yanayoikabili historia ya Kiswahili ni pamoja na:

1. Hakuna uthibitisho kamili juu ya nadharia zinaelezea asili ya lugha ya Kiswahili na kuenea kwake.
2. Uchunguzi wa asili ya Kiswahili ulifanywa na wataalamu wa kizungu ambao waliandika historia ya Kiswahili jinsi walivyoelewa wao baada ya kupata ushahidi kidogo tu.
3. Wazawa hawakushirikishwa ipasavyo katika uchunguzi wa lugha ya Kiswahili.
4. Hapakuwa na kumbukumbu za kutosha kwa sababu babu zetu hawakujua kusoma wala kuandika hivyo basi kuna upungufu wa kumbukumbu.

Kutokana na matatizo hayo yanayoikabili historia ya Kiswahili kuna nadharia mbalimbali zinazoelezea historia ya lugha ya Kiswahili. Nadharia hizo ni kama vile:-

(i) Kiswahili asili yake Kongo

(ii) Kiswahili ni kundi au pijini

(iii) Kiswahili ni lugha ya vizalia

(iv) Kiswahili ni Kiarabu

(v) Kiswahili ni Kibantu.

1. **<u>KISWAHILI ASILI YAKE NI KONGO</u>**

Baadhi ya wataalamu hudai kuwa asili yake ni Kongo (Zaire). Madai haya yanaimarishwa zaidi na wazo jingine linalodai kwamba katika vipindi lengwa vilivyopata kuwepo sehemu za Pwani ya Afrika Mashariki hazikuwa zimekaliwa na watu. Lakini kutokana na hali ya uzito, ufugaji, na biashara inadaiwa kuwa wabantu walisambaa Afrika Mashariki kupitia Kigoma na baadhi ya sehemu za Uganda. Wakati wa kusambaa kwao walieneza pia lugha zao kikiwemo Kiswahili.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

**UDHAIFU**

Madai kuwa asili ya Kiswahili ni Kongo hayana msingi kwa sababu mpaka sasa wataalamu wa nadharia hiyo hawajaweza kueleza na kuthibitisha kisayansi ama kihistoria juu ya lini hasa watu walianza kuishi Pwani ya Afrika Mashariki.

**II. KISWAHILI NI KRIOLI AU PIJINI**

Baadhi ya wataalamu hudai kuwa asili ya Kiswahili ni tokeo la mwingilio baina ya wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki na wageni wa kiarabu. Wataalamu hawa hudai kuwa Kiswahili ni lugha ya kati iliyozuka ili kurahisisha au kufanikisha mawasiliano katika shughuli ya biashara ya mwanzo. Wataalamu hawa husisitiza kuwa lugha ya Kiswahili haikuwepo kabisa kabla ya hapo. Wanaona lugha ya Kiswahili ilianza kama pijini na baadaye kukua na kuwa kama Krioli kutokana na lugha hiyo kuwa lugha ya mwanzo kwa wazungumzaji.

**Pijini ni nini?**

Ni lugha ambayo huzuka kutokana na kuwepo pamoja kwa makundi mawili yanayotumia lugha mbili tofauti. Ili makundi hayo yaweze kuwasiliana, huundwa lugha ambayo kitabia ni tofauti na zile zinazozungumzwa na makundi yanayohusika. Lugha hii inaweza kuwa na msamiati kutoka katika lugha moja kati ya hizo mbili, au inaweza ikawa na msamiati wenye uzito sawa. Lugha hii ndiyo huitwa Pijini. Pijini huzuka kutokana na vitu kama vile biashara, utumwa, ukoloni, n.k

**Krioli ni nini?**

Kwa kawaida watu wanaozungumza lugha ya pijini wanaweza kuzoeana na kuishi kwa pamoja hata kuoana. Watoto watakaozaliwa hutumia lugha ya pijini kama lugha yao ya kwanza. Lugha hii inayotumiwa na watoto hawa watakaozaliwa huitwa krioli. **Krioli ni pijini iliyokomaa.**

Wataalamu wa nadharia hii hutumia kigezo cha msamiati uliopo katika lugha ya Kiswahili ambao kwa kiasi kikubwa unatoka katika lugha ya Kiarabu. Ni kweli kuwa lugha hii inamchango mkubwa wa msamiati katika lugha ya Kiswahili.

**UDHAIFU**

Hutumia kigezo kimoja cha msamiati peke yake kama kigezo pekee ni udhaifu kwa kuwa lugha inaweza kutazamana kwa kutumia vigezo vingine, matamshi, maumbo ya maneno au miundo ya sentensi. Ukitumia vigezo mbalimbali vya uchambuzi wa lugha, lugha ya Kiswahili ina mfanano zaidi na lugha za kibantu kuliko madai yaliyotolewa na nadharia hii.

**III. KISWAHILI NI KIARABU**

Kuna madai kwamba lugha ya Kiswahili asili yake ni Kiarabu. Wataalamu wa nadharia hii hutetea madai yao kwa hoja kuu tatu:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. Idadi kubwa ya maneno yaliyomo katika Kiswahili takribani 30% ni maneno yenye asili ya Kiarabu. Hivyo basi ni uthibitisho tosha kwamba Kiswahili kilianza kama pijini ya Kiarabu.
2. Neno lenyewe, Kiswahili; ambalo asili yake ni Kiarabu. Neno Kiswahili limetokana na neno ***'sahil'*** ambalo ni neno la Kiarabu lenye maana ya ***'Pwani***' na neon ***'Swahili***' hutumika likiwa na maana ya 'Pwani". Kwa hiyo neno, 'waswahili' lina maana 'watu wa pwani'.
3. Dini / Biashara / Mila na desturi. Inadaiwa kwamba kwa kuwa Kiswahili kilianzia Pwani na kuwa kuna idadi kubwa ya wenyeji wa Pwani ni waislamu kwa imani zao, na kwa kuwa uislamu ulileta na waarabu, basi hata Kiswahili nacho kililetwa na waarabu.

**UDHAIFU**

1. Kutumia kigezo cha msamiati ni udhaifu kwa sababu kila lugha huchukua msamiati kutoka lugha nyingine. Kiswahili hakikuchukua msamiati kutoka Kiarabu pekee kutoka lugha nyingine kama: Kiajemi, Kireno, Kihindi, Kijerumani na Kiingereza.
2. Lugha huchukua msamiati mwingi kutoka lugha fulani si kigezo cha kuhalalisha kuwa lugha fulani ina asili fulani mfano: Kiingereza huchukua maneno kutoka lugha ya Kifaransa, haiwezekani kuhitimisha kuwa Kiingereza ni Kifaransa.
3. Pia kutumia kigezo cha dini ni udhaifu. Kwa mfano hatuwezi kusema Kiingereza ni Ukristo kwa kuwa Waingereza ni Wakristo kwa imani yao. Pia nchi kama Senegal ambayo ina Waislamu wengi lugha ya Kiswahili haizungumzwi huko. Ni wazi kuwa Uislamu ungekuwa unafungamana na Kiswahili, kingezungumzwa kila sehemu ambapo Uislamu umeenea.

## IV. KISWAHILI NI KIBANTU

Nadharia hii hutumia ushahidi wa kiisimu na kihistoria kuchunguza lugha ya Kiswahili katika mfumo mzima wa kihistoria wa mgawanyiko na usambaaji wa lugha za kibantu . Nadharia hii inaungwa mkono na wataalamu kama ***Malcom Guthrie***, ***C. Meinhoff*** na ***C. Rohl***. Wataalamu hawa huhitimisha kuwa Kiswahili ni mojawapo ya lugha ya jamii kubwa ya lugha za kibantu. Nadharia hii ndiyo inaelekea kukubalika- kwa wengi kuwa ndiyo sahihi katika kuelewa asili ya Kiswahili. Kwa sababu nadharia hii imethibitishwa kwa hoja za **kiisimu** na hoja za **kihistoria**.

## A. USHAHIDI WA KIISIMU

Ushahidi wa kiisimu ni ushahidi unaothibitishwa kwa misingi ya sayansi ya lugha. Isimu huchunguza lugha kwa undani kwa kutumia tanzu zake. Baada ya kufanyiwa utafiti wa kina na wataalamu mbalimbali, ilithibitika kuwa asili ya Kiswahili ni kibantu kutokana na vingezo vifuatavyo**:-**

- **Utafiti wa Malcom Guthrie**

Ni mtaalamu wa isimu kutoka chuo kikuu cha London, aliyefanya utafiti wa kutafuta uhusiano kati ya lugha ya Kiswahili na lugha za kibantu kwa miaka 20 katika nchi za Kiafrika zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zinasadikika kuwa ndipo wabantu wanapoishi.

Katika utafiti wake alichunguza mizizi ya maneno 22,000 kutoka lugha za Kibantu ikiwemo lugha ya Kiswahili

**Katika utafiti wake aligundua mambo yafuatayo:-**

(a) Mizizi ***2,300*** ilizagaa katika lugha mbalimbali za kibantu ikiwemo lugha ya Kiswahili.

(b) Mizizi 500 iliungana katika lugha zote 200 alizozifanyia utafiti.

(c) Alipolinganisha lugha hizo na lugha ya Kiswahili, zilionesha ulinganifu kama ifuatavyo:-

- Kiwemba (Zambia) kililingana na Kiswahili kwa 54%.

- Kiluba (Katanga) kililingana na Kiswahili kwa 51%

- Kikongo (DRC) kililingana na Kiswahili kwa 44%

- Kiswahili cha (A. Mashariki) 44%

- Kisukuma (Tanzania) 41%

- Kiyao (Tanzania, Msumbiji) 35%.

- Kirundi (Burundi) 43%

- Kisotha (Botswana) 20%

Mtaalamu huyu pia aligundua kadri unavyoshuka Kaskazini ya Katanga ndiyo msamiati unavyoachana zaidi,

- **Mfanano wa msamiati**

Ushahidi huu ulitokana na utafiti wa ***Prof. Maganga*** ambaye alibaini kuwa ***60%*** ya maneno ya Kiswahili yenye kuandikika na kutamkika, yana asili ya Kibantu. 30% ya msamiati wa lugha ya Kiswahili unatoka katika Kiarabu na ***10%*** inatoka katika lugha nyingine mfano: Kireno, Kiingereza.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Ni wazi kuwa msamiati wa Kiswahili na Kibantu hautofautiani sana, hasa katika matamshi:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | → | Maji | mtu |
| Kindali | → | amashi | umundu |
| Kizigua | → | manzi | mntu |
| Kijita | → | amanji | omanu |
| Kipare | → | mbombe | mndu |
| Kichaga | → | mringa | mndu |
| Kinyakyusa | → | amesi | mundu |
| Kihangaza | → | amazi | |
| Kipogoro | → | maishi | |

- **Miundo ya tungo:-**

Miundo ya tungo za maneno ya Kiswahili inafanana na miundo ya tungo za maneno ya Kibantu. ***Mfano***: miundo ya sentensi za Kiswahili huwa na muundo wa Kiima na kuarifu hali kadhalika miundo ya sentensi za Kibantu huwa na muundo huo huo.

***Mfano:-***

- Mama / anakunywa maji (Kiswahili)

K A

- Mayo / aling'hwa minze (Kisukuma)

K A

- Jubha / ikonwa amesi (Kinyakyusa)

K A

- Yubha / inywa lulenga (Kihehe)

K A

- Mawe / ang’wa mazi (Kiha)

K A

***NB:*** Pia miundo ya sentensi za Kiswahili hubadilika katika maumbo ya umoja na wingi.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pia maumbo ya kibantu hubadilika katika maumbo ya umoja na wingi.

***Mfano:*** Watoto / wanakunywa maji (Kiswahili).

- Mwana / ikonwa amesi (Kinyakyusa)

K A

- Mwana / avana vinywa lulenga (Kihehe)

K A

- Ng'wana / aling'wa minze (Kisukuma)-umoja

K A

- Bhana / bhaling'wa minze (Kisukuma)-wingi

K A

- **<u>Ngeli za majina</u>**

Makundi ya majina mbalimbali katika lugha ya Kiswahili huwa na makubaliano kwa kufuata maumbo ya umoja na wingi pamoja na upatanisho wa kisarufi.

Tabia hizi za majina ya Kiswahili hujitokeza pia katika majina ya Kibantu;

(a) **Kwa kutumia maumbo ya majina.**

Majina mengi ya Kiswahili huwa na maumbo ya umoja na wingi, halikadhalika kwa majina mengi ya Kibantu.

| | | |
|---|---|---|
| ***Mfano:*** Kiswahili | m-toto | wa-toto |
| Kisukuma | ng'-ana | bh-ana |
| Kinyakyusa | mw-ana | b-ana |
| Kihehe | mw –ana | v-ana |
| Kiswahili | ki –ti | vi – ti |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

| | | |
|---|---|---|
| Kinyakyusa | ki-goda | vi-goda |
| Kihehe | ki-kota | vi-kota |

(b) **Kigezo cha upatanisho wa kisarufi.**

Kwa kutumia kigezo hiki, nomino za Kiswahili na za kibantu hufuata upatanisho wa kisarufi kwa kupachika viambishi pia. Viambishi hivyo hubadilika kutokana na mabadiliko ya maumbo ya umoja na wingi.

***Mfano:*** Mtoto mzuri anakunywa maji

Watoto wazuri wanakunywa maji

Mwana mnunu ikonwa amesi

Bana banunu b**i**konwa amesi

Mwana mnofu inywa lulenga-umoja

Vana vanofu vinywa lulenga-wingi

- **Vitenzi vya Kiswahili na vya Kibantu**

Tabia ya vitenzi hivi hufanana. Mfanano huo hujitokeza katika vipengele vifuatavyo:-

(a) **Viambishi**

Lugha ya Kiswahili na kibantu, vitenzi vyake huwa na mzizi pamoja na viambishi awali na tamati.

***Mfano:*** Kiswahili a – na - lim – a

Kindali a – ku – lim – a

Kikurya a – ra – rem – a

1 - viambishi vya nafsi

2 - Viambishi vya wakati

3 - mzizi

4 - Viambishi tamati maana.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(b) **Vitenzi vya lugha ya Kiswahili na Kibantu vina tabia ya kunyumbuka**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | Kucheka | kuchekesha | Kuchekelea | kuchekwa |
| Kinyamwezi | Kuseka | kusekesha | kusekelela | Kusekwa |
| Kindali | Kuseka | Kusekesha | kusekelela | kusekwa |
| Kipogoro | Kuseka | kusekesa | kusekelela | Kusekwa |
| Kibena | Kuheka | kuhekesha | kuhekelela | kuhekwa |

(c) **Mwanzo wa vitenzi**

Vitenzi vya Kiswahili na Kibantu huanza na viambishi vya nafsi mwanzoni.

***Mfano:*** Ni – nakwenda

- ni - sumwike

- ni – ngenda

(d) **Mwisho wa vitenzi**

Vitenzi vingi vya lugha ya Kiswahili na vile vya kibantu, huishia na irabu ('a') mwishoni.

***Mfano:-***

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kukimbia – a | Kuwind- a | Kushuk – a | kiswahili |
| Kupil-a | Kuhwim –a | Kutend – a | kisukuma |
| Kukimbil -a | Kufwin- a | Kuwik -a | kihehe |

B. **USHAHIDI WA KIHISTORIA**

Licha ya ushahidi wa kiisimu, pia kuna ushahidi wa kihistoria unathibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu.

Ushahidi huo unathibitishwa na wageni mbalimbali waliofika Afrika Mashariki na kudhihirisha kuwa Kiswahili kilizungumzwa Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wageni.

Ushahidi huu ulitolewa na wageni mbalimbali waliofika Afrika ya Mashariki na kuthibitisha kuwa kabla ya kufika kwao, Kiswahili kilizungumzwa.Wageni hao ni kama wafuatao:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- **Ushahidi wa Marco Pollo**

Ni mwanataaluma wa Kizungu aliyejishughulisha na masuala mbalimbali ya Kijiogragia na kusafiri sehemu nyingine duniani.

Katika moja ya maandiko yake, anasema hivi; "Zanzibar ni kisiwa kilicho kizuri ambacho kinamzunguko wa maili 200" Watu wake wanaabudu Mungu. Wana mfalme na wanatumia lugha yao na hawalipi ushuru kwa mtu

Nukuu hii imenukuliwa kutoka kitabu cha "***SAFARI ZA MARCO POLLO***" ***(1958 – 301)***. [Penguin Books]

Pia katika kitabu chake cha Kijiografia ambacho hakikuchapishwa lakini kimetafsiriwa kwa Kirusi na Kifaransa lakini kina maneno kama vile; Ungudya ambako sasa ni Unguja. Zanguaba ambako sasa ni Zanzibar. Maneno mengine ni kama; kundi, firi, Omani, Murijani, na kisuka. Haya ni majina ya aina mbalimbali za ndizi zilizopatikana Zanzibar.

- **Ushahidi wa Al – Masoud (915 BK)**

Katika moja ya maandishi yake anazungumzia juu ya wakazi wa mwambao ambao walijulikana kwa jina la Waenji. Kwa dhana hii neno Zanzibar linatokana na neno Zanjibar, yaani pwani ya Zanji.

Al – Masoud anaonesha kwamba, Wazanji walikuwa na watawala kwa nguvu za Mungu. Viongozi hawa walikuwa wacha Mungu, Huenda neno Wakitumia / ina maana ya wafalme. Anasisitiza kuwa walisema lugha fasaha na walikuwa na viongozi walio hutubia kwa lugha yao. Kutokana na neno Zanji inawezekana kabla ya kuja kwa waarabu, Kiswahili kilikuwa Kizaramo au Kizanji.

- **Historia ya Kilwa**

Kimsingi habari hizi zinaeleza historia ya Kilwa, karne ya 10 mpaka 16 BK na zinahusiana na kutaja majina ya utani kama vile Mkoma watu, Nguo nyingi n.k Ambayo walipewa Masultan wa kwanza wa Kilwa ambao ni Ali Ilbin Hussein na mwanawe. Mohamed Ibin Ali kutokana na habari hizi huenda lugha ya Kiswahili ilianza kuzungumzwa kuanzia karne ya 10 au 11.

Maelezo ya kihistoria yanaeleza juu ya Sultani aliyeitwa Talt Ibin Al – Hussein aliyepewa jina la utani Hasha haefiki

- **Ushahidi wa Ibin Batuta (14 BK)**

Mohamed Bin Abdallah Ibin Batuta ana asili ya kiarabu alifika Afrika Mashariki kunako mwaka 1331 BK, Katika maandishi yake anaeleza maisha ya watu wa nchi ya Afrika Mashariki ingawa yeye aliita nchi ya Waswahili. Anataja miji kama vile Mogadishu, na Kilwa. Alisema, "Basi nilianza kusafiri baharini kutoka Mogadisho kwenda nchi ya Waswahili na Kilwa ambao umo

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

katika nchi ya Zanji. Tulifika Mombasa kisiwa kikubwa, mwendo wa siku mbili kutoka nchi ya waswahili, Watu hawajishughulishi na kilimo ingawa huagiza nafaka toka kwa waswahili.”

- **Maandishi ya Morrice**

Maandishi haya yalijitokeza mwaka ***1779,*** Katika maandishi hayo Morrice anawagawa watu wa Afrika Mashariki katika makundi matatu, ambayo ni waarabu, wasuriana na waafrika. Anasisitiza kuwa masuriana na waafrika walishakaa na kuwa kundi moja. Wakaelewana na kusema lugha moja ya kisuriana. Kuna kuwa huenda kisuriana ndicho Kiswahili cha leo.

- **Ugunduzi wa Ali Idris**

Ugunduzi huu ulifanywa huko Sicily mwaka 1100 mpaka 1166 BK kwenye mahakana ya mfalme Roger II, Katika ugunduzi huu ilisadikika Kiswahili kiliandikwa kabla ya karne ya 10 BK. Al Idrisi alikuwa wa kwanza kugundua jina la zamani la Zanzibar kuwa ni Ungudya. Katika maelezo yake anaandika pia majina ya aina za ndizi mbalimbali zilizopatikana huko Ungudya kama vile kikombe, mkono wa tembo, sukari, na muriani.

- **Vitabu vya Periplus na Yu – Yanga Tsa - Tsu:-**

**- Kitabu cha Periplus**

Hiki kinahusu mwongozo wa bahari ya Hindi na inasadikika kuwa kiliandikwa karne I katika mji wa Alexander. Kitabu hiki kinataja habari za Azania yaani Afrika Mashariki na habari za vyombo vya baharini kama vile ngalawa, madema na mitepe. Kitabu hiki kinaeleza kuwa watu wageni hutozwa ushuru na wafanyabiashara wenyeji na wanaijua pia lugha ya wenyeji vizuri.

**- Kitabu cha Yu- Yanga Tsa - Tsu**

Kitabu hiki kinaeleza habari za upwa wa Afrika Mashariki na shughuli mbalimbali za Wachina hapa Afrika mashariki.

**- Chu – Fan – Chi**

Kilichapishwa 1226 na kinaeleza bahari za Zanzibar na shughuli mbalimbali za Wachina hapa Afrika Mashariki.

- **Ushairi wa Kiswahili.**

**- Utenzi wa Fumo Lyongo**


Hili ndilo shairi la zamani kabisa. Lilipata kuandikwa katika lugha ya Kiswahili na inasemekana liliandikwa karne ya 13 BK. Uwepo wa shairi hili unadhihirisha kuwepo kwa Kiswahili kabla ya hapo. Huenda kilitumika kabla ya karne ya 10 BK.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## CHIMBUKO LA KISWAHILI

Nadharia hii inazungumzia kuhusu mahali hasa ambapo lugha ya Kiswahili ilichipukia. Wataalam wa lugha ya Kiswahili wanatofautiana kuelezea mahali hasa ambapo ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili ilichipukia Kaskazini, Mashariki mwa Kenya na ilitokana na Kingozi na kuna wengine wanadai kuwa Kiswahili chimbuko lake ni Bagamoyo mpaka Mzizima, eneo lililojulikana kama Dar es Salaam hadi Kilwa. Wataalam hawa wanadai lugha ya Kiswahili ilienea kama **Kishomvi**. Madai ya wataalamu hawa hayajawahi kuthibitishwa kwa hoja makini na tafiti zinaonesha kwamba madai hayo hayana ukweli yanahitaji tafiti zaidi. Kwa ujumla madai haya yanaweza kuwekwa kwenye mchoro kama ifuatavyo:-




***NB:*** Kuna kundi la wataalamu wengine linalodai kuwa chimbuko lake ni sehemu mbalimbali za Pwani ya Afrika Mashariki. Mfano mtaalamu ***Freeman Grenvill*** katika makala yake inayoitwa ***Medieval For Swahili (1959)*** anadai kuwa lugha ya Kiswahili ilianza na kuinuka katika upeo wote wa Afrika Mashariki kama ambavyo baadhi ya maneno, majina ya watawala na maofisa wa serikali yanavyojitokeza katika fasihi.

Madai ya mtaalamu huyu yanaashiria kwamba watu walioishi katika maeneo mbalimbali ya upande wa Afrika Mashariki walikuwa wakizungumza lugha zao mbalimbali. Lugha zote hizi zilikuwa za kibantu na hazikutofautiana sana.

Watu hawa katika kuwasaidia hasa katika biashara walilazimika kurahisisha lugha zao kwa kiasi fulani ili waweze kuwasiliana na miongoni mwao. Urahisishaji huo wa lugha na kuzuka kwa lugha hiyo kubwa ni jambo lililotokea katika sehemu zote za upwa wa Afrika Mashariki. Matokeo yake kulizuka lugha ambazo zilijulikana kama lahaja za Kiswahili. Lahaja hizo zilizungumzwa kutoka kusini mwa Somalia hadi Kaskazini-mashariki mwa Msumbiji.

Hapo tunapata lahaja kama vile kitikwa, Kiamu, Chichifundi, Kimvita, Kimombasa, Kimtang'ata, Kimakunduchi, Kihadimu, Kitumbata na Kipemba. Lahaja hizo zinafanana zaidi na lugha mbalimbali za kibantu kuliko zinavyofanana na Kiswahili sanifu kwa kuwa Kiswahili sanifu kina maneno mengi ya mkopo.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**MASWALI**

1. Kwa kutumia hoja madhubuti fafanua chimbuko la lugha ya Kiswahili.

2. Wanadai kuwa Kiswahili ni Kiarabu, wanahoja kubwa kuu tatu. Fafanua hoja hizo.

3. Kiswahili ni Kiarabu kwa jina lake, lakini ni Kibantu kwa asili yake, thibitisha kwa hoja za kiisimu.

## LUGHA MAMA (LUGHA YA KWANZA), LUGHA YAPILI NA LUGHA RASMI

**Lugha rasmi ni ipi?**

Ni lugha inayoteuliwa na serikali ili itumike katika shughuli za kiserikali. Kiswahili

Tanzania ni lugha ya taifa pia ni lugha rasmi.

**Sifa za lugha rasmi:-**

(i) Yaweza kuwa lugha sanifu au isiwe sanifu lakini pia yaweza kuwa fasaha au isiwe fasaha.

(ii) Inaweza ikawa lugha ya taifa au isiwe lugha ya taifa.

(iii) Huwa haifuati kabila wala mchanganyiko wa makabila yaliyopo nchini.

(iv) Yaweza kuwa lugha ya kigeni kama vile kiingereza, Kifaransa, Kichina.

(v). Hutegemea utawala uliopo madakarani.

**Lugha mama (Lugha ya kwanza):-**

Ni lugha ambayo mtu hujifunza utotoni baada tu ya kuzaliwa, kabla ya kujifunza lugha

ya pili. Mtoto hujifunza lugha hii kwa kusikiliza kutoka kwa wazazi au majirani. Lugha

hii ni rahisi kujifunza kulingana na ya pili kwa sababu zifuatazo:

(i) Mtoto huwa na muda mrefu wa kujifunza (usio koma)

(ii) Mtoto hujifunza lugha katika mazingira halisi, mfano vile anavyojifunza vipo pale pale.

(iii) Uhusiano wa mtoto na wanaomzunguka kuwa mzuri.

(iv) Kuna kuwa na msaada wa kutosha katika kujifunza.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(v) Kuna kuwa na uzoefu katika lugha hiyo hiyo moja.

**Dhima ya lugha ya kwanza:-**

Kukidhi haja ya mawasiliano kwa watu wanaomzunguka mtoto.

***NB:*** Lugha ya kwanza inaweza kuwa lugha ya pili kwa watu wengine na lugha ya pili inaweza kuwa ya kwanza kwa watu wengine. Mfano: Kiswahili ni lugha ya kwanza kwa Watanzania wote waliozaliwa mjini lakini yaweza kuwa lugha ya pili kwa Watanzania waliozaliwa vijijini.

**Lugha ya pili:-**

Lugha ya pili ni lugha ambayo mwanadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Mara nyingi lugha ya pili huwa na athari ya lugha ya kwanza kuhusishwa na mazingira ya lugha ya pili. Kwa Watanzania walio wengi hasa waliozaliwa kijijini Kiswahili ni lugha yao ya pili.

**Matumizi ya lugha ya pili:-**

1. Kutaka kukidhi haja ya mawasiliano kwa jamii ambazo si wazungumzaji wa lugha ya kwanza.
2. Kutaka kujihusisha na jamii inayozungumza lugha hiyo ya pili.

***Mfano:*** tunajifunza Kiingereza ili kujihusisha na jamii nyingine.

---

# UHAKIKI WA FASIHI ANDISHI

## UHAKIKI WA RIWAYA YA

## "MFADHILI"

**WACHAPISHAJI:** MACMILLAN AIDAN LTD

**MWANDISHI:** HUSSEIN TUWA

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**MWAKA:** 2007

**A.MAUDHUI**

**UTANGULIZI**

Ni riwaya inayozungumzia mapenzi katika jamii pamoja na athari zake katika jamii. Ikizungumzia hasa mapenzi ya dhati nayale yasio ya dhati.

**DHAMIRA KUU**

**MAPENZI NA NDOA**

Mwandishi anaonyesha mapenzi ya dhati na yasiyo ya dhati pamoja na ndoa.

**Mapenzi ya dhati**

- Kati ya Gaddi na dada yake Bi Hanuna.
- Gaddi kwa Dania
- Gaddi kwa Junior
- Mama Mlole na wafanyakazi wake
- Nunu kwa Dania
- Nunu na Boaz
- Dk Virani na Gaddi
- Wazazi wa Dania na Dania mwenyewe
- Nunu na Gaddi

**Mapenzi yasiyo yadhati**

- Kati ya Jerry na Dania
- Rafiki yake Gaddi kwa Gaddi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Ndoa yenye mapenzi ya dhati**

- Gaddi kwa Nyambuja

**Ndoa isiyo ya mapenzi ya dhati**

- Nyambuja kwa Gaddi

**USALITI**

Msanii ameonyesha watu mbalimbali waliosalitiwa na athari za usaliti huo.

Nyambuja alimsaliti Gaddi kwa kufanya mapenzi nje ya ndoa. Tena alimsaliti na rafiki wa Gaddi, athari yake, utendaji wa kazi wa Gaddi ulishuka na hatimaye alipoteza kazi.

Mfano:

**Dania kwa Gaddi.**

Athari yake Gaddi kupata shinikizo la moyo kutokana na Jerry na Bi Hanuna kufungwa.

Afisa uzalishaji na Gaddi, athari yake gaddi alishushwa cheo kazini.

**JerrykwaDania.**

Hakutokea siku ya harusi, pia katika kutoa ini kwa Dania alipokuwa anaumwa.

**USALITI MZURI.**

Daktari viiani kwa Gaddi Bulah.

**UONGOZI MZURI**

Mwandishi amemtumia mama Mlole kwani aliwasimamia vizuri wafanyakazi wake,

Alimsaidia Gaddi Bullah alipopata tatizo kazini

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pia alimsaidia Dania wakati amepata matatizo.

**BIDII KATIKA KAZI**

Mwandishi anaonesha Dania na Gaddi kuwa na bidii katika kazi mpaka tu pale walipopata matatizo. Pia Daktari viran alimhudumia Gaddi Bullah kwa moyo.

**CHUKI**

Ameonyesha chuki mbalimbali kati ya wahusika,

- Bi Hanuna alikuwa na chuki na Nunu sababu ya Dania.
- Dania kwa Gaddi. ( mwanzoni)
- Dania kwa Jerry baada ya kuachwa.
- Nunu kwa Jerry kwani alimsaliti Dania
- Wazazi wa Dania kwa Jerry kwani alimtenda binti yao.

**DHARAU**

Mwandishi amemtumia Nyambuja kama mwenye dharau. Mfano alisafiri safari za ghafla na kumtaarifu tu mumewe kwa simu. Vilevile alichelewa kurudi nyumbani.

Nyambuja kufanya mapenzi na rafiki yake Gaddi ni dharau. Pia barua aliyomwandikia Gaddi ni kitendo cha dharau.

Dania kwa Gaddi ofisini pia alipomfukuza mbele ya Junior. Vile vile baada ya kumwacha Gaddi na kurudi kwa Jerry.

**NAFASI YA MWANAMKE,** Mwanamke ameonyeshwa/amechorwa kama ifuatavyo:-

Kama kiumbe asiye na msimamo. Dania hakuwa na msimamo katika maamuzi yake. Mfano: Jerry- Gaddi- Jerry- Gaddi

Kama mtu mwenye huruma na mshauri mzuri. Mfano mzuri ni Nunu aliyekuwa bega kwa bega na Dania. katika matatizo yote pia mama mlole kwawafanyakazi wenzie

Kama mtu katili na msaliti. Mfano mzuri ni Dania na Nyambuja kwa jinsi walivyomtenda Gaddi.

Kama kiumbe jasiri, Nunu aliyefanya kazi ya kumpatanisha Gaddi na Dania hata kumteka Bi Hanuna dada yake Gaddi.

Mwenye upendo na moyo wa huruma. Bi Hanuna aliyempenda sana Gaddi na Mama fausta mlole aliyependa wafanya kazi wake.

**NAFASI YA MWANAUME**

- Mtu mwenye mapenzi ya dhati kama vile Gaddi na Boaz.
- Kiumbe katili na msaliti kama Jerry na rafiki yake Gaddi.
- Mtu mwenye huruma mfano Gaddi Bulla.
- Asiyekuwa na msimamo kama vile Jerry.
- Mvumilivu na jasiri. Gaddi na Boaz

**UJUMBE**

- Rafiki wa kweli ni yule anayekusaidia wakati wa shida.
- Si kila king'aacho ni dhahabu
- Mtu akitenda kosa ni lazima akubali kutubu kosa.
- Ni vigumu kumpata mtu wa kukupenda kama unavyompenda wewe.
- Bidii na ufanisi katika kazi ni chachu ya maelendeleo

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Matatizo, chuki, majaribu na dharau ni lazima katika mapenzi na ndoa.

- Mwandishi ameonesha dhahiri kwamba uchungu wa mwana aujuaye mzazi.

**FALSAFA**

Msanii anaamini kuwa katika mapenzi kuna kupenda na kupendwa, kuna kuoa na kuachwa, hivyo ni vigumu kumpata mtu mwenye mapenzi ya dhati. Mfano Gaddi, Bullah, Jerry, Dania, Nyambuja.

**MSIMAMO**

Msimamo wa mwandishi ni wa kimapinduzi, kwani anaonyesha wazi kuwa katika suala la mapenzi na ndoa kuna matatizo yake. Watu lazima tukubali kusameheana kwani hujui ni yupi atakayekusaidia wakati wa shida.

**MGOGORO**

- Mgogoro kati ya Gaddi na Nyambuja (sababu ya usaliti ,kuachana)

- Mgogoro kati ya Gaddi na Dania(kurudiana na jerry, kutengana)

- Mgogoro kati ya Gaddi na Jerry(sababu ya Dania, kupigana)

- Jerry na wazazi wake Dania(jerry kuwa msaliti, alikataliwa)

- Nunu na Jerry.(Dania)

- Nunu, Boaz na Bi Hanuna (ugonjwa wa Dania, kumtoa Bi Hanuna)

- Dania na Jerry (usaliti, kurudiana)

- Mgogoro wa kinafsia (Gaddi, Dania)

**B. FANI**

**MUUNDO**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mwandishi ametumia muundo changamano, Kuna muundo rejea (SURA YA I), Muundo wa Msago (SURA YA II – MWISHO).

**MTINDO**

Mtindo wa masimulizi umetumika kwa kiasi kikubwa na kiasi kidogo ametumia daolojia/majibizano, Mwandishi pia ametumia nafsi zote tatu, Ametumia pia barua (uk. 65)mazungumzo ya simu. (uk. 118, 72)

**MATUMIZI YA LUGHA**

Lugha ni rahisi iliyojaa misemo, methali, matusi na mbinu mbalimbali za kisanaa
Lugha ya matusi.Mfano: Dania ni shwetwaani
Misemo na nahau. Mfano: Jibu lile lilimkata maini

**Methali**: Mfano:-

- Ukistaajabu ya musa utaona ya firauni
- Bora nusu shari kuliko shari kamili
- Hakuna marefu yasiyo na ncha
- Mkaidi hafaidi mpaka siku ya iddi

**Matumizi ya kingereza. Mfano:-**

- Boaz go! go! go! go! gooo!
- Nunu what the hell are you doing?

**Tamathali za semi na mbinu mbalimbali za kisanaa**

Tashbisha Mfano:

- Paa lake
- Nunu alikuwa kama mtu aliyepagawa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Kumfukuza kama mbwa kutoka katika nyumba ya marehemu mumewe.

**Sitiari** Mfano:

- Dania ni shwetwaani
- Kila mwanaume ni Jerry

**Takriri,** Mfano:-

- Hatua ndefu za harakaharaka
- Kwenda mwana kwenda
- Yaani alikuwa ni kimya moja kwa moja

**Tanakali sauti,** Mfano:-

- Sauti za Ko! Ko! Ko!

**Mdokezo,** mfano:-

- Ah! Ni kweli! Aunti.....lakini......

**Tashtiti,** Mfano:-

- Kamsubirie hukoooo! Siyo hapa kwangu, upo?
- Yaani alikuwa kimya moja kwa moja
- Yule

**Mjalizo,** Mfano:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Katili jeuri, masaliti na asiyestahili heshima hata kidogo
- Gaddi Bullah
- Ndiyo bwana

**Nidaa,** mfano:-

- Ee bwana we!
- Khah!
- Mnnh!

**MANDHARI**

- Ofisini
- Baa
- Nyumbani
- Barabarani
- Hospitalini
- Dar es salaam
- Arusha
- Pemba
- Chumbani

JINA LA KITABU

**Kwa kiasi kikubwa linasadifu yaliyomo:**

- Mama mlole alimfadhili Gaddi dhidi ya kashfa
- Mama mlole alimfadhili Dania baada ya kurudia pombe

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mama mlole alimfadhili Dania na Gaddi
- Gaddi alimfadhili Dania kwa kumpa ini ili asife
- Gaddi alimfadhili Junior

**KUFAULU NA KUTOFAULU**

Kufaulu kimaudhui.

Amefaulu kuonyesha matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii hasa swala la mapenzi na ndoa, kisha kutoa suluhisho la matatizo hayo.

Kufaulu kifani

Amefaulu kutumia lugha rahisi na inayoeleweka na amejenga wahusika wake vizuri

- Kutofaulu kifani

Ametumia viswahili badala ya Kiswahili sanifu,Pia matumizi ya kingereza,

- Kutofaulu kimaudhui

Ameangalia tu suala la mapenzi na kusahau matatizo mengi katika jamii.

**VUTA N'KUVUTE**

**Adam Shafi Adam**

Vuta n'Kuvute ni riwaya ya Kiswahili iliyoandikwa na mwandishi mahiri na mkongwe Shafi Adam Shafi na kuchapishwa kwa mara ya kwanza na Mkuki na Nyota Publishers Dar es Salaam.

Adam Shafi ni mwandishi wa Fasihi ya Kiswahili ambaye ameandika kazi nyingi na miongoni mwa kazi zake nzuri alizowahi kuandika ni Kuli na Kasri ya Mwinyi Fuad. Riwaya ya Vuta n'Kuvute imejikita juu ya Vuta ni Kuvute za kisiasa, kiutamaduni na kijamii.vuta n'kuvute hizi zimeweza kuibua dhamira mbalimbali ambazo mwandishi alikusudia ziifikie jamii aliyoiandikia. Pia mwandishi ametumia ufundi mkubwa wa kisanaa katika kuzielezea dhamira.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## Maudhui katika vuta n'kuvute

## VUTA NKUVUTE ZA KISIASA

Miongoni mwa vuta ni kuvute alizozijadili msanii ni vuta nkuvute za kisiasa, Vuta ni kuvute hii imeibua dhamira zifuatazo: mapambano, kujitoa muhanga umoja na mshikamano, mbinu/mikakati ya kuyaendea mambo, uongozi mbaya, ubaguzi na ukiukwaji wa haki za binadamu.

### i. Mapambano Dhidi Ya Dhuluma (Ukoloni)

Dhamira kuu inayojitokeza katika riwaya hii ni mapambano dhidi ya dhuluma. . Kama zilivyo kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili na ya Afrika huzungumzia mapambano ya kuleta ukombozi kwa jamii kandamizwa kwa kuwa jamii ya Kiafrika imepitia katika la kukandamizwa kutawaliwa (ukoloni) na kuibiwa rasilimali yake ndio maana mwandishi ameibua dhamira hii ili kuishajihisha jamii isiendelee kukubali kudhulumiwa, ipambane ili kujikomboa kutokana na unyonge, kudhulumiwa na kulinda heshima na utu wao. Dhamira hii ya mapambano ameizungumzia pia katika riwaya yake ya Kuli ambapo mhusika Rashidi na Mwenzake walianzisha mapambano dhidi ya Wazungu walio wakiwadhulumu Waafrika.

Dhamira ya mapambano imeonyeshwa kupitia mhusika Denge akishirikiana na kikundi chake cha akina Mambo, Sukutua, Chande, Huseni, Pazi na Salehe. Denge na kundi lake wanaanzisha mapambano dhidi ya Serikali ya kikoloni ya Kiingereza ili kuleta ukombozi wa kisiasa katika nchi za Zanzibar na Bara la Afrika kwa ujumla. Tazama maelezo haya:-

"Basi lazima tutumie njia za siri kwani mapambano yetu ni ya vuta n'kuvute. Wao wanavutia kule na sisi  tunavutia huku na katika mvutano huo, hapana suluhisho. Linaloweza kupatikana isipokuwa kuwa huru" (uk. 113).

Maelezo hapo juu yanaonyesha jinsi Denge alivyodhamiria kupambanua na serikali ya kikoloni mpaka uhuru upatikane na kuweza kujikomba kisiasa. Kuonyesha kwamba, mwandishi amekusudia kuonyesha dhamira ya mapambano, tazama maneno ya Denge:

"Haya ni mapambano, mapambano ya vuta n'kuvute, ni vita, tena vita vikubwa kila mmoja anamwinda mwenzake. Wao au sisi, lakini ushindi ni wetu, tutashinda tu"(uk. 122)

Maelezo hayo yanaonyesha Denge na kikundi chake walivyodhamiria kupambana na serikali dhalimu ya kikoloni na kuleta ukombozi kwa wananchi wa Zanzibar. Tena Denge amekusudia hasa kupambana na anajipa matumaini lazima ushindi upatikane dhidi ya wakoloni.

Kwa hiyo msanii anakusudia kuiamsha jamii isikubali dhuluma ya aina yoyote na iwe tayari kupambana kwa hali na mali kuhakikisha dhuluma inaondoka na kuleta haki na usawa ndani ya jamii.

Vile vile Denge na kundi lake wamepambana dhidi ya ubaguzi kwa kupanga kufanya fujo na vurumai katika ukumbi wa karimjee "Karimjee club" ukumbi uliokuwa unaendeshwa kwa misingi ya kibaguzi. Ni ukumbi uliokuwa ukitumiwa na watu wa asili ya Kihindi. Denge na kundi lake walioamua kufanya katika ukumbi huo ili kuonyesha hisia zao za kupinga ubaguzi. anasimulia:

*"Lilianza vurumai kubwa na hapo hapo*
*ilirushwa chupa nyingine iliyofuatiwa*
*na mawe kutoka katika kila pembe.*
*Kizilizala kikubwa kiliingia densini mle,*
*watu wakaanza kutimka bila ya kujua*
*wanakwenda wapi"(uk 136).*

Kwa hiyo Denge na wenzake walionyesha juhudi ya mapambano ya dhuluma ili waweze kujikomboa

### ii. Kujitoa Muhanga kwa manufaa ya umma katika jamii

Dhamira ya kujitoa muhanga imegusiwa sana na wasanii wa fasihi ya Kiswahili ili kuishajiisha jamii iwe tayari kujitolea kwa manufaa ya umma. Kwa mfano Mtolewa wa "Kivuli Kinaishi" alijitoa muhanga kupambana na uongozi dhalimu wa Bi - Kirembwe ili kukomboa wananchi wa Giningi. Vile vile Rashidi wa Kuli alijitolea muhanga kuwaongoza makuli kupambana na uongozi ukoloni uliokuwa ukiongoza bandari. Hiyo ni mifano michache katika fasihi ya Kiswahili. Hali kadhalika, msanii wa Vuta n'kuvute ameishughulikia dhamira hii ya kujitoa mhanga. Denge, Yasmin, Mambo na

Zanga ni wahusika ambao wamejitoa muhanga kuendesha harakati za kupambana na wakoloni wa Kiingereza huko Zanzibar.

Denge alijitoa muhanga kuendesha mapambano dhidi ya wakoloni wa Kiingereza. Serikali ya kikoloni ilikuwa na nguvu katika harakati zake. Denge alisafiri safari za hatari usiku kutoka Unguja kwenda Dar es Salaam kwa mashua, kwa ajili ya kusafirisha karatasi na vitabu vilivyokuwa vinawahamasisha wandugu waunge mkono mapambano ya kuing'oa serikali ya kikoloni. safari zao zilikuwa na mashaka makubwa, dhoruba, mawimbi makubwa lakini yote hayo Denge hakujali, alilokuwa anataka ni kupambana na kuikomboa jamii yake. Mfano Denge alisafiri safari ya kwenda Dar es Salaam kuchukua mashine ya kuchapia ambapo baada ya kurudi Unguja walikamatwa na askari wa kikoloni, Kabla ya kukamatwa Denge alisema"

*"Hii inaonekana madhubuti, sasa watatutambua, ikafika tu tutaanza kutoa gazeti"*
*"Mtaliitaje"*
*Kimbunga (uk. 224).*

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi Denge alivyokuwa tayari kwa lolote, amejitolea muhanga kupambana mpaka uhuru upatikane. Mwandishi anaonyesha safari ya kutoka Dar es Salaam kurudi Unguja ilivyokuwa na misukosuko.

*"...Lakini kitaacha wapi kwenda mrama*
*na mawimbi yalikuwa yakijizonga na*
*Kujizongoa, yakajitandaza juu ya uso wa*
*Bahari kwa kishindo; wakilipita wimbi hili*
*Jingine liko tayari mbele yao. Safari yote*
*Ikawa ya msukosuko mtupu usiku kucha"(uk. 225.)*

Msanii anataka kuonyesha jamii, katika harakati zozote kuna misukosuko kwa hiyo hakuna budi watu kujitoa mhanga ili kufanikisha harakati hizo, kama watu watarudi nyuma wakishindwa kujitoa basi mafanikio hayawezi kupatikana. Pia, Denge alijitoa muhanga kwa kupanga mipango na kwenda kwenye nyumba ya inspekta Wright kupekua na kuchuka data muhimu jambo ambalo liliichanganya serikali ya kikoloni na lnspekta Wright.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Tazama mazungumzo kati ya Denge na Yasmini kuonyesha kwamba Denge amedhamiria kujitoa mhanga.
*Denge anamwambia Yasmini:*

*" Hii ni kazi ngumu, ina matatizo mengi*
*na inahitaji kujitolea muhanga na mimi ni*
*miongoni mwa hao waliojitolea mhanga,*
*kufa kupona, potelea mbali..." (uk. 145)*

Yasmini pia ameonyesha dhamira ya kujitoa mhanga kutokana na vuta n'kuvute ya kisiasa. Yasmini alikuwa ameshawishiwa na Koplo Matata shirikiane na polisi ili kumkata Denge. Koplo Matata alimpa karatasi yaliyoandikwa uchochezi iii ayaweke kwenye chumba cha Denge ili iwe njia ya kumkata. Makaratasi hayo yaliandikwa hivi:

*"Sisi makomonisti wa visiwa hivi tunaapa*
*kupindua serikali na siku hiyo tutamuua*
*sultani" (uk. 154).*

Yasmini badala ya kuweka karatasi hizo kwenye chumba denge kwa kificho bila Denge kujua ili polisi wa kikoloni wamkate,Yasmini alimkabidhi karatasi hizo Denge na kumwambia mambo yote waliyozungumza na Koplo Matata, na Denge akachukua tahadhari.

*"Waliingia ndani na baada ya kuingia*
*tu Yasmini alimkabidhi Denge yale*
*makaratasi. "Koplo Matata kaniambia*
*niyalete kwako lakini wewe usijue kama*
*nimeyaleta" (uk. 154).*

Kitendo alichokifanya Yasmini ni cha kujitoa mhanga kunusuru maisha ya Denge na kunusuru harakati za mapambano.kusaliti Makubaliano na polisi tena wa kikoloni ni kujiota mhanga Ina maana Yasmini alikuwa tayari kwa lolote kutoka kwa polisi maana hakujali kukamatwa au kuchukuliwa hatua yeyote na polisi Ikizingatia wanamjua kwa kila kitu.

Mambo naye alijitoa mhanga kupeleka karatasi bandarini ili zisafirishwe kwenda Pemba kwa ajili ya kuwahamasisha wananchi wapiganie na kudai uhuru wao. Karatasi zenyewe zilikuwazimeandikwa hivi;

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*"Kufa au kupona tunataka uhuru"*

*"Ndiyo, kufa au kupona tunataka uhuru..." (uk. 186)*

Karatasi hizo zilitakiwa zibandikwe nchi nzima, Unguja na Pemba. Mambo alichukua karatasi hizo bila kuogopa ili kuzipeleka melini kwa kijana mmoja ambaye alizisafirisha kwenda Pemba. Mambo alifanya kazi ya hatari, maana bandarini kulikuwa na ulinzi na angeweza kushikwa na kuchukuliwa hatua, lakini alisukumwa na moyo wa uzalendo kuendesha mapambano hadi uhuru upatikane. Msanii anasimulia:

*"Ilipofika saa mbili za usiku Mambo akawa*
*yumo safarini anakwenda gatini, wasiwasi*
*umemjaa lakini kila akifikiri imani aliyekuwa*
*nayo kwa Denge wasiwasi ulimpungua."(k. 187).*

Maelezo hayo yanayoonyesha namna gani Mambo alikua amejitolea kufanya kazi ya hatari alimradi harakati za mapambano zisonge mbele.

**iii. Ushirikiano katika harakati za kudai uhuru kwenye jamii**

Kushirikiana katika harakati za kudai uhuru dhidi ya dhuluma ni dhamira iliyoshughulikiwa na msanii katika kuijenga dhamira kuu ya mapambano. Dhamira hii imeshughulikiwa na wasanii mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili na Afrika kwa ujumla Kwa mfano msanii mkongwe Marehemu Saadani Kandoro katika diwani yake ya "Mashairi ya Saadan" katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika alitunga mashairi yaliyokuwa yakiwataka wananchi wawe na umoja na mshikamano katika kupigania uhuru, mfano shairi la "Waafrika Njooni." Liliwataka wananchi wajitokeze kukiunga mkono chama cha TANU katika kupigania uhuru. Wanyonge na wanaodhulumiwa wanatakiwa waungane pamoja wawe na nguvu moja katika kupigania haki zao.

Shafi Adamu Shafi katika Vuta n'kute ameishughulikia dhamira hii kwa kumuonyesha Denge na kikundi chake jinsi walivyookuwa na ushirikiano katika harakati zao za kupambana na wakoloni wa Kiingereza. Denge , Mambo, Sikutuwa, Chande, Husein, Mwajuma, Yasmini, Zanga, Pazi wameonyesha umoja na mshikamano wa hali ya juu katika kuendesha harakati zakupambana na ukoloni.

Wameshirikiana katika kusafirisha na kusambaza karatasi za kuwamasisha wananchi kudai uhuru (uk. 187), Wameonyesha ushirikiano

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kumuokoa Denge asikamatwe na polisi kutokana na mtego uliowekwa na polisi wa kumtumia Yasmini kuweka karatasi za uchochezi ndani ya chumba cha Denge. Mambo, Chande na yasmini walishirikiana wakazichoma moto zile karatasi za uchochezi, Denge akaondoka na Chande akaenda kulala kwenye chumba cha Denge, ambapo polisi walipofika katika chumba hicho Denge walikosa kidhibiti na kuondoka zao (uk. 159). Katika kuonyesha vijana hawa walikuwa wana umoja na mshikamano tazama mazungumzo kati ya Chande na Denge.

*"Wakifiri hivyo n'do barabara, lazima wajue kwamba hakuna hata mtu mmoja katika nchi hii ambaye yuko pamoja nao, lazima sasa waelewe kwamba Denge huko peke yako." (uk.156)*

Maelezo yanaonyesha Denge katika harakati za kupambana na wakoloni hayuko peke yake, kuna watu wengie wanashirikiana na ndio ushirikiano unaotakiwa katika kuendesha mapambano ya dhuluma.

Pia ameizungumzia dhamira hii kwa kuonyesha ushirikiano waliokuwanao wafanyakazi katika kulaani ukoloni. Siku ya Mei mosi walibeba vitambaa na mabango yaliyoandikwa kwa maneno ya kuhimiza kuungana kwa wafanyakazi kulaani ukoloni (uk. 139). Kwa hiyo msanii anasisitiza umoja unahitajika katika makundi yote ya kijamii ili kufanikisha mapambano dhidi ya dhuluma. Msanii anaonyesha wanyonge kokote walipo, lazima waungane na washirikianekupinga dhuluma. Tazama mazungumzo denge

*"Mia moja" Denge alishangaa, "Vijana kama mimi na zaidi yangu mimi wapo zaidi ya alfu moja, wapo ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar. Kila mmoja wao ana mchango wake anaotoa katika kufanikisha mapambano yetu...." (uk.113).*

Maelezo hayo yanaonyesha kuwa akina Denge walifanya harakati zao kwa umoja na ushirikiano mkubwa ndani na nje ya Zanzibar. Na huo ndio umoja na ushirikiano anaouonyesha msanii katika riwaya yake hii.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## (iv) Mbinu/Mikakati ya Kuyaendea Mambo katika jamii

Suala la mbinu, mikakati, mipango kwa ajili ya kuyaendea mambo mbalimbali, mfano mapambano limeshughulikiwa na msanii. Shafi A. Shafi anaelimisha jamii kuwa utekelezaji wa jambo lolote lazima lipangiwe mikakati na sio kujiendea ovyo. Denge na kikundi chake wameonesha mbinu na mikakati mbalimbali waliokuwa wakiipanga na kuifanya katika harakati zao za kupambana na ukoloni wa Kiingereza.

Katika harakati zao za mapambano, akina Denge walitumia mbinu mbalimbali, miongoni mwao ni: Kusambaza karatasi vitabu vya kuihamasisha jamii kupigania uhuru. Walifanikiwa kusafirisha na kusambaza na kuyabandika karatasi katika Unguja na Pemba kwa siku moja, jambo ambalo liliichanganya serikali ya kikoloni chini ya Inspekta Wright (uk.189).

Chande na Hussein walipanga mbinu ya kumuokoa Denge asikamatwe na polisi baada ya polisi kumuwekea mtego Denge kumuingizia karatasi ya uchochezi chumbani mwake ili akamatwe. Denge alipangiwa mpango akaondoka, chumba cha Denge kikasafishwa, siku hiyo Chande alilala katika chumba cha Denge, Polisi walipofika kumkamata (Denge) hawakumkuta badala yake walimkuta Chande na karatasi walizozitarajia hawakuziona chumbani mle. (uk. 159).

Bukheti, Mambo, Yasmini na Fikirini walipanga mbinu ya kumtoa gerezani Denge alikokuwa amefungwa na wakafanikiwa. na Bukheti na Mambo wakafanikiwa kumtoa Denge toka gerezani kumsafirisha ughaibuni ambako alikwenda kuendelea na harakati za kudai uhuru (uk. 240 - 244).

Mwandishi ametuonyesha mbinu nyingine aliyotumia katika harakati zao za kupambana na ukoloni ni Denge alijibadili sura ili kukwepa kukamatwa na polisi.

*"Denge hakuwa na wasiwasi wowote,*
*kwani alikuwa na hakika kwamba hakuna*
*mtu yoyote atakayeweza kumtambua kwa*
*jinsi alivyobadilika.Uso wake ulizungukwa na*
*sharafa ya ndevu zilizoungana na nywele*
*kubwa zilizochanwa vizuri*
*zikapasuliwa njia upande wa kushoto.*

*Miwani myeusi iliyofunika macho yake*
*yakawa hayaonekani..." (uk. 173)*

Mbinu hii ilimfanya Denge aweze kutua uwanja wa ndege Zanzibar akitokea ughaibuni bila kujulikana na hakuweza kukamatwa mpaka akafika nyumbani kwake, na akaendelea na harakati za kudai uhuru. Katika ukurasa 113 msanii anaonesha ni jinsi gani kina Denge waliendesha mapambano yao kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo ziliwasumbua na kuwanyima raha wakoloni. Tazama maelezo haya:

*"Siku tunaleta magazeti au vitabu*
*hawawezi kutugundua hata kidogo, kwani*
*wana mbinu gani zilizokuwa za ubingwa*
*zaidi hata tusiweze kuzipiku? Tushaingiza*
*vitu vingapi bila ya kukamatwa navyo?*
*tushatorosha vijana wangapi waliokataa kuwapa paspoti na sasa wako nje*
*wanasoma? (uk. 113)*

Maelezo hayo yanayoonyesha kwamba katika harakati za kupigania au kupambana na dhuluma lazima wapambanaji wawe na mbinu na mikakati mbalimbali katika kuziendea hizo haraka iwezekanavyo hawatafanikiwa.

## (v) Uongozi mbaya katika jamii

Suala la uongozi mbaya limeshughulikiwa na Shafi Adam Shafi kama ambavyo waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili wanavyolizungumzia katika mitazamo mbalimbali. Mara nyingi uongozi mbaya huelezewa kuwa ni ule unaokandamiza, kunyanyasa, kudhulumu na unajihusisha na ufisadi na ulaji rushwa. Mwandishi wa Vuta n'kuvute amelishughulikia suala hili kwa kuonyesha uongozi mbaya wa serikali ya kikoloni dhidi ya wananchi wa Zanzibar na Bara zima la Afrika.

Mwandishi ameonyesha pamoja na dhulurna nyengine ambazo hufanywa na uongozi mbaya, amegusia jambo moja ambalo uongozi wowote mbaya huwa unalifanya ambalo ni hila na visingizio kwa raia.

Shafi Adam Shafi ameonyesha jinsi uongozi mbaya unavyoweza kuongoza kwa kutumia hila na uongo kwa kuwazushia raia ili iweze kuwaadhibu.Katika riwaya hii, serikali ya kikoloni kupitia jeshi la polisi inatumia hila kumsingizia Denge kuwa ni komonist, hamjui Mungu na

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

anataka kumuua sultani, ili waweze kumkamata Denge na kumtia gerezani asiendelee na harakati za kupigania uhuru. Tazamamaelezo haya:

*"furaha ilioje aliyokuwa nayo Inspekta siku ile, kwani kwa visingizio tu, yeye alikuwa navyo vingi na kisingiziocha kumkamata Denge yeye hakitompa shida (uk. 153).*

Maelezo hayo ya Inspekta Wright yanathibitisha ni kwa jinsi gani uongozi mbaya na wa kidhalimu huongoza kwa hila na wasingizia raia wema mambo mbalimbali ili kuweza kuwatisha na kuwadhibiti. Uongozi mbovu kama huu ndio unaoifanya dunia leo kuwepo na machafuko ya mara kwa mara. Dunia haina amani kutokana na uongozi unaoongoza kwa hila na visingizio.

Inspekta Wright alimzuishia Denge kwa kuandika vikaratasi vya uchochezi na kumpa Koplo Matata avipeleke nyumbani kwa Denge bila yeye (Denge) kuwa na habari halafu askari wafanye upekuzi kwenye hicho chumba na Denge akamatwe.vikaratasi alivyokuwa ameviandika Inspekta Wright kwa ajili ya kumsingizia Denge viliandikwa hivi:

*"Sisi makomonist wa visiwa hivi tunaapa kuipindua serikali na siku hiyo tutamuua Sultani" (uk. 154).*

Maneno yaliyoandikwa kwenye vikaratasi hivyo vilivyoandikwa na Inspekta Wright yalikuwa ya kumchonganisha Denge na serikali na jamii kwa ujumla. Denge aonekane mtu mbaya, muuaji na anayetaka kupindua serikali hivyo iwe halali vyombo vya dola kumdhibiti na jamii inayomzunguka isimuhurumie na kumuona hafai. Tazama maelezo haya yaDenge:

*"Ukisema kweli wewe komonist. Ukipinga kutawaliwa wewe koministi. Lolote utakalolifanya madhali halina maslahi kwao basi wewe kominist. Mau Mau wa Kenya wameitwa komonisti, wapigania uhuru wa Algeria wameitwa makominist. Kila anayedai haki kwao ni koministi, na sumu yao kubwa wanayoitumia ya kutaka kuwiitenganisha watu kama hao na wananchi wenzao ni kusema kwamba watu hao wanaowaita makomunist hawaamini Mungu" (uk. 68).*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Maelezo hayo yanaonesha namna gani uongozi mbaya unavyoweza kuzua visingizio kwa raia wake kwa lengo unavyoweza kuwatenganisha raia wanaowazulia visingizio na raia wenzao na wasiweze kupata msaada toka kwa raia wenzao na waonekane hawafai ndani ya jamii ili serikali itakapowadhibiti raia iliyowawekea visingizio raia wengine waone ni sawa kwa wenzio kutendewa hivyo. Kwa hiyo mwandishi anaitahadharisha jamii iwe macho na uongozi wa namna hii, wachunguze kwa makini kila kauli ilivyotolewa na serikali dhidi ya raia au kundi fulani ndani ya jamii,, vinginevyo uongozi wenye hila na visingizio utakuwa unasingizia raia wema na jamii ikawaona raia hao hawafai kumbe ni kwa maslaihi ya uongozi ni si kwa wananchi.

**(vi)ubaguzi katika huduma za jamii ndani ya nchi**

Dhamira nyingine inayotokana na vuta n'kuvute za kisasa aliyeshughalikia msanii ni ubaguzi. Siasa za kikoloni chini ya inspecta Wright zilikuwa zinatofautiana na siasa za akina Denge na raia wa Unguja waliokuwa wanapinga na kupambanana ukoloni. Kutokana na mvutano huo, serikali ya kikoloni iliwabagua waafrika na kuweka sera za kibaguzi. Ubaguzi ulionyeshwa katika huduma za kijamii na sehemu za starehe. Kulikuwa na kumbi starehe ambazo ziliendeshwa kwa misingi ya ubaguzi. Ukumbi wa english Club ulikuwa ukitumiwa na Wazungu na watu watu wa hadhiya juu. "Karimjee Club' ni ukumbi uliokuwa unatumika na watu wenye asili ya Kihindi, na sehemu zote hizo Waafrika hawakuruhusiwakuingia kwenda kustarehe kwenye kumbi hizo. Kumbi za Waafrika walizokuwa wakitumia kustarehe ni kama mwewembetanga, kwa Mzee Kiroboto, sehemu ambazo zilikuwa duni kukiuzwa pombe za kienyeji na fujo nyingi.

Pia kuna ubaguzi katika ajira. Denge anabaguliwakutokana na kwamba yeye (Denge) amesomea Urusi nchi ya kikomunist ambayo inapingana kiitikadi na siasa za Uingeleza serikaliya kikoloni ya Kiingereza ilimbagua Denge katika ajira kwa kumuona ni komunisti hivyo haendani na itikadi za kibepali matokeo yake Denge alikosa ajira pamoja na elimu aliyokuwa nayo abaki akiishi katika hali ngumu. Hata katika jeshi la polisi la koloni kulikuwa na ubaguzi. Wazungu ndio waliokuwa na vyeo a juu mfano Inspekta Wright na Waafrika walikuwa katika azi za chini mfano Koplo Matata.

**(vii) Uvunjaji wa Haki za Binadamu katika jamii**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Suala la uvunjaji wa haki za binadamu limeshughulikiwa na Shafi Adamu Shafi. Mwandishi ameonyesha ni jinsi gani serikali kupitia vyombo vya dola kama polisi na magereza zinavyo dhalilisha utu wa binadamu. Polisi na Magereza zina kanuni na sheria azowaongoza katika kukamata wahalifu na kuchunguza wafungwa wakiwa gerezani. Lakini vyombo hivi vimekuwa mstari wa mbele katika kuvunja haki za binadamu.

Kwa mfano, Denge alivamiwa usiku nyumbani kwake askari wakiongozwa na Inspekta Wright, ambapo askari aliusukuma mlango, Denge alipofungua mlango, akiwa amevaa chupi tu akapigwa kofi na Inspekta, kabla hajakaa sawa akapigwa kofi jingine akabebwa kitikiti na kutupwa ndani ya gari (uk. 191). jambo hili ni uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu. Denge alipofikishwa kituo cha polisi aliamrishwa avue nguo.

*"Vua nguo!" askari mmoja alimwamrisha Denge.*
*"Nakwambia vua nguo" aliamrisha tena yule askari"*

denge ikabidi atii ale amri, akavua chupi na kubaki uchi. Yule askari alimgeuza geuza akamwambia tena

*"Vaa nguo zako" (uk. 191)*

Kumkamata mtu akiwa na nguo ya ndani tu ni kuvunja haki zabinadamu. Kitendo cha askari wawili kumpiga makofi Denge ni uvunjaji wa haki za binadamu. Kitendo cha askari kumuamuru denge avue nguo na kubaki uchi kama alivyozaliwa ni udhalilishaji mkubwa na uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu. mwandishi anaionyesha jamii ni jinsi gani vyombo vya dola vinavyokiuka haki binadamu.

Vile vile mwandishi ameonyesha jinsi gani walinzi wa (askari magereza) wanavyokiuka sheria na kuvunja haki za binadamu Tazama jinsi walinzi wa jela walivyomdhalilis mfungwa mmoja ndani ya jela:

*"Wakaingia walinzi wa jela wanne waliombeba mfungwa mmoja kitikiti na marungu yao mkononi. Walimtupa chini wakaanza kumpiga marungu bila yahuruma wala kujali kama yule wamtesae ni kiumbe mwenzao. Mlinzi mmoja alimpiga teke la kiunoni, mwingine akamkanyaga shingoni, mwingine akamtandika rungu tumboni.*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Mfungwa yule alipiga kelele mpaka nguvu*
*zikamuishia akabaki kukoroma kama*
*anayekata roho (uk.234)*

Maelezo hayo yanazidi kuthibitisha uvunjifu wa haki za binadamuunufanywa na vyombo vya dola. Sidhani kama kuna sheria ya askari wanne kwa pamoja kumshambulia kwa marungu na mateke mfungwa hasa akiwa chini ya himaya yao. Huo ni uvunjaji wa haki za binadamu. Binadamu hastahili kushambuliwa namna ile,

pia anaonyesha mazingira wanayoishi wafungwa ndani ya magereza ni ya udhalilishaji na uvunjaji wa haki za binadamu, Mwandishi anasimulia mazingira wanayoishi wafungwa

*"Chumbani mle mhjaa harufu ya uvundo.*
*Mlikuwa na virago vilivyokunjwa upande*
*mmoja vitano na upande mwingine vitano*
*au pembeni kabisa palikuwa na ndoo....*
*lakini alipoikaribia harufu ya uvundo*
*ilizidi na ndoo ile ilikuwa tupu (uk. 192)*

Maelezo hayo yanaonyesha namna gani wafungwa Wailopokuwa gerezani wanaiShi katika mazingira mabovu, hakuna Vitanda wala magodoro, sehemu ya kujisaidia ni humo humo wanamolala Huku ni kuvunja haki za binadamu.

Pia Denge alipokuwa gerezani aliingizwa kwenye chumba chenye giza akavuliwa nguo zote akawa uchi, chumba hicho kina·joto mchana kutwa na baridi kali sana wakati wa usiku jambo lililomfanya Denge aishi katika hali ngumu sana (uk. 236).

Kwa ujumla msanii anataka kuonyesha jamii ni jinsi gani vyombo vya dola vinavyotumia mamlaka yao vibaya kuvunja haki za binadamu.

## VUTA N'KUVUTE ZA KIJAMII

Katika riwaya hii vuta n'kuvute za kijamii zimeshughulikiwa na msanii. Mambo ya kijamii ni yale yanayohusu mahusiano, ndoa, mapenzi, urafiki, ujirani n.k. Msanii kaonyesha vuta n'kuvute ya marafiki..wawili, Yasmini na Mwajuma, vuta n'kutuve kati wanandoa Mzee Raza na Yasmini, Vuta n'kuvute kati ya Shihabu Yasmini na Vuta n'kuvute kati ya wapenzi wawili

Bukheti na yasmini; Pia msomaji anaweza kufanya utafiti na kupata vuta n'kuvute nyingine za kijamii. Katika vuta n'kuvute hizi za kijamii zinazoelezea ndani ya kitabu, zimeweza kualibua dhamira zifuatazo: ndoa za lazima / Mapenzi ya lazima, Mapenzi ya dhati, Wivu katikandoa, Ukandamizaji wa mwanamke na Usaliti katika ndoa.

## (i) ndoa za Lazima katika jamii

Suala la ndoa za kulazimisha limeshughulikiwa na mwadishi kwa kuonyesha ndoa kati ya Yasmini na Mzee Raza. ni alilazimishwa na wazazi wake aolewe na Mzee Raza. Ndio a ndani ya ndoa yao hakukuwa na amani, ndoa yao haikuwa na kila siku ndani ya nyumba kulikuwa na malumbano. Ndoa yao kulazimishwa ilikuwa ya vuta n'kuvute. Tazama jinsi ndoa hii ya ilivyokuwa ya vuta n'kuvute.

1. *"Usinikere Bwana mimi nataka kulala"*
*"Mbona unalala mapema? N'do kwanza saa mbili. Amka tuzungumze,*
*"Bwana Raza alinguruma, Yasmini alimpuuza akalala" (uk.3).*

2. *Kutokumpenda Bwana Raza pamoja na utumishi wa kutwa dukani pake kulimfanya Yasmini ayachukie maisha ya unyumba na mumewe" (uk. 2)*

3. *"Bwana Raza hakuwa na raha ya kuwa na mke na Yasmini ya kuwa na mume. Maisha ya watu wawili hawa yalikuwa ya bahati nasibu na hakuwa mmoja kati yao aliyekuwa na raha " (uk.4)*

Maelezo yote hayo yanaonyesha ndoa kati ya Yasmini na bwana raza haikuwa na amani, raha wala starehe. Na hii yote ni kwasababu bwana Raza alilazimisha kumuoa Yasmini, binti mdogo mwenye umri wa miaka 15 ambaye hakumpenda kabisa bwana raza aliyekuwa na umri wa miaka 52.

## (ii)Mapenzl ya Dhati katika jamii

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Suala la mapenzi ya dhati limeshughulikiwa pia na Shafi adamu Shafi, Yasmini alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Denge alimpenda sana Denge kwa kuwa alikuwa kijana mwenzie, mchapakazi na mpambanaji. Hakujali hali ya kimaisha aliyokuwa kuwanayo denge alikuwa masikini, hana kazi, anaishi katika chumba kimoja ambacho kila siku kilikuwa kichafu. Yote haya Yasmini haku hakujali bali alionyesha mapenzi ya ukweli kwa Denge. Malumbano hatimaye kupigana kati ya Yasmini na rafiki yake Mwajuma.kuonyesha jinsi gani Yasmini alivyokuwa na mapenzi ya dhati kwa Denge. Mwajuma alijaribu kumshawishi Yasmini akukubali kuolewa na shilab bin antar na hapo ugomvi ndipo ulipo ibuka maneno ya Mwajuma.

*"Aaam babu we! Denge, Denge, unafikiri*
*Denge atakupa nini, mtu mwenyewe hohe hahe,*
*matatizo matupu, heshi kuandamwa na*
*maaskari utafikiri mwizi." (uk.169)*

Maelezo hayo ni maneno ya Mwajuma akimshawishi yasmini aachane na Denge na akubali kuolewa na Shihab.sikiliza majibu ya Yasmini:

*"Lakini si mwizi"Yasmini aliyadakia maneno.*
*"Wanamwonea tu, na mimi mwenyewe*
*nimehakikisha kama wanamwonea."*
*(uk.169)*

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi Yasmini alivyokuwa na huruma na Denge na jinsi anavyompenda Yasmini anaendelea:

*"Mwajuma usikasirike,tuombe*
*Mungu anijaaliye niijifungue salama*
*na hata wakati huo naamini*
*Denge atakuwa amekwisharudi,*
*popote pale atakapokwenda,*
*nitamshauri nimsikilize ataniambia nini (uk. 170).*

Tazama majibu ya Mwajuma:

*"Na weye nawe na Denge wako, kila*
*uambiwalo,Denge, Denge, unafikiri Denge*
*atakupa nini?Yeye mwenyewe hana*
*mbele hana nyuma,riziki inakuja hivi*

*hivi unaipiga teke,na kama hukuolewa sasa unafikiri utaolewa lini?Mwajuma alimkaripia utafikiri mtoto mdogo."*
*(uk.170)*

Mwajuma anamkasirikia Yasmini kwa kuonyesha msimamo wake wa kumpenda kwa dhati Denge hivyo kwa nini akatae kuolewa na bahati imefika?

Kwa upande mwingine, hata Mwajuma anaonesha ana mapenzi ya dhati kwa Yasmini. Mwajuma anaumia, anamuonea huruma Yasmini, bahati ya kuolewa imepatikana kwa nini rafiki yake kipenzi asiolewe akaondokana na ujane na dhiki alizokuwa nazo? tazama maneno ya Mwajuma:

*"Yasmini utaishi mjane mpaka lini?*
*kupata mwanamume akataka kukuoa si rahisi siku hizi.*
*Unafikiri mimi! mwenyewe napenda kuishi kama hivi ninavyoishi?*
*Natamani na mimi ningelikuwa na mume wangu....(uk.170).*

Maelezo hayo yanaonyesha Mwajuma alikuwa akimuhurumia rafiki yake, hakutaka rafiki yake aendelee kuishi maisha ya ujane na dhiki kama zile, ndio maana alikasirika kwa uchungu kuona rafiki yake amepata bahati na kutaka kuichezea.

Pamoja na malumbano hayo marafiki hawa walipatana na kuonesha kuwa wana mapenzi ya dhati na baadaye Yasmin akaolewa na Shihab. Hata Yasmini alipoolewa na Shibah alikuwa bado anamkumbuka Denge.

Mapenzi ya dhati mengine yameonyeshwa kwa Denge na kundi lake kuipenda nchi yao na kuanza harakati za kupambana na wakoloni ili kupatikane uhuru wa kweli wa wananchi wa Zanzibar pia vuta n`kuvute kati ya Bakheti na Yasmini inaonyesha mapenzi ya dhati ya yasmini kwa denge(uk231)

Pia Bukheti alikuwa na mapenzi ya dhati kwa yasmini bukheti alisafiri mara mbili toka Mombasa kwenda Unganda kumfatilia Yasmini. Bukheti alikubali masharti yote aliyopewa na yasmini ili amuoe likiwemo la kumtoa Denge gerezani, wakati alikuwa akijua yasmini na Denge walikuwa na uhusiano.

## (iii)Wivu katika Ndoa kwenye jamii

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mwandishi pia amezungumzia suala la wivu katika ndoa Wivu katika ndoa ni chachu ya ndoa lakini wivu ukizidi sana huleta madhala ndani ya ndoa. Ndoa ya Shihab na Yasmini imetawaliwa na wivu wa kupindukia kiasi ambacho raha ya ndoa miongoni mwa wana ndoa hawa ikakosekana. Shihabu mume wa Yasmini alikuwa na wivu sana. Mwandishi anasema:

*"Wivu wa Shihab ulikuwa ni ila yake kubwa aliyoijua kila mwanamke mjini Tanga na kwa sababu ya wivu wake huo, alikwisha waacha wanawake watatu na Yasmini sasa ni mke wake wa nne......Alimpa kila starehe ila uhuru wa kutoka, na starehe zake ziliishia ndani ya nyumba yake kubwa iliyokuwa na kila aina ya anasa ndani yake, zote asizione kitu, kubwa akawa aning'inia madirishani..."(uk. 197).*

Maelezo hayo yanaonyesha Shihab alivyokuwa na wivu wa kupindikia na tabia yake hiyo ilimfanya ashindwe kuishi na nawake, alikwisha aachana na wanawake watatu kutokana na tabia yake ya wivu. Kutokana na wivu wa kupindukia wa Shihab, yasmini alinyimwa uhuru wa kutoka nje hadi akakumbuka maisha yake ujane aliyokuwa akiishi na Mwajuma.

Kuhusiana na wivu aliokuwa nao Shihab:-

*"Nisikonde! Mwanaume yule! Ana wivu, ana gubu, ana nongwa kama mwanamke" Yasmini alilalamika." Nakwambia kaniweka ndani kama mwari, hata huyo mwali ana afadhali, sina shoga , sina jirani, sina jamaa, mimi na ndani na ndani na mimi, siendi sirudi (uk. 211)*

Maelezo hayo yanaonyesha Shihab alikuwa mume mwenye wivu sana ambapo uliwanyima uhuru wake aliowaoa. Wivu wa kupindukia wa Shihab ndio ilikuwa chanzo cha kifo chake. (Uk. 15).

**(iv) Ukandamizaji wa Haki za Wanawake katika jamii**
Suala la ukiukwaji na ukandamizaji wa haki za wanawake ndani ya jamii limeshughulikiwa na msanii kupitia ndoa mbili, ambazo ni ndoa kati ya Bwana Raza na Yasmini na nyingine. shlhab na Yasmini. Suala la

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ukandamizaji haki za wanawake limezungumziwa sana na wanafasihi wa Kiswahili Ikiziingatiwa jamii imepitia na bado imo katika mfumo dume.

Shafi Adamu Shafi ameonyesha namna gani mwanamke aliyenyimwa haki kwa Yasmini kulazimishwa kuolewa na Raza , Yasmini hakupewa nafasi na uhuru wa kuolewa na mwanaume aliyempenda kwa dhati yake (uk. 1).

Pia bwana Raza kama mwanaume ndani ya nyumba alimtumikisha mkewe (Yasmini) kama mashine Jambo ambalo jamii nyingi za Kiafrika humfanya mwanamke ni chombo ulizalisliaji mall, na mwanaume ni mtu wa kufaidi matunda yallyozalisliwa na mke katika familia. Hali hii ni kumkandamiza Mwanamke. Yasmini alikuwa anatumika kutwa nzima dukani jambo ambalo hakulifurahia na kupelekea kuzidi kuichukia ndoa yao.

*"Kutompenda Bwana Raza pamoja*
*na uturnishi wa kutwa dukani pale*
*kulimfanya Yasmini ayachukia maisha ya*
*unyumba wake" (Uk.2)*

Bwana Raza alimfanya Yasmini ni mtumishi wa kwake, na si mke mwenye hadhi. Ndoa kati ya Shihab na Yasmini nayo inaonyesha jinsi mfumo dume unavyokandamiza kunyima haki za wanawake ndani ya familia. Shihab kama mume alimnyima uhuru mkewe wa kutoka nje ya nyumba, kuwasalimia watu wengine na hata kujishughulisha na shughuli nyingi kijiongezea kipato katika familia. Shihab alimlazimisha Yasmin akae ndani tu na hakuna ruhusa ya kutoka nje na alijisifia kitendoo hicho. Kumnyima uhuru mwanamke wa kutoka nje ya nyumba au kumfungia mwanamke asitoke ndani ya nyumba au kufungia mwanamke ndani ya nyumba ni ukiukaji wa haki wanawake ndani ya familia.

Yasmini pamoja na kuwa kwenye nyumba nzuri na inakila kitu, lakini alinyimwa uhuru, jambo ambalo lilimhuzunisha Soma maelezo haya:

*“Alijiona kama ndege aliyefungiwa tunduni*
*akapewa kila kitu isipokuwa uhuru wake*
*wa kuruka hewani....alihisi Shihab alikuwa*
*kama aliyemtupia mshipi, akaumeza*
*pamoja na ndoana, chambo na chubwi.*
*Sasa amenasa, ni mahabusu wake, si huru*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*tena wa kwenda apendako, na nyimbo
za taarabu ambazo alikuwa bingwa wa
kuziimba kwenye tafrija za chama cha
Cheusi Dawa sasa akawa anaziimba
chumbani tu na badala ya kumletea furaha
na msisimko sasa zikawa zinamletea
mawazo na simanzi..." (uk. 197).*

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi Shihab alivyomnyima uhuru mke wake hata akajiona kama mfungwa ndani ya mahabusu hali hiyo ilimfanya Yasmini aishi kwa majonzi makubwa. Jambo la kujiuliza kwa nini mwanamke ndio afungiwe ndani tu. Pamoja hayo *Yasmini aliyazoea maisha hayo ya kifungo:*
*"Taratibu Yasmini aliyazoea maisha ya utawa,
akawa mke wa nyumbani aliyewekwa akakaa,
akatulia na Shihabu akawa anajisifu kwa rafiki
zake wote" Safari hii nimepata mke" (uk. 198)*

Shihab kujisifu kuwa amepata mke hali anamfungia ndani na kunyima uhuru wa kutoka nje ni kumdhalilisha na kumkandamiza mkewe.

**(v) Usaliti katika Ndoa kwenye jamii**

Usaliti katika ndoa ni dhamira iliyoshughulikiwa na mwandishi. Jambo hii linajitokeza sana katika jamii tunamoishi. wanandoa katika jamii tunamoishi baadhi yao si waaminifu hivyo huzisaliti ndoa zao. Na usaliti katika ndoa unaweza kusababishwa na mambo mbalimbali, inawezekana miongoni mwa mambo hayo wa wivu.

Yasmini mke wa Shihab anasaliti ndoa yake, kumuaga mewe (Shihab) anakwenda Unguja kuwaangalia wazazi wake kumbe alikuwa anataka kwenda kumuona Denge mzazi mwenzie.

*“Yasmini alimshawishi mumewe akashawishika,
akawashika akalaghaika, akawa kama
aliyezugwa akaamini kabisa kwamba
anakwenda Unguja mara moja kuwaangalia wazee wake" (Uk. 210).*

Maelezo hayo yanaonyesha kuwa Yasmini alifanya usaliti kwa kumlaghaimume wake. Yasmini alipofika Unguja na kumkuta Denge, akahamia kabisa kwa Denge akaishi miezi miwili wakati ruhusa aliomba kwenda unguja mara moja na kurudi kwake tanga. Mwandishi anaeleza:

*siku ni usiku ule, usiku aliyolala na kuamka na Denge. Siku ya pili akahamia kwake akawa ni wa kupika na kupakua" (uk.214).*

Maelezo hayo yanaonyesha ni namna gani Yasmini alifanya usaliti ndani ya ndoa. Kumuacha mume wake Tanga alifika Unguja anaishi kinyumba na mume mwingine. Hata kama alikuwa na mapenzi ya kweli kwa Denge, maadamu aliolewa na mume mwingine (Shihab) hakuruhusiwa kufanya hivyo katika ndoa, jambo ambalo lilisababisha kifo cha mume wake bwana Shihab ambaye alifariki kwa kihoro.

**(c) VUTA N'KUVUTE ZA KIUTAMADUNI**

Kuna vuta n'kuvute za kiutamaduni ambazo zinaonyeshwa migongano baina ya tamaduni moja na tamaduni nyingine. mgongano kati ya utamaduni wa Kiafrika na wa Kihindi ,migongano kati ya utamaduni wa vijana na utamaduni wa ..., mfano kuna vuta n'kuvute kati ya Yasmini na wazazi wake. Vuta n'kuvute kati ya Bukheti na Bashiri. Vuta n'kuvute za kiutamaduni zimeweza kuibua dhamira zifuatazo: Kuchaguliwa mme Ubaguzi wa rangi na utii kwa wazazi.

**(I) Kuchaguliwa Mme/Mke katika jamii.**

Suala la vijana kuchaguliwa mke wa kuoa au mume wa kuolewa limeshughulikiwa na msanii wa riwaya hii. Utamaduni ulioje katika jamii nyingi hasa za Kiafrika ni wazazi kuwachagulia watoto wao wake au waume kwa ajili ya ndoa. Utamaduni huu ulishazoeleka lakini kwa sasa umeshapitwa na wakati na hivyo kusababisha migogoro ya kifamilia.

Wazazi wa Yasmini walimchagulia binti yao mume wa kumuoa, mume mwenyewe alikuwa na umri mkubwa ukilinganisha umri wa Yasmini. Yasmini hakuridhika na mume aliyechaguliwa na wazazi wake ndio maana ndoa yenyewe haikudumu. Yasmini aliondoka kwa Mzee Raza. Msanii anaeleza:

*"Mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasmini aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya lthanaashiria ambaye alikuwa akiishi jirani naye hapo Mtendeni."(uk.1)*

Maelezo hayo yanaonyesha wazazi wa Yasmini kutokana utamaduni uliojengeka walimchagulia binti yao mume ambaye yeye mwolewaji hakumpenda wala hakuridhika naye.

Yasmini baada a kushindwa kuishi na Bwana Raza na kurudi kwa wazazi wake, walimfukuza kwa kuwa alionekana amevunja mila na utamaduni wao. Tazama jinsi mjomba wake Yasmini alipomfukuza Yasmini nyumbani kwake baada ya kurudi unguja toka kwa Mzee Raza:

*"hapa palikuwa kwenu kabla hujaolewa.Sisi
tulikupa mume ili tupungukiwe na mzigo.
Sasa madhali umemkimbia mumeo, tafuta pa
kwenda" (uk. 18).*

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi wazazi walivyong'ang'ania utamaduni wa kuwachagulia watoto waume wa kuwaoa hata wao hawakuridhika. Yasmini hakuridhika kuchaguliwa mchumba.

"Yasmini hakupenda hata kidogo kuolewa na mume kama yule kwani yeye mwenyewe angelipenda sana kupata mume kijana kama yeye mwenyewe" uk.1)

Bashiri ami yake Bukheti anafuata utamaduni wa wazazi kuwachagulia watoto wake wa kuoa. Bukheti alikuwa amevutiwa na kumpenda yasmini hivyo aliamua kumchumbia na kumuoa awe mke wake Bukheti alipomwambia ami yake Bashiri kwamba amepata mchumba na anataka kumuoa, Bashiri alimkatalia nakumchagulia somoye ndiye awe mke wake. Kwa hiyo Bashiri na Bukheti walikuwa katika mgongano.Sikiliza majibu ya Bashiri kwa bukheti:

> *"Ndugu yako somoye yupo hapa kama
> mke kweli tutakuoza Somoye.
> Wacha mambo ya kwenda kutafuta maponjoro.."
> (uk.254)*

Maelezo hayo yanaonyesha utamaduni uliojengeka wa wazazi kuwachagulia wachumba watoto wao. Matar anapingana na mawazo ya Bashiri na Gulam, mjomba wake Yasmini, yeye wasichaguliwe wachumba. Tazama maneno ya matar;

*"huyu ami yako mpuuzi, hayajui mambo
leo Bashiri.Hajui kama siku hizi vijana
wanatafutana wenyewe.Kijana anatafuta
wake. N'do mnamwitaje vile siku hizi,gali
frendi sijui (uk. 259)*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Maelezo hayo ya Matar yanaonyesha kuwa utamaduni wa wazazi kuwachagulia watoto wao wake wa kuoa au waume wa kuwaoa umepitwa na wakati, hivyo wazazi wawape uhuru vijana wao bukheti hakukubaliana na wazo la ami yake na akamchumbia yasmini na kumuoa.

**ii Ubaguzi wa Rangi katika jamii**

Ubaguzi wa rangi ni dhamira iliyoshughulikiwa na mwandishi Kutokana na tofauti za kiutamaduni na rangi za watu ndani ya jamii wanaweza kubaguana. Jamii ya Wahindi na jamii ya waafrika wana mtuzamo wa kubaguana. Kwa mfano, Bashiri alitaka kumzuia Bukheti asimuoe Yasmini kwa kuwa Yasmini ni mhindi (mwenye asili ya Kihindi) ila amuoe Somoye ambaye ni ndugu yake na Mwafrika mwenzake. Tazama maelezo ya Bashiri:

> *"Ya nini kwenda kutafuta Wahindi mwanangu. Wewe una jamaa zako chungu nzima, kuukeni na kuumeni. Badala ya kumchukua jamaa yako ukamsitiri wewe unakwenda kutafuta Wahindi" (uk. 254).*

Maelezo hayo yanaonyesha ubaguzi, Bashiri anambagua yasmini kwa kuwa Yasmini ana asili ya Kihindi na Bashiri na nduguye ni Waafrika. Mama yake Yasmini anaonesha ubaguzi wa rangi a kumshutumu Yasmini kuwa anaishi na kushirikiana na aafrika. Kwa Mama Yasmini, mwanae kuishi na Waafrika ni kosa ni aibu kwa jamii ya Kihindi. Maneno ya mama Yasmini kwa mwanae:

*"Umekujisha kufenza nini hapa wewe mwanaharamuUmeacha Raza Mombasa umekujisha Zanzibar kufunzauhuni kutilisha sisi aibu, jamatini vatu ote nazungumza habari yako,nasema veve siku hizi nafuatana na golo. Toka toka kwenda zako..."(uk. 43).*

Maelezo hayo yanaonesha ubaguzi wa rangi waliyokuwa nayo jamii ya Kihindi dhidi ya jamii ya Kiafrika. Mama Yasmini na Jamatini wanamuona Yasmini amefanya jambo la aibu kabisa la kufuatana na "golo" yaani Waafrika. Huu ni ubaguzi.

Suluhisho la tatizo hili mwandishi ameonyesha jamii inatakiwa iishi bila kubaguana kama alivyoonyesha kwa Yasmini muhindi kuishi na Mwajuma

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

na kuwa na uhusiano na Denge pia aliolewa na Bukheti ambao wote hao ni Waafrika na hakuna tatizo lolote lililotokea. Pia Mzee Gulam, mjomba wake Yasmini alioa mke wa Kiafrika na hakukua na ubaya wowote.

**iii Utii kwa Wazazi katika jamii**

Jambo la kuwatii na kuheshimu wazazi limeshughulikiwa na mwandishi . Mwandishi anawataka watoto wawe na utii kwa wazazi wao wasionyeshe dharau kwa wazazi, hata kama kutotokosea mzazi, kafanya kosa basi mtoto anatakiwa awe mvumilivu na asionyeshe aina yoyote ile ya dharau mbele ya wazazi. Yasmini ni binti aliyeonyesha utii naheshima kwa wazazi wake, hakupinga mbele ya wazazi kuolewa na Mzee Raza mume aliyechaguliwa nao Yasmini anaonyesha hakumpenda wala hakumridhia mzee Raza kuwa mumewe bali hakutaka kuwaudhi wazazi wake. Tazama maneno haya:

*"kukubali kwake kuolewa ilikuwa ni kwa*
*sababu ya kuwaridhi wazazi wake tu.*
*Yeye mwenyewe hakuona fahari yoyote kuolewa*
*na mzee anayeweza kumzaa...."(uk.1)*

*"ah Yule alikuwa si mume wa kumtaka*
*Mimi mwenyewe, niliozeshwa tu na*
*wazee na mimi sikuweza kuwavunja..."(uk.23)*

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi Yasmini alivyokuwa na heshima kwa wazazi wake. Hakutaka kubishana na kuonyesha utovu wa nidhamu mbele ya wazazi. Hivyo, mwandishi kupitia yasmini anasisitizavijana kuwa na heshima kwa wazazi na watu wazima Kukosa adabu mbele ya wazazi kunasababisha na mmomonyoko wa maadili ambapo inaweza kuzalisha viongozi wasio na adabu na utii kwa wanaowaongoza. Msomaji anaweza kufanya utafitina kupata dhamira nyingine kama vile umasikini na hali ngumu ya maisha na nyinginezo.

**MIGOGORO KATIKA VUTA N'KUVUTE.**

Migogoro lmeonyeshwa mingi ndani ya riwaya hii, na hapo tutaeleza kwa ufupi migogoro michache tu:

kwanza, ni mgogoro kati ya Denge na serikali ya kikoloni chini ya idara ya polisi iliyokuwa ikiongozwa na Inspekta Wright. Denge pamoja na wenzake walikuwa wanapinga serikali ya kikoloni iliyokuwa chini ya Mwingereza katika visiwa vya Zanzibar yaani unguja na Pemba. Kwa mfano; mwandishi anadhihirisha mgogoro huu anaposema:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*Denge alikuwa ametulia kimya, ananisikiliza kwa makini kabisa kabisa. "Yasimini mimi najua kuwa unanipenda, na mimi nakupenda vile vile, lakini kuna kitu kimoja napenda uelewa, kuna mapenzi na wajibu wa mtu katika jamii. Kila mtu ana wajibu fulani katika jamii na mimi wajibu wangu mkubwa ni kufanya kila niwezalo kwa kushirkiana na wenzangu ambao wengine unawajua na wengine huwajui kuona nchi hii inakuwa huru. Hii ni kazi ngumu Ina matatizo mengi na inahitaji kujitolea muhanga kufa, kupona potelea mbali" uk 145.*

Pili, mgogoro kati ya Yasimini na wazazi wake (mjomba mama yake). Mgogoro huu ni wa kijamii ambapo wazazi wake yasmini walimlazimisha kuolewa na mzee Raza mwenye umri wa miaka 52. Yasmini alikubali kuolewa kwa sababu ya kulazimishwa na mwandishi anavyoeleza:-

*"Ah, yule alikuwa si mume wa kumtaka mimi mwenyewe niliozeshwa tu na wazee wangu na mimi sikuweza kuwa vunja" alisema Yasimini uk 23*

Tatu, mgogoro kati ya Yasimini na mzee Raza. Huu, pia ni mgogoro wa kijamii juu ya ndoa ya Yasimini na mume wake mzee raza kwa sababu Yasimini hakumpenda mume wake. Kwa hiyo ndoa hiyo ilikuwa katika mvutano na hatimaye ilivunjika. Kwa mfano mwandishi anasema:-

*usinikere bwana mimi nataka kulala"*
*mbona unalala mapema?*
*Ndo kwanza sasa mbili Amka tungumze" bwana Raza*
*aliunguruma Yasmini alimpuuzana kulala uk 3.*

Nne mgogoro kati ya Mwajuma na Yasimini. Mgogoro huu ulitokea pale Mwajuma alipokuwa akimshawishi Yasimini achane na Denge na aolewe na Shihab kijana wa Tanga. kwa mfano mwandishi anaeleza;

*Na weye na Denge wako kila uambiwalo,*
*Denge. Denge, unafikiri Denge kakupa nini?*
*" Yeye mwenyewe hana mbele h ana nyuma,*
*riziki inakuja hivi hivi unaipiga teke, na kama*
*hukuolewa sasa unafikiri utaolewa lini?*
*Mwajuma alimkaripia utafikiri mtoto mdogo.*
*Uk 170*

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Tano, mgogoro kati ya Yasimini na Shihab mume wake wa pili baada ya Raza. Mgogoro huu ulitokea kwa sababu ndoa ya Shihabu na Yasmini ilitawaliwa na wivu wa kupindukia kiasi kwamba Yasmini hakufurahia maisha ya ndoa kama ilivyotegemea.

Kwa mfano; mwandishi anaeleza:-

*“nisikonde! Mwanaume Yule ana wivu ana gubu, ana nongwa kama mwanamke” Yasmini alilalamika; nakwambia kaniweka ndani kama mwari sina jirani,sina jamaa, mimi na ndani na ndani na mimi siendi sirudi Uk 211.*

Sita ni Mgogoro kati ya Waafrika na Wahindi. Mgogoro huuvile vile ni wa kijamii kwa sababu Waafrika (waswahili) na wahindi wana mtazamo wa kubaguana kutokana na tofauti za kiutamaduni na rangi za watu ndani ya jamii inayoishi katika nchi moja. Kutokana na mgogoro huo wa kiubaguzi, wahindi wanawaita waswahili (wanfrika) GOLO na waswahili nao wanawaita wahindi MAPONJORO kwa mfano, juu ya wahindi mwandishi anasema;

*Umekujisha kufenza nini hapa wewe mwenaharamu,
umeacha Raza Mombasa umekujisha Zanzibar kufenza
uhuni kutilisha sisi aibu ote nzungumza habari yako,
nasema veve siku hizi nafatana na golo uk. 43*

Pia kwa upande wa Waswahili (Waafrika) mwandishi anasema:Badala ya kurnchukua jamaa yako ukamsitiri wewe unakwenda kutafuta wahindi" Bashiri aliweka kikombe cha kahawa barazaniameshangaa anamtazama Bukheti. Ndugu yako Somoye yupo ha pa. pia unataka mkwe kweli tutakuoza Somoye. Wacha mambo ya kwenda kutafuta Maponjoro. Unasemaje? uk. 254

Na saba ni mgogoro wa kinafsi waliokuwa nao Denge, Yasmini, Bukheti na Mwajuma. Kwa mfano, Yasmini ana mgogoro wa kinafsi kuhusiana na mambo kadhaa yanayomkabili. Yasmini ana mawazo kichwani kwake kuhusu mtafaruku aliokuwa nao wazazi wake, ana mawazo juu ya kifo cha mume wake Shihabu na amezongwa na majonzi ya kukamatwa mpenzi wake Denge,amezongwa na mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo juu ya Denge naye sasa yuko mikononi mwa vyombo vya dola na mwisho amezongwa na

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

hamu kubwa ya kumnusuru Denge. Huo ni mgogoro wa kinafsi aliokuwa nao Yasmini.

## Ujumbe

Baada ya kusoma riwaya hii unaweza kutoka na mafunzo mengi, baadhi ya mafunzo hayo ni:

1. Ushirikiano wenye upendo ambao umejikita katika misingi ya haki na usawa kwa kila mhusika ni jambo la msingi kabisa katika harakati za kuleta mabadiliko ndani ya jamii.

2.Ndoa ya lazima mara nyingi haiwezi kudumu.

Utamaduni wa wazazi kuwachagulia wachumba watoto wao umeshapitwa na wakati katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia.

3. Popote palipo na dhuluma na ukandamizaji mapambano nilazima yachukue nafasi ili kuondoa dhuluma hizo.

4. Ndoa huweza kudumu kwa watu waliochaguana na kuridhiana.

5. Penye nia daima pana njia

6. Suala la mapenzi ya kweli halichagui rangi, kabila au mali.

## Falsafa Ya Mwandishi

Mtazamo na msimamo wa mwandishi ni kuleta mabadiliko ndani ya jamii ambapo mabadiliko hayo yatafanikiwa kwa mapambano kama vile Denge alivyopambana, Yasmini alivyopambana na Bukheti alivyopambana.

## MATUMIZI YA VIPENGELE VYA FANI KATIKA VUTA N'KUVUTE

Shafi Adam Shafi katumia sanaa ya hali ya juu katika kuijenga kazi hii. Ndio maana riwaya hii ilipata tuzo wakati ba do ni mswada wa riwaya ya Kiswahili kabla hata haijachapishwa kwenye tamasha la vitabu la dar es salaam mwaka 1998. Kutokana na sanaa iliyotumika,inatia mvuto kwa msomaji anapoanza kukisoma asikiweke chini mpaka akimalize. Vipengele

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

vya fani vitakavyo shughulikiwa ni: muundo, mtindo, wahusika mandhari na matumizi ya lugha.

1. **Muundo**

Muundo tunaangalia kwa kuona jinsi gani mwandishi alivyosuka visa na matukio na namna gani kazipanga sura katika kitabu chake. muundo uliotumika katika riwaya hii kwa upande wa mfululizo wa visa namatukio ni wa moja kwa moja. Mwandishi anaanza kusimulia kisa cha Yasmini binti mwenye umri wa miaka 15 kuozeshwa kwa mzee mwenye umri wa miaka 52 kwa jina Mzee Raza. Binti anaamua kumkimbia Mzee Raza, anarudi nyumbani kwa wazazi wake, wazazi wake wanamfukuza, anaamua kwenda kuishi kwa rafiki yake Mwajuma huko anakutana na kijana mwenzake Denge ambaye alikuwa akiongoza harakakati za kupambana na wakoloni wa Kiingereza na kupendana naye hatimaye wakaazaanaye mtoto.

Denge kutukana na harakati zake alifungwa gerezeni yasmini akafunga ndoa na Shihab ambayo ilikuwa ndoa yake ya pili ndoa hii Ilitawaliwa na wivu wa kupindukia uliosababisha yasmini anyimwe uhuru na mumewe na kutokana na wivu shihab alifariki kwa kihoro. Mwisho Yasmini anafunga ndoa yake ya tatu kijana Mwafrika toka Mombasa na kuishi naye unguja kwa raha na starehe.

kwa upande wa mpangilio wa sura, riwaya imejengwa kwa sura kumi na nnekuanzia sura ya kwanza hadi sura ya kumi na nane na katika sura ya kumi na nane (18) mwisho kabisa kuna kishilizio alichokiita tamati katika ukurasa wa 274.

(ii) Mtindo

Mwandishi ametumia mtindo wa masimulizi ambao utumiwa takriban na waandishi wengi wa kazi za fasihi ya kiswahili. Katika mtindo huu mwandishi ndiye anayejua na simulia hadhira visa na matukio yote, kama vile anavyotusimulia visa na matukio yote yaliyofanywa na Yasmini na wahusika wengine. Pamoja na mtindo huu wa masimulizi (Monolojia).

Pia, mtindo wa barua ameutumia mwandishi pale Shihab alipomwandikia barua Yasmini ya kumueleza nia yake ya kutaka muoa (uk. 168). Barua nyingine ni ile iliyoandikwa na Yasmini kwenda kwa Denge iliyokuwa inaonyesha masikitiko aliyokuwa nayo Yasmini ya kuondoka Unguja na kumwacha Denge (uk.184).Vile vile mtindo wa dayalojia

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

umetumika pale mwandishi powapa nafasi wahusika wenyewe wazungumze kwa Thizana. Kwa mfano mazungumzo kati ya Mwajuma na Yasmini, mazungumzo kati ya Yasmini na Koplo Matata, Mazungumzo kati Denge na Yasmini, mazungumzo kati ya Denge na Mambo, mazungumzo kati ya Denge na Inspekta Wright, Mazungumzo kati Bukheti na Bashiri, mazungumzo kati ya Yasmini na Kalmar na zungumzo mengine mengi. Mazungumzo hayo yaliyofanywa wahusika ili kutajirisha maudhui.

Zaidi ni kwamba, kuna mtindo wa nyimbo. Mwandishi amemtumia Mwajuma; akifua huku akiimba:-

*Jamani ujana unanitoka,*
*Mfano wa jua linapotoweka,*
*Sasa wako wapi, walionitaka,*
*Uzuri hakika, kitu cha kukopa*
*Hakika ni kweli, nilibahashika*
*Kuringia kitu, kisichoenzika,*
*Mithili ya ua, ukishalikata*
*Uzuri hakika kitu cha kukopa. (uk. 85 - 86)*

(iii)**wahusika**

Mwandish amewatumia wahusika wengi kupaza sana yake hapo tutawadondoa wahusika wachache muhimu.

1. **Yasmini**

Binti wa kihindi kutoka jamii ya lthnashiria, aliyeku na umri wa miaka kumi na tano (15) wakati alipoolewa na Mzee raza alichaguliwa mume na wazazi wake aliyekuwa mzee mwenye umri wa miaka 52 na kuolewa naye. Alionyesha utii kwa wazizi wake kama binti mwenye maadili, heshima na adabu. Hakuridhika kuishi katika ndoa yake ya lazima, ambapo aliamua kuondoka kwa mzee raza na kuishikwa Mwajuma.

Anaonyesha mapenzi ya dhati kwa Denge. Anapinga mila na utamaduni wa kuchaguliwa mume. Anapinga mila na utamaduni na ubaguzi wa rangi ndio maana aliamua kuishi kwa Mwajuma ambapo ni mwafrika, pia alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Denge ambaye ni mwafrika na pia aliolewa na Bukheti ambaye alikuwa Mwafrika ni mwanamapinduzi ambaye alishirikiana na akina Denge kupambana katika harakati za kupambana na wakoloni wa Kiingereza huko Unguja ni mvumilivu na

asiyekata tamaa. Ni mhusika mviringo ambaye alimsaliti mume wake Shibab na kwenda kwa Denge mpenzi wakati alifunga ndoa na wanaume watatu kwa nyakati tofauti

2. **Denge**

kijana aliyeishi maisha ya ukapera. Alipata elimu ya juu katika nchi ya Urusi (nchi ya Kikomunisti). Pamoja na elimu yake ya juu aliyokuwa nayo alikosa ajira katika serikali ya kikoloni kutokana na chuki, Alikuwa mpenzi wa Yasmini hadi wakazaa mtoto

Denge ni kijana shupavu ambaye aliongoza harakati na mapambano dhidi ya serikali ya kikoloni. Alifungwa gerezani na kupata mateso makubwa kutokanana kuongoza harakati, za kudai uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza. Ni mchapakakazi mvumilivu na hakuwa mtu wa kukata tamaa. Alijitolea muhanga kwa hali na nafasi yake kupambana na wakoloni wa Kiingereza.

3. **Mzee Raza**

Mzee mwenye umri wa miaka 52 ambaye aliamua kumuoa binti mdogo mwenye umri wa miaka 15 sawa na mjukuu wake. Alikuwa mfanyabiashara. Alihamishia biashara zake toka Unguja kwenda Mombasa. Alitawaliwa na mfumo dume kwa kumtumikisha mkewe Yasmini. Kutokana na umri aliokuwa nao, alikimbiwa na mke wake.

4. **Gulam**

Mjomba wake Yasmini. Anatoka katika jamii ya lthnashiria. Alishirikiana na wazazi wa Yasmini kumuoza binti yao kwa Mzee Raza. Alimfukuza Yasmini nyumbani kwake kwa karaha kwakuwa Yasinini aliondoka kwa mume wake (Raza) kutokana na kushindwa kuishi na mume asiyempenda. Anafuata utamaduni wa kikale wa wazazi kuwachagulia watoto wao waume.

5. **Mama Yasmini**

Mama wa Kihindi kutoka jamii ya Ithnashiria Mama mzazi wa Yasmini. Anashiriki kumuozesha binti yake kwa Mzee Raza. Alimfukuza binti yake (Yasmini) nyumbani kwake kwa kuwa ondoka kwa mumewe Mzee Raza, Mume ambaye hakumpenda tokana na kuwa halikuwa chaguo lake. Ni

mbaguzi wa rangi - alimshutumu na kumlaumu mwanae (Yasmini) kwa nini anaishi a Waafrika. Hafai kuigwa na jamii.

6. **Matar**

Jina lake maarufu aliitwa Bwana Mashuguli. Alikuwa fanya biashara wa chupa tupu, pia alikuwa muuza genge Darajani. alifuatwa na Bukheti iii amsaidie kumshawishi Bashiri (baba yake dogo Buketi) amkubali kumuoa Yasmini na apeleke posa kwa Gulam ya kumuoa Yasmini. Alimkabili na kumweleza kweli. Anapingana na mawazo ya kale ya wazazi kuwachagulia achumba watoto wao. Anakubaliana kuwa vijana wapewe uhuru wa kuchagua wake wa kuwaoa au waume wa kuolewa nao.

7. **Koplo matata**

Mwafrika aliyekuwa anatumikia jeshi la polisi la kikolo anaunga mkono juhudi za wakoloni kuwakandamiza Waafrika wenzie anashirika kupanga njama za kumkamata Denge asiendeleze harakatiza kupambana na ukoloni. Ni msaliti wa kiafrika.

8. **Inspekta wright**

Ni mzungu kutoka Uingereza. Kiongozi wa ngazi za juu wa jeshi la kikoloni. Alikuwa jeuri, mkatili na muonezi ni hodari wa kupanga njama na kuwasingizia raia wasio na hatia ili wakamatwe na kutiwa nguvuni na jeshi la polisi. Alishirikiana kumwekea visingizio Denge kuwa kuchapisha vikarata vya uchochezi ili akamatwe na jeshi la polisi. Alishiriki kufuatilia harakati za akina denge hadi akamkata Denge na kupelekwa kufungwa gerezani Alitaka kumrubuni na kumshawishi Denge aachane na harakati za kudai uhuru kwa kumuahidi kumpatia cheo.

9. **Mwajuma**

mwanamke wa Kiafrika aliyeishi Unguja katika chumba chake bila mume Alikuwa rafiki kipenzi wa Yasmini. Alikuwa mwimbaji maarufu katika kikundi cha Cheusi Dawa. Alimpokea yasmini na kuish naye nyumbani kwake baada ya Yasmini kufukuzwa na wazazi wake kutokana na kuondoka kwa mume wake mzee raza. Anapenda starehe, hasa kunywa pombe na kucheza dansi Ana mapenzi ya dhati kwa Yasmini. Ni mvumilia na mwenye huruma. Alishiriki harakati za mapambano dhidi ya ukoloni , kwa kushirikiana na akina Denge na Mambo. Wahusika wengine walioshiriki ni

Mambo, Chande, Sefu, Sikutua, Karma Hussein na wengine wengi ambao wametumika kutajirisha maudhui.

**(IV)Mandhari**

Mandhari iliyo tumika kujenga riwaya hii ni mandhari inayopatikana ukanda wa juu wa afrika mashariki ambayo ni unguja Mombasa tanga na dare s salaam pia kumetajwa urusi mahali alikosomea Denge. Pamoja na miji hiyo, pia kuna mandhari ndogondogo ambazo zinaonyesha uhalisia wa maisha mwanadamu ya kila siku. Kuna mandhari ya chumba cha Denge, mandhari ya chumba cha Mwajuma, mandhari ya Darajani, mandhari ya gerezani, mandhari ya nyumba ya Matar, mandhari ya nyumbani kwa Inspekta Wright, mandhari ya Karimjee "club" mandhari ya English club, mandhari ya nyumbani kwa mzee Kiroboto, mandhari zote hizo kazitumia msanii katika kutajirisha maudhui yake.

**(V) MATUMIZI YA LUGHA**

Lugha ndiyo zana inayotumika kujengea sanaa ya fasihi. wa upande wa lugha mwandishi ametumia utaalamu na ufundi wa hali ya juu kiasi ambacho kuna mvuto wa hali ya juu kwa msomaji. mwandishi anajua namna ya kuyateua maneno na yakaendana na husika wake aliowapa wayaseme yakiambatana na vitendo.

Kwa ujumla kuna matumizi ya aina zote za lugha ndani riwaya hii. Kuna matumizi ya lugha sanifu, lugha isiyo sanifu, lugha ya mtaani, matone ya lahaja ya Kiunguja, lugha ya ucheshi, lugha kali (matusi) na matumizi ya tamathali za,semi, misemo na methali kadhaa, pia kuchanganya ndimi (amechanganya lugha). 'Lugha Sanifu

**1. LUGHA SANIFU**

Riwaya imetumia lugha sanifu ambayo inajulikana kwa watumiaji wote wa lugha ya Kiswahili.

**2. LUGHA ISIYO SANIFU**

Katika kurembesha na kuboresha kazi yake baadhi sehemu kuna matumizi ya lugha isiyo sanifu, yaani lugha inayokiuka kanuni za sarufi ya Kiswahili. Matumizi ya lugha isiyo sanifu wamepewa wahusika ambao si Waswahili

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

asilia na wenye asili ya kigeni ili kutajirisha maudhui. Mfano tazama lugha yotumia mama yake na Yasmini.

*"Umekujisha kufenza nini papa wewe mwenaharamu,*
*Umeacha Raza Mombasa umekujisha*
*Zanzibar kufenza uhuni katilisha sisi aibu.*
*Jamatini vatu ote na zungumza habari*
*yako..." (uk.43)*

maelezo hayo yote yanaonesha upoteshaji wa Sarufi ya Kiswahili kwa hiyo ni lugha isiyo sanifu. Tazama mfano mwingine toka kwa inspekta wright ambaye ni mzungu

"wewe iko hakika denge ndiyo naleta material hizi?"

Eleza mimi progress ya investigation yako kwa denge(uk.76) inspecka wright anaongea Kiswahili kisicho sanifu. Msanii amefanya hivi ilikuleta msisimko na kutajirisha maudhui yake. Msomaji anaweza kufanya utafiti na kugundua mahali pengine ambapo lugha isiyo sanifu imetumika.

## 3. LUGHA YA MTAANI.

Kuna matumizi ya maneno ya mtaani mfano barobaro(uk.13) alikuwa kijana barorbaro mwenye umbo……………

*" tazama ulivyokongoroka umebaki fremu tu"(uk.32)*
*"kijana mmoja aliyekuwa na "nishai" changachanga…."(uk.61)*

Ubela-ubela (uk.220)
Wacha mambo ya kwenda kutafuta "maponoro"(uk.254)
Mkweche wa kutupwa(uk.79)

## 4. MATONE YA LAHAJA YA KIUNGUJA

"chombo kikateremshwa pwani"(uk.225)

Akamkalia dagi (uk.257)

Amle,mbiza amle mboza?(uk.104)

Mkoko n`do kwanza ulikuwa ukichanua maua(uk.85)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Nabahashuka na wewe?(uk.170)

### 5. Lugha kali

Baadhi ya sehemu mwandishi katumia lugha kali isiyo na kificho

Mfano: tazama maelezo haya:

*"Alikuwa mtoto mrefu
mwembamba mwenye nywele
ndefu nyeusi ambazo alizitimua
zikateremka mpaka matakoni..."
(uk. 135).*

Neno, 'matakoni' ni lugha kali, ilihitaji kutumika tafsida

lugha kali Nyingine

mwenye laana weye kahaba mkubwa" (uk. 170).

**MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI**

Shafi Adamu Shafi ametumia tamathali za semi mbalimbali katika riwaya yake ya Vuta n'kuvute iii kutajirisha maudhui yake kwa jamii husika. Kutokana na wingi wa tamathali za semi zilizotumika, sisi tunabainisha ni wajibu wa walimu na wanafunzi kubainisha tamathali nyingine za semi kama vile tashihisi,takriri, tabaini, mubalagha na kejeli

Tashbiha ni mfananisho wa vitu viwili au zaidi. Mara nyingi tamathali hii hutambuliwa kutokana na matumizi ya maneno kama mwandishi wa vuta n'kuvute ametumia tashibiha mbalimbali. baadhi ya tashbiha zilizotumika katika riwaya ya vuta n'kuvute Jumamosi ikapeperuka kama kishada kilicho katika orjojo (uk14 ), Yasimini amechachamaa, amekuja juu kama moto wa kifuu (uk.15), Nimekwenda kwa mjomba, nimetimuliwa kama mbuzi. 19), Walibaki chumbani mle kimya kama mabubu (uk 25), salumu mbele Roger nyuma anafuata tu kama mkia (uk. 27), Pale pembeni amesimama kama mlingoti (uk 37), na watu wa nchi hiyo wafupi kama Athumani Kafupi (uk 53)

Pia mwandishi ametumia tashbiha zifuatazo;- Yasimini alichana nywele zake vizuri akazizongazonga na kuzifungia juu akawa kama sega la nyuki (uk 61), Jua liliwaka likawa kama moto 66), Alikuwa bado amekamatana

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kama aliyepakwa ulimbo (uk.75), Moyo wake ulikuwa kama uliotiwa kitanzi (uk 96).

Kwa mbali mwanga wa taa za jiji la Dar es salaam ulianza onekana kama jua la alfajiri linapoibuka kutoka baharini (uk 4), lnspekta Wright alikuwa mkali kama moto (uk 151) na alinong'ona peke yake kama mwendawazimu (uk 159).

Vile vile msanii ametumia tashibiha kama vile, komamanga ilikuwa inaelea, mpera kama bua (uk 272), Alizichana nywele zake zikawa kama mawimbi madogo madogo (uk 164), Alikuwa kama mwizi na wasi wasi ukamjaa, akahisi kama watu wote wanamshangilia yeye (uk 270), Alikurupuka kutoka ofisini kwake kama mtu aliyepandwa na pepo (uk 189),Wafungwa walitimka kutoka vyumbani mwao kama mbuzi waliofunguliwa kutoka zizini (uk. 263) walikuwa wanatazama tu kama majogoo walio kwenye Mapigano (uk 190), na ananukia kama jini (uk 249)

Zaidi ni kwamba mtunzi wa vuta n'kuvute ametumia tashibiha kama vile wafungwa wakawazongea kama inzi wanapouzonga mzoga (uk 195), Kwa ghafla ikaibuka kwa mbali kutoka mawinguni kidogo kama mwewe aliyechanua mbawa zake (uk.215)Maruirui tu yaliyozagaa mbele yake kama umande uliotanda (uk. 210)Unaendesha baiskeli kama mwendawazimu (uk.229) ukabaki kukoroma kama aliyekata roho (uk, 234)

**7. METHALI**

pia msanii ametumia methali nyingi, miongoni mwake ni

-Mwisho wa dhiki ni faraja (uk. 43)

-umdhaniaye ndiye kumbe siye (uk.59)

-Wagombanao hupatana (uk. 172)

-Maji ukiyavulia nguo, sasa lazima ayakoge (uk. 193)

-Kelele za mpangaji hazimkeri mwenye nyumba (uk.229)

Methali hizo na nyingine nyingi zimetumika kupamba kazi na kutajirisha maudhui

**8. KUCHANGANYA NDIMI/KUCHANGANYA LUGHA**

Mwandishi kachanganya lugha katika kazi hii. Baadhi· ya sehemu katumia lugha ya Kiingereza kutokana na mhusika wake aliyempa kutumia lugha hiyo ili kutajirisha maudhui. Pia mahali ametumia lugha ya Kiarabu. Mfano

Matumizi ya lugha ya Kiarabu: Yasmini na Mwajuma walipokuwa wanazungumza kuhusiana na askari kumtafuta Denge.Mwajuma alitumia maneno ya Kiarabu...." Allahu yaall (uk.66) ikiwa na maana Mungu ndiye anayejua kisa cha askari kumtafuta mtu huyo. Mahali pengine palipotumika lugha ya kiarabu

*"alhamdu lillahi rabbi-el - alamin" (uk. 81)*
*"La tamsak, mall n-nas" (uk. 212)*

Pia lugha ya Kiingereza imetumika, kwa kuwa baadhi ya wahusika ni Wazungu wa Kiingereza ambao walikuwa wanatawala zanzibar. Tazama mazungumzo kati ya kamishna wa polisi inspekta Wright.

*"Well" Alisema Kamishna na kuvunja kimya kilichokuwa ofisini mle*
*"The Situation is very grave!"*
*"Indeed Sir!, alijibu inspekta Wright.*
*"We must inform the British Resident"*
*We must Sir" (uk. 190)*

Pia mazungumzo ya inspekta Wright na Koplo Matata. inspekta Wright anasema:

*"Right now sit down"*
*The communies, we shall*
*give them hell, inspekta*
*Wright alisema (uk. 76)*

Matumizi haya ya lugha ya Kiingereza yametumika kana na wahusika walivyojengwa na kutaka kufikisha dhui yaliyokusudiwa, mfano jeuri na dharau waliyokuwa o wakoloni wa Kizungu dhidi ya Waafrika.

**JINA LA KITABU**
Jina la kitabu, Vuta n'Kuvute linasadifu na yale ambayo yameshughulikiwa na kusimuliwa ndani ya riwaya hii. Visa na matukio yaliyomo yanaonesha Vuta n'kuvute. Kua Vuta n'kuvute kisiasa baina ya wakoloni na wananchi, kuna Vuta n'kuvute mapenzi na ndoa, vuta n'kuvute za vijana (watoto) na wazazi nyinginezo nyingi. Kwa ujumla riwaya hii ina vuta n'kuvute za

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kisiasa, vuta n'kuvute za kijamii na vuta n'kuvute za kiutamaduni kama zilivyojadiliwa katika kipengele cha maudhui ya kitabu hiki.

**KUFAULU KWA MWANDISHI**
Mwandishi amefaulu kwa kiwango cha hali ya juu katika kuijenga kazi yake kifani na kimaudhui.

**KIMAUDHUI**
Mwandishi amefaulu kufikisha ujumbe katika jamii dhamira yake kuu ya mapambano ili kuleta ukombozi. Wapambanaji wake wote wamefaulu . yasmini amefaulu mapambamo dhidi ya ubaguzi wa rangi ambapo ameweza kuishi na Waafrika wakati yeye ana asili ya kihindi pia kaolewa na Mwafrika ambaye ni Bukheti; pia Gulum mwenye asili ya kihindi ameoa Mwafrika na alimkubalia mpwawe yasmin aolewe na bukheti ambaye ni Mwafrika.

Yasmini amefaulu mapambano ya ndoa za lazima baada ya kuondoka kwa Mzee Raza mumewe na kuolewa na mume asiyempenda.

Denge amefaulu kwa kiasi fulani mapambano ya haraka dhidi ya ukoloni kwa kutikisa serikali ya kikoloni mpaka inspekta wright akataka urafiki na Denge na kutaka kumrubuni kumuahaidi cheo kikubwa. haya ni mafanikio katika harakati za mapambano.

Mwandishi ametafuta katika kuijenga fani ya kazi ameteuwa na kuyapanga maneno vizuri, amewapanga wahusika wake vizuri na kuwapa maneno stahiki ya kusema na kutenda kulingana na uhusika wao. Kuwatumia baadhi ya wahusika na kuwapa lugha waliyoitumia isiyo sanifu ndiko kuliko ongeza mvuto katika kazi hii. Wahusika Wanazungumza kwakupangilia lugha ile waliyoitumia ni kuongeza ladha katika fani. kosa la kiufundi lilifanyika kwa upande wa fani ni kule kutumia lugha kali (matusi)badala ya kutumia tafsida.

**KUTOFAULU KWA MWANDISHI**
Kwa upande wa maudhui, mwandishi hakufaulu katika kumjenga Mhusika Yasmini kufanya usaliti katika ndoa.hakutakiwa kuchezewa. Kumfanya mhusika wake awe msaliti katika ndoa ni kufeli kwa mwandishi, kwani haikupata funzo zuri kutokana na kitendo hicho.

**MASWALI**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. Miongoni mwa maudhui yanayoibushwa katika riwaya ni machungu ya wanawake dhidi ya kani kinzani na kasheshe wanazofanyiwa katika mikakati yao ya kutaka kujinasua. Toa maoni yako ukitumia riwaya ya Vuta n'kuvute.

2. "Kuwepo kwa fasihi katika jamii ni tarajio la kimsingi; inapokosekana jamii hupata mapungufu katika ukamilifu wake...". Kwa kutumia riwaya ya Vuta n'kuvute kataa au kubali hoja hiyo.

3. "Ukombozi si jambo rahisi". Hakiki kauli hiyo ukihusisha riwaya ya vuta n'kuvute. Toa hoja tano (5).

4. Ujenzi mzuri wa fani husaidia uwasilishaji wa maudhui katika kazi ya fasihi. jadili usemi huu kwa hoja tano (5) madh'ubuti ukitumia Vuta n'kuvute.

5. Muhusika mkuu ni kipaza sauti cha msanii wakati muhusika mdogo ni mjenzi wa muhusika mkuu" Fafanua kauli hii kwa hoja tano (5) ukitumia vuta n'kuvute.

**UHAKIKI-TAMTHILIA**

KITABU: NGUZO MAMA

MWANDISHI: PENINA MHANDO

MWACHAPATI: DUP

MWAKA: 1982

Tamthiliya inazungumzia matatizo mbalimbali yanayowakabili wanawake katika jamii ya kitanzania na afrika kwa ujumla. Mwandishi anaonesha unyanyasaji na mateso ya wanawake kutoka kwa waume zao kutokana na mfumo dume uliojengeka katika jamii nyingi.ametumia mandhari ya patata kuyasawiri maisha ya mwanamke wa kiafrika.

**MAUDHUI**

**DHAMIRA KUU.**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. **UKOMBOZI WA MWANAMKE**,

Ni tamthiliya inayochambua kwa undani matatizo mbalimbali yanayowakabili wanawake pamoja na jitihada zao ili kujikwamua katika minyororo ya utumwa kwa mwanaume na manyanyaso mengine mazito mengine wanayoyapata kutoka kwa jamii kwa ujumla. Ameyataja manyanyaso hayo kama vile: wanawake kupigwa, kufanyishwa kazi nyingi (kufua, kupika, kulea watoto, kuchota maji, kukusanya kuni n.k). Pia ameonesha mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa na mwanamke kujikomboa. Mwandishi ameugawa ukombozi wa mwanamke, kama ifuatavyo

**Ukombozi wa kiuchumi.**

Mwandishi kwa kuwatumia wanawake wa patata ameonesha jinsi walivyoanzisha miradi ambayo ingewawezesha kujipatia fedha na kuwafanya wanawake wote wajitegemee, Wasiwe tegemezi.

“**BI NNE**…………………. Miradi tutatiliya mkaazo, Miradi

Yakila aina, vilabu vya pombe, maduka

Ya kanga, ushirika wa kushona, kupika

Hotel na mengine mengi…………………”

**BI PILI** naye aliamua kuanzisha kilabu cha pombe ili aweze kujikwamua katika maisha magumu kiuchumi.

“**BI MSIMULIZI**………. Kaamua bi pili

Pombe kujipikia na kilabuni

Kuiuza, pesa akipata, pesa msema

Kweli. Na mauzo mama atasimama”

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Nukuu hii inonesha umuhimu wa pesa katika ukombozi wa mwanamke, kwani pesa ndiyo iletayo maendeleo stahiki.

Bi moja alijiunga na wenzake na kuanzisha viwanda vya kufuma mapambo ya nyumbani.

“**BI MSIMULIZI** ..............katokea bi moja

Na wazo lake jipya kiwanda

Kuanzisha mapambo ya nyumbani

Kufuma………”

- **Ukombozi kijamii.**

Kwa kutumia mhusika bi Nane mwandishi amonesha ukombozi wa kijamii kwani alianzisha umoja wa walimu wa kike, Lengo likiwa kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili katika ufundishaji.

“**BI MSIMULIZI** ..............katokea bi nane na wenzake

Wengi makubwa hawakujitakia

Vizuri walijishauri

Tuanze na yetu matatizo……….

Kazi yetu yakufunza vyema kuchapa

Vingi vikitokomea

Vyema vijana watafunzika”

Mwandishi anaonesha kuwa elimu ni nyenzo mojawapo ya kumkomboa mwanamke, Katika kumkomboa mwanamke kijamii, mwandishi ameonesha jamii nzima lazima ishirikishwe, Mwanamke peke yake atoweza kujikomboa.

**“BI NANE**……tushirikishe wanaume pia

Nguzo mama inafaida kwa wote“

Mwandishi anaonesha mwanamke akikomboka ni faida kwa jamii nzima. Pia mwandishi anaonesha umoja na mshikamano kama njia itakayowawezesha wanawake kujikomboa.

Pia mwandishi anaonesha kupitia mikutano watu wengi wataelewa zaidi kuhusu ukombozi wa mwanamke na ..., wayapatayo wanawake nahivyo kuwa rahisi kubadilika.

- **Ukombozi wa kisiasa.**

Mwandishi anaonesha juhudi mbalimbali za wanawake wa patata ili kujikomboa kisiasa. Nafasi za uongozi kwa wanawake ni moja kati ya njia hizo ndiyo maana mwandishi anonesha jitihada mbalimbali zilizofanywa na wanawake wa patata ili kuchukua uongozi serikalini. Mwandishi anasema:

**“BI NNE**............madaraka kwa akina mama

Jambo hili tumetilia mkazo,

Wakina mama watapewa vyeo

Orodha tumeshapanga, tutapata

Mawaziri, mameneja, mabalozi n.k

Wengine tayari wameshapata kama

Tunavyofahamu”

Mwaandishi ameonesha umuhimu wa mwanamke kupewa uongozi kujikomboa kisiasa. Baadhi ya waliopata uongozi ni Bi Nne, mwenyekiti wa kamati ya vyeo. Bi Tatu, mwenyekiti wa kamati ya malezi bora. Bi Nane mwenyekiti wa umoja wa walimu.

**Ukombozi wa kififikra.**

Mwandishi ameonesha tatizo linalosumbua wanawake wengi, Wanawake wengi wamekuwa na fikra potofu. Kuwa baadhi ya mambo ni ya wanaume tu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

hayamuhusu mwanamke, mfano , uongozi , kufanya kazi , kumiliki njia za uzalishaji mali, kujitegemea wao wenyewe n.k kwa mfano bi Nne aliyekuwa mwenyekiti wa wanawake alishiriki kuyachunguza mashtaka ya bi Nane na akatoa hukumu kwa kusikiliza upande mmoja, jambo hili ni fikra potofu. Bi Nane licha ya kufahamu kuwa mashtaka yake ni ya uongo anakubali kila kitu alichoelezwa na bi Nne.

Kwa ujumla ukombozi wa kifikra juu ya wanawake na jamii kwa ujumla vinahitajika ili kufikia ukombozi wa kweli wa mwanamke.

**DHAMIRA NDOGONDOGO.**

2. **UONGOZI MBAYA.**

Mwandishi ameonesha umuhimu wa uongozi katika jamii. Pia amemuonesha kiongozi kama mtu anayeweza kuipeleka jamii katika mafanikio, au katika matatizo.

Mwandishi anasema:

"BI NNE' tena kwetu sie kiongozi uongeza njia

Aweza kutupeleka kwenye neema

Au mdomoni mwa simba"

Viongozi wengi wamekuwa wakipelekea jamii zao katika midomo ya simba, kwani hutumia uongozi wao kujipendelea wenyewe, na kujiona watukufu kwenye daraja la juu, Wanafanya maamuzi watakavyo bila kufuata utaratibu. Mwandishi anasema:

"BI MSIMULIZI: bi Nane akawaza kumbe kazi

Hii ya uongozi au uwenyekiti

Inampa mtu uwezo wa kufanya

Mambo kinyume cha kawaida"

Kutokana na dondoo hizi mwandishi anathibitisha kuwa uongozi mbovu ndio chanzo cha matatizo yanayoikabili jamii ya patata. Viongozi

kama bi Nne na mwenyekiti wa kamati mashauri, mfano wa viongozi wabovu wanaorudisha nyuma.

Udikteta umeoneshwa kama tatizo linalotokana na uongozi mbovu. Kiongozi kama mwenyekiti wa kamati ya mashauri ameoneshwa kama dikteta anayetumia uongozi atakavyo. Anaongozwa na hisia au kufuata anavyoambiwa na watu wengine wa karibu badala ya kufuata miongozo ya kikatiba iliyowekwa. Mwenyekiti anatumia vitisho kumlazimisha bi Nane akubaliane na kitu ambacho ajafanya kwakuwa yeye ni kiongozi, pia anaamua kesi kwa kusikiliza upande mmoja bila kumpa mshitakiwa nafasi ya kujieleza. Mwandishi anasema:

"BI MSIMULIZI: vipi mtu atatoa ushauri

Kufuatia maelezo ya mshitakiwa pekeyake

Tena tuliyoelezwa wakati mshitakiwa hakuwepo?

…………………………………………………

Na ajabu kupita yote

Vipi mwenyekiti bila kamati

Akatoa ushauri katika mashtaka?

Pia baadhi ya wanawake utumia madaraka ya waume zao ili kuwakandamiza wenzao, na hivyo kukwamisha harakati za ukombozi wa mwanamke.

Mfano: bi tatu anasema.

"mkitaka nitalipa hela badala ya

Kufanya kazi samahani, kwaherini

Tena hata kesho siwezi kufika, Tuna

Pati nyumbani kwetu ya kazini kwa

Mume wangu kwahiyo sitafika"

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

"BI NANE: haya jamani sisi tusiokuwa na
Wanaume wa kutubembeleza sisi ambao
Waume zetu sisi watu wakubwa
tuendelee"

Katika hali halisi wanawake baadhi, hutumia madaraka ya waume zao kunyanyasa wanawake wengine badala ya kuyatumia kuwaakomboa, Pia mwandishi anaonsha kuwa viongozi waliopewa madaraka na waliotegemewa kufanya mabadiliko ndiyo wamekuwa viongozi wabovu. Mfano

"kwa wema na kwa huruma

Labda kamuelezea bi Nne"

Chizi anamshangaa bi Saba kwani licha ya kuudhuria vikao mbalilmbali alikuwa aelewi hata nini maana ya NGUZO MAMA na pia viongozi hawakuweza kumsaidia kwa lolote.

## 3. ELIMU.

Elimu imeoneshwa kama nyenzo muhimu katika mandeleo ya jamii. Mwandishi wa tamthiliya hii amethibitisha umuhimu wa elimu katika ukombozi wa mwanamke na jamii kwa ujumla. Mwandishi anasema.

"BI NNE: ...........tumepiga nia sana,
: Jambo hili la ushonaji, sasa tutapata vitu
: Patata kate. Pia somo laushonaji, litatiliwa
: Mkazo mashuleni. Kila shule itafundisha ili
: Watoto wetu wajue kushona, wavae vizuri na
: Kupamba nyumba zao vizuri".

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Kwa upande mwingine bi Nane anaonesha kuwa watu wasipopata elimu hawatapata maendeleo pia.

“BI MSIMULIZI…………………………

Tuvitoe vigingi vile vituzuiavyo,

Kazi yetu ya kufunza vyema kuichapa

Vigingi vikitokomea

Vyema vijana watafunzika

Wakifunzika wote patata

NGUZO MAMA Itasimama”.

Dondoo inatuonesha kuwa kutokana na kukosekana kwa elimu jamii ya patata imeshindwa kupata maendeleo na kuwakomboa wanawake.

Pia elimu imeoneshwa kama kikwazo cha uongozi. Viongozi hawakuwa na elimu kiasi kwamba hawakujua kinachoendelea katika masuala ya uongozi. Kwa mfano: bi Nne alikuwa na uongozi mbaya kwasababu hakuwa na elimu. Pia wakina mama wengi hawakufahamu masuala ya uongozi na hata viongozi wao kutokana na kutokuwa na elimu, Wala viongozi wake. Baada ya chizi kumuuliza bi Saba, anajibu hivi:

“BI SABA……….

Mwanangu mie sijui,

Labda kamuulize bi Nne

Lakini juzi kachaguliwa katibu

Sijui na kamati gani ile, nimesahau

Kwa upande mwingine mwandishi amezungumzia umuhimu wa elimu ya malezi katika jamii. Katika ulimwengu wa sasa ambao unakabiliwa na matatizo mengi, kama vile magonjwa (UKIMWI), tamaa ya pesa, matumizi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ya dawa za kulevya na kuporomoka kwa maadili kwa kiasi kikubwa, elimu ya malezi inaonekana kuwa ya muhimu zaidi katika jamii.

Mwandishi anasisitiza kuwapo kwa elimu ya malezi itakayo wasaidia vijana na wanawake hasa wale wanaokumbana na matatizo mbalimbali kama vile utoji wa mimba na kutupa watoto sharti wapate elimu ya malezi ili waache tabia hiyo.

"BI NNE: ...........pia wasichana kutupa

watoto kwenye mapipa kuna

semina wiki ijayo kuzungumzia

jambo hili ni aibu kubwa sana

kwetu"

Sambamba na hilo mwandishi anataka elimu ya malezi itolewe pia kwa jamii ili ukombozi wa kweli upatikane. Mfano, mwandishi anaitaka jamii ielimishwe ili kubadilisha sheria ya ndoa. Kila mtu awe na mke mmoja, Pia itungwe sheria ya kuwabana wanaume wanao piga wake zao ovyo. Mwandishi anasisitiza kuwa elimu itolewe kwa watu wakubwa wenye tabia ya kuwapa mimba watoto wa shule, Pia itungwe sheria kalli itakayodhibiti tabia hiyo.

"BI NNE: ...........sheria ya ndoa itabadilishwa

Kila mtu mke mmoja........

Na mambo ya kupigwapigwa hatutaki

Pia mabo ya watoto wa shule kupewa

Mimba ovyo, Tene na watu wakubwa

Kwa miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia mmomonyoko mkubwa katika jamii yetu,Hivyo elimu ya malezi bora ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii.

## 4. DHULUMA.

Mwandishi amemtumia Bi Saba kuonesha jinsi wananwake wengi wa kiafrika wanavyodhulumiwa mali, hasa wajane, pindi wanapofiwa na waume

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

zao. Bi Saba baada ya kufiwa na mume wake alidhulumiwa mali zote alizochuma na mume wake. Shemeji zake waligawana kila kitu hadi watoto na kumuacha bi saba akihangaika asijue la kufanya.

"BI SABA...........hao! Shemeji mmerudi kuchukua hata
Kitanda! Hata sufuria! Nitalala wapi
Na nitapikia wapi jamani!"

Mwandishi ameonesha wanawake wengi wanao dhulumiwa hawana msaada ndiyo maana dhuluma imetapakaa kila mhali.

"BI MSIMULIZI.............................

Akalia bi Saba tena akalia

Hana wakumsaidia

Mumewe kafa nduguze wanakuja juu

Vyombo na nguo zote wakagawana

.........................................................

Kiti hiki changu, mie lile jembe,

Mie suruali hizi, ilimradi likawa zogo"

Dondoo hii inathibitisha kuwa dhuluma ni tatizo lililopo katika jamii yetu.

Kwa upande mwingine mwandishi ameonesha dhuluma inayofanywa na viongozi dhidi ya wale wanaowaongoza. Viongozi wanaonekana kupewa kipaumbele zaidi katika mambo mbalimbali kuliko wale wanao ongoza. Mfano chizi amemuonesha bi. Nne kuwa yeye ni mtu mkubwa na anayepewa kipaumbele zaidi.

"CHIZI.................................

Lakini bibi yangu aliniambia

Binadamu wote sawa"

Pia mwandishi anaonesha jinsi viongozi wanavyowadhulumu wanao waongoza kwa kuwalazimisha na kuwapa masharti yaliyo kinyume na katiba. Hii ni dhuluma dhidi ya democrasia.

"MWENYEKITI: Jambo la pili nakueleza kuwa

Hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa

Kufanya mkutano bila kibali cha

Ofisi hii ..................................

Sheria hii ipi na inajulikana"

"BI MSIMULIZI: lahaula!

Sheria hii bi nane hajapata kusikia"

Pia kitendo cha viongozi kutokuwajibika na baadhi hata kutofahamu maana ya NGUZO MAMA, ni dhuluma dhidi ya wale wanaowaongoza.

5. **USALITI.**

Mwandishi ametuonesha suala la usaliti kama tatizo linaloikabili jamii yetu. Mwandishi amonesha waalimu wenzao, Bi Nane kwa kutoa siri za vikao wanavyovifanya na kumpelekea bi nne ambaye ni adui wa bi nane. Usaliti huu ulimsababishia matatizo bi nane kwani alituhumiwa kuwa ni msaliti na mvuruga amani. Mwandishi anasema;

"BI NNE ...

Tena mwenyekiti mimi

Nilikwambia hao walimu

Wengine awampendi bi Nane

Yeye tu ndiye anayejiweka kimbelembele kama

Anawapenda mbona wanatoka kueleza mipango yao?

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pia usaliti huu ulipelekea bi Nane kuingia kwenye migogoro mikubwa na mwenyekiti

“MWENYEKITI.............................

Kwa kifupi nikwamba tumepata habari

Kwamba wewe umeanzisha kukindi cha

Kupinga juhudi za wenzenu.........................

Tena kikundi hicho kimekuwa kikifanya

Mikutano kupanga njama za kuchafua”

Kwa upande mwingine mwandishi ameonesha jinsi ambavyo baadhi ya watu huwaka kwa ndugu zao kutokana na matatizo waliyokuwa nayo. Mfano shangazi yake chizi alimkana tena huku akimdhiaki kwa kumtukana na kutaka kumuitia mbwa.

“CHIZI..................................

Huyu bi tatu ni shangazi yangu

Haki ya mungu tena! Naambiwa yeye

Ni shangazi yangu kabisa katoka baba

Yangu alafu yeye. Siku moja............. ngojeni

Niwaoneshe”.

**“BI TATU:** usiniite shangazi. Toa balaa lako

Hapa. Ukirudi nitakuitia mbwa

Akuume”

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Dondoo hii inatuonesha jinsi jamii ilivyobadilika, wazazi ambao ni tegemeo la watoto, hawawathamini, hasa watoto wenye matatizo.

Pia usaliti wa mume wa bi Tano na bi Sita dhidi ya bi Tano.

## 6. UVIVU NA UZEMBE.

Mwandishi ameonesha kuwa watu wa jamii ya patata ni wavivu na wazembe, yaani hawawajibiki ipasavyo katika kufanya kazi. Mwandishi ameonesha uvivu na uzembe umechangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha jitihada za akina mama katika kuinua nguzo mama. Mfano wakina mama walipokuwa wakiinua "NGUZO MAMA" baadhi walikuwa wanategea kwa kufanya mazungumzo ambayo ayakuhusiana na mukutadha wa kazi hiyo. Mwandishi anasema;

"BI NNE:

Haya bi Moja, bi Mbili, bi Tatu. Vuta!

Tena vuta!"

"BI MOJA: aise hizi kanga mpya umenunua wapi?"

"BI TANO: huna habari kuwa zimetoka? Hizi

Nimenunua jana pale kwa mwarabu"

"BI NANE: Sasa jamani bi moja una kwenda wapi tena?"

"BI MOJA: Aaa, jamani nitarudi, lakini kanga hizi sikosi"

Pia mwandishi ammuonesha bi Sita kama mwanamke asiyewajibika kwani kwake wanaume ni muhimu kuliko kazi.

Bi Tatu naye anaacha kufanya kazi na kuamua kufuatana na mume wake kwenda kwenye sherehe kwani kwake yeye sherehe ni muhimu zaidi kuliko NGUZO MAMA". Mwandishi anasema.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

“BI TATU: Sio utani ndugu yangu. Tunakwenda

Kwenye pati na mume wangu leo saa

moja lazima nipalilie unga kwa baba

watoto wangu ati, Nitakula nini”

Viongozi nao wnaonekana wababaishaji, wamejaa maneno pasipo kuwajibika, Kwa mfano bi Nne ambaye ni kiongozi anaacha kazi ya kunyanyua NGUZO MAMA na kwenda kwenye vikao ambayo ni kazi ya kupiga soga.

Kutokuwajibika kwa viongozi pamoja na wanawake kwa ujumla unakwamisha harakati za kuinua NGUZO MAMA pia kwa kiasi kikubwa ugumu wa maisha katika jamii yetu unatokana na tabia ya uvivu na uzembe.

## 7. MAPENZI NA NDOA.

Mwandishi ameyajadili mapenzi katika sura mbili, Kwanza ameonesha mapenzi yanayo jali pesa, usaliti pia katika mapenzi na ndoa. Amonesha mapenzi yanayojali pesa kwa kutumia maganga mume wa bi tano. Anamsaliti mkewe na kuwa na mahusihano na bi sita. Bi tano anasema:

“BI TANO: ...

Wee bi sita mshenzi, Unanichukulia

Mume wangu hivihivi kimacho macho”

Usaliti huu unapelekea ugumu wa maisha kwa familia ya bi Tano, kwani watoto wanalala njaa kwa kukosa chakula na mahitaji mengine muhimu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pia mwandishi anaonesha jinsi mapenzi yanayoendeshwa na pesa badala ya utashi wa mtu. Mfano; mapenzi kati ya bi Tatu na mume wake yaliendeshwa na pesa.

“BI TATU…………………

Unasema hivyo kwakua wewe

Unakazi ya mshahara hata

Ukiachwa unajitegemea, na mie je

……………………………………………………

Tuna pati nyumbani kwetu ya

Kazini kwa mume wangu kwa

Hiyo sita fika”

Kwa upande mwingine mwandishi ameonesha mapenzi ya uongo yanavyotawaliwa na misukosuko mingi. Mfano Sudi alikuwa akimpiga mara kwa mara bi Pili.

Hii inaonesha kwamba Sudi hakuwa na mapenzi ya dhati kwa mkewe.

“SUDI: Wacha mdomo nitakupiga mbele

ya hawara zako”

Sambamba na hilo mwandishi anaonesha jinsi jamii inavyokubaliana na tabia ya wanaume kuwa na mke zaidi ya mmoja, Anaonesha jinsi wanawake wanavyojitahidi kulibadilisha suala hili.

## 8. NAFASI YA MWANAMKE.

Mwandishi amemchora mwanamke katika namna tofauti tofauti,

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Kama chombo cha starehe**. Ameoneshwa kwamba anatumia mwili wake kama bidhaa iuzwayo sokoni na kumpatia faida. Kwa mfano bi Sita alikuwa kahaba. Mwandishi anasema:

“BI MSIMULIZI:

Mji huu sikuingia leo ndugu

Yangu, mawaziri makabwera

Mapadri kwa mashehe vijana

Kwa wazee, mie breki mie jeki

Kwangu mie utasimama”

Bi Sita alitumika kama starehe ya mume wa bi Tano na hivyo kusababisha migogoro kati yake na bi Tano

- Kama kiumbe duni asiyekuwana thamani wala uwezo wa kufanya jambo lolote katika jamii. Mwandishi ameonesha wanaume waliwadharau sana na kuwabeza wanawake na kuwaona watu wasiokuwa wakamilifu.

- Kama jasiri mwenye kujitoa mhanga na mwenye elimu. Mfano Bi Nane alikuwa na elimu na alitumia vizuri kwa maendeleo ya jamii nzima. Pia alionesha ujasiri wake alipomjibu mwenyekiti kufuatia shitaka alilotakiwa kujibu kwani alitakiwa kujibu kwa maandishi.

- Kama mtu mtumwa wa mwanaume, mwanamke ni chombo cha uzalishaji mali, mfano Bwana sudi alimtumikisha mkewe Bi pili na kumuachia majukumu ua kutafuta mahitaji ya familia huku yeye akiwa anakunywa pombe tu.

- Kama kiongozi wa familia ambaye amebeba majukumu ya kuikuza jamii na kama mwanamke asingekuwepo katika jamii na jamii isingekuwepo.

**NAFASI YA MWANAUME**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Amependelewa
- Mvivu mfano Sudi
- Muonevu mfano Sudi
- Chombo cha starehe mfano Maganga

- **UJUMBE**

1. Kukosekana kwa umoja na mshikamano miongono mwa wanawake ni kikwazo kikubwa cha ukombozi wa wanawake.
2. Ulevi, uvivu, unafiki na usaliti ni maadui wa maendeleo
3. Ili tuweze kupata maendeleo ya kweli katika kila jambo ni lazima jamii nzima ishirikishwe.
4. Uongozi ni jambo la msingi katika kufikia malengo mbalimbali tunayojiwekea
5. Wanawake pia wanastahili kupewa nafasi za uongozi sawa na wanaume
6. Suala la malezi kuwa ni muhimu katika familia na sharti lihusishe wazazi wote wawili
7. Kuwa na mke zaidi ya mmoja ni kikwazo kwa familia na jamii kwa ujumla.
8. Wanaume ni kikwazo cha ukombozi wa mwanamke hivyo wanahitaji kuelimishwa ili kiondokana na dhana potofu ya kuwaona wanawake kama viumbe duni wasioweza kuchangia chochote katika maendeleo ya jamii.

- **MIGOGORO**

1. Kati ya Bwana Sudi, Shaba, na Totolo. Chanzo ni shaba na Totolo kumtetea Bi Pili ambaye alikuwa mke wa Sudi. Suluhisho la mgogoro ni kwamba Bi Pili aliamua kukimbia.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

2. Kati ya chizi na shangazi yake Bi Tatu, hakumpenda wala kumthamini Chizi na hiki ndicho chanzo cha mgogoro suluhisho ni kwamba Bi Tatu aliamua kumfukuza bila kumpa msaada wowote Chizi.

3. Kati ya Bi Saba na shemeji zake. Chanzo ni kifo cha mume wa Bi Saba. Baada ya kufiwa na ndugu wa mume wake waliamua kuchukua vitu vyote, hivyo kumtaka Bi Saba, lakini Bi Saba alikataa. Mwisho waliamua kumnyang'anya vitu hivyo kwa nguvu wakagawana mpaka watoto.

4. Kati ya Sudi na mkewe, Chanzo ni bwana Sudi kudai pesa kwa mkewe na mkewe akakataa kwani zilikuwa zinahitajika kwa familia nzima. Suluhisho ni kwamba Sudi aliamua kumpiga mkewe.

5. Kati ya Bi Tano na Bi Sita. Chanzo Bi Sita kumchukua mume wa Bi Tano. Na suluhu ni Bi sita kuondoka na Bwana Sudi kukimbia.

6. Mgogoro kati ya Bi Tano na wanakikundi, chanzo ni vitambaa alivyopewa Bi Tano kutokuuzika. Suluhisho ni kwamba aliamua kugawana vitambaa kila mtu akauze.

7. Mgogoro kati ya Bi Nne na Bi Nane.

8. Mgogoro kati ya......................................

- **MSIMAMO**

Msimamo wa mwandishi ni wa kimabadiliko kwani ameweza kuonesha matatizo mbalimbali yanayowakabili wanawake katika harakati za kujikomboa na kwa baadhi ya matatizo hayo ameeleza nini kifanyike.

- **MTAZAMO.**

Mtazamo wa mwandishi ni wa kiyakinifu kwani matatizo aliyoyaeleza dhidi ya wanawake ni halisi na yapo katika jamii yetu. Pia mbinu alizopendekeza kukabiliana na matatizo hayo ni mbinu sahihi.

- **FALSAFA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mwandishi anaamini kuwa ili wanawake waweze kujikwamua lazima wawe na maelewano umoja mshikamano kusiwepo na usaliti, pasiwepo na wivu wala kugombana.

## B. FANI

- **MUUNDO**

Mwandishi ametumia muundo msago yaani matukio yamepangwa toka mwanzo na kusimuliwa kwa mfululizo mpaka mwisho. Mwandishi amegawa tamthiliya katika maonesho manne ambayo katika onesho la kwanza ameanza kuonesha nguzo ikiwa chini na harakati za wanawake kuinua kuanzia onesho la pili mpaka la tatu anaonesha jitihada walizofanya akina mama kuinua nguzo mama na matatizo mbalimbali jinsi akina mama mbalimbli walivyokumbana nayo. Onesho la mwisho linaonesha jinsi akina mama walivyoshindwa kabisa kuinua NGUZO MAMA

- **MTINDO**

Mwandishi ametumia mtindo wa dailojia na analojia kwa kiasi kikubwa.

"BI MSIMULIZI: kwa vile chizi kakimbia

Hadithi tamalizia

Wakaamua wakainuka

Siku ya kwanza ikapita

NGUZO MAMA pale pale"

"BI NNE: Inuaaa!

BI NNE: Hebu tutazame kwanza kwanini haisogei ?

Pia mwandishi ametumia lugha ya kishairi ili kuongeza mvuto katika kazi yake.

Mfano :

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

“CHIZI; Chizi mie chizi mie

Sikizeni langu rimba

Rimba nimelitengeneza

Kwa mikono yangu hii”

Pia kuna matumizi ya hadithi ndani ya tamthiliya ambacho ni kipengele cha fasihi simulizi – mfano kuna Bi Msimulizi kuna hadhira. Pia kuna

“BI MSIMULIZI; Hadithi hadithi

HADHIRA; hadithi njoo!

Mwisho msimilizi anamalizia kwa kuuliza hadhira.

“BI MSIMULIZI; niendelee nisiendeleee

HADITHI YANGU IMEKWISHA

**Pia kuna matumizi ya nyimbo,** Bi moja anapagia jukwaani anaambatana na wimbo. Na mwisho wa tamthiliya inamalizika na nyimbo.

“Mkarara; nguzo mama, nguzo mama

Tukupambaje maua

Tukupambaje maua

**Pia mwandishi ametumia nafsi mbalimbali**

“BI MSIMULIZI; Kwa vile chizi kakimbia

Hadithi tamalizia

Wakainua wakainua

Siku ya kwanza ikapita....

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Ili kuuboresha mtindo mwandishi ametumia chizi ambaye ni mtu mwenye matatizo ya akili. Lakini ametumia kusema maneno yenye ukweli na uhalisia katika kazi yake.

“CHIZI: Wananiita mimi chizi

Chizi mie au nyie

Ambao macho mwakodoa

Kuwachia wacheke

Wanavyotaka kufanya”

Kuandika majina ya wahusika wote kwa herufi kubwa. Jambo hili linamsaidia msomaji kufuatilia kazi ya mwandishi kwa urahisi.

> “Bi MOJA; tena maneno yako yanatutia uvivu kabisa.
>
> BI NANE; bila umoja hatutafanikiwa kitu”

Mwandishi ametumia mbinu ya kuweka picha katika jalada inayoonesha wanawake wakiinua NGUZO MAMA, ambayo pia ni mwanamke. Picha inasadifu yaliyomo kwani inaonesha harakati za kina mama zilivyoshindwa kuwa NGUZO MAMA.

- **<u>MATUMIZI YA LUGHA</u>**

Mwandishi ametumia lugha fasaha na inayoeleweka iliyojaa matumizi ya nahau, misemo, na tamathali za semi pamoja na mbinu za kisanaa.

- **Nahau/ misemo**

**Mfano:** utakufa kibudu”

> “Dume Malaya si dume roho yako kusumbua”
>
> “Utakiona cha mtemakuni”
>
> “Watoto ni taifa la kesho”

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

"Akachanganya ulimi"

- **Methali**

Mfano: "asiye na mwana aeleke jiwe"

"Umoja ni nguvu utengano ni uadhaifu"

· TASWIRA

Kuna taswira ya NGUZO MAMA ambayo inaonesha haki za wanawake

"BI MOJA: lakini kweli bila shaka tukivuta itasimama hii NGUZO MAMA

Jembe – kuachiwa mkulima

Kama – mbinu za kuinua NGUZO MAMA

Mana - viti vizuri

**Tamaathali za semi:-**

- **Tashbiha**

"Amevaa kama mkulima wa bara"

"Wanamwagwa kama mbuzi"

"Anatembea kama kapigwa bumbuwazi"

- **Tashihisi**

"Hasira zikampanda Bi Nane"

- **Sitiari**

"Mbwa mume wako, anayefuata wanawake ovyo"

"Mie breki mie jeki"

Mbinu nyingine

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- **Takriri**

"Wakajaribu wakajaribu"

"Wakaenda wakaenda wakaenda"

- **Mdokezo**

"Wakavuta ...............wakavuta"

"Hebu tutazame kwanza kwanini hawasogei..............."

- **Tanakari sauti**

Kigelegele

" Lu lu lu lu lu lu lu lu !

- **Mjalizo**

"Wakazaliana wakaongezeka"

"Mvi, wakavu, vipara"

- **Matumizi ya lugha ya matusi**

"Malaya mkubwa wewe"

"mbwa wee"

".....mshenzi mkubwa"

- **Lugha ya sauti ya kishairi**

"CHIZI: Sikilizeni na sauti

Kama ndege wa nyikani

Lakini moja sitaki

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Msinitazame usoni

Mama yangu kanizaa

Sura langu baya baya

Lakini mwenyewe mama

Kwa hakika ni mzuri

Baba yangu simjui

Mama hataki nambia

- **Matumizi ya kingereza**

"My God"

- **WAHUSIKA**

- Bi Nane

Alichangia kwa kiasi kikubwa kuonesha dhana ya ukombozi wa mwanamke, Ni mwanamke msomi mwenye ushirikiano, alipenda kuwaelimisha wenzake. Mvumilivu na asiyekata tamaa, hakuwa na chuki wala hasira na hakupenda kulipa kisasi, Anafaa kuigwa.

- Bi Nne

Ni mpiga majungu anawivu mbinafsi mwenye chuki mwenye dhana potofu, Amechangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha juhudi za kuinua NGUZO MAMA, anatumia madaraka vibaya na hakuwa na elimu ya kutosha. Hafai kuigwa na jamii.

- Mwenyekiti

Mpenda fitina na mpika majungu anachukia wanawake anatumia madaraka yake vibaya. Ni kielelezo cha viongozi wasiokuwa na elimu ya kutosha. Hafai kuingwa na jamii.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Bi Msimulizi

Huyu ndiye msimulizi wa matukio yaliyotendwa na wahusika mbalimbali, Ametumiwa kuuboresha mtindo hasa vipengele vya fasihi simulizi.

- Chizi

Mpenda demokrasia, Alipiga vita tabia ya uongo, Msema ukweli na mfichua maovu yaliyo katika jamii anaonyesha waziwazi sababu zilizosababisha wanawake wakashindwa kujikomboa.

- Bi. Moja

Mpenda anasa, Mke wa shabani. Ni mzembe hakuwa na msimamo katika kusimamia NGUZO MAMA. Anawakilisha wanawake, mwanamke anaependa kujipamba na kusahau maendeleo. Hafai kuigwa.

- Bi Pili

Ni mke wa sudi aliyenyanyaswa sana na mume wake. Ni mvumilivu hakuwa na elimu ni mlezi mzuri wa familia anafaa kuigwa.

- Bi Tatu

Mpenda starehe hana ushirikiano na wenzake hapendi kazi zisizokuwa na mshahara ni kielelezo cha wanawake wengi wanaokubali kuwa watumwa kwa kubembeleza wanaume zao kwa kuogopa kuachwa, Hafai kuigwa.

- Bi Tano

Ni mke wa maganga mwenye hasira anapenda anasa. Hakumpenda Bi Sita kwa sababu alimchukulia mume wake anafaa kuigwa na hafai kuigwa, Anakata tamaa mapema.

- Bi Sita

Ni kahaba anatembea na waume za watu, mkorofi na mwenye matusi. Hapendi ushirikiano na wanawake wenzake, Anapenda starehe kuliko kazi, Hafai kuigwa kabisa.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Bi Saba

Ni kiwakilishi cha wajane wanaoonewa katika masuala ya mirathi ni mlezi wa watoto aliyenyang'anywa kila kitu pamoja na watoto.Hafai kuigwa.

- Sudi

Mume wa Bi Pili mlevi na mvivu kiwakilishi cha wanaume wenye tabia ya kunyanyasa wake zao, Hafai kuigwa.

- Maganga

Mume wa Bi Tano si mwaminifu katika ndoa yake ni kielelezo cha wanaume wahuni, Hafai kuigwa.

Pia kuna wahusika wengine kama vile msichana ambaye ni kiwakilishi cha vijana, Pia Totolo, shaba kiando, makange, la mgambo.

· **MANDHARI**

Madhari ni ya kubuni lakini inayosawiri kwa kiasi kikubwa maisha ya vijijini na kwa kiasi Fulani maisha ya mjini, Mfano kilabuni, uwanjani, nyumbani ambamo zinauwezo kuwa mjini au vijijini. Pia uwepo wa vitu kama vile benz, Volvo na Bi Tatu kwenda kwenye pati inaashiria madhari ya mjini, Ngoma za madogori, Bi Pili kuwa mkulima, vilabu vya pombe vya mataputapu madhari ya kijijini.

Unyanyasaji na ugandamizaji wa wanawake ulionyesha madhari ya nchi yoyote ya kiafrika ambako kuna matatizo haya kwa kiasi kikubwa.

· **JINA LA KITABU**

Jina la kitabu ni "NGUZO MAMA"ambayo kimejengwa kitaalamu na kinaisadifu vizuri yaliyomo ndani. Tamthiliya hii inaonesha harakati za wanawake wakiungana kwa pamoja kuunganisha umoja wao ili kupata maendeleo. Lakini harakati hizo zinakwama kutokana na matatizo kama majungu, fitina, na kutokuelewana.

· **KUFAULU**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Kimaudhui**: Amefaulu kuonesha matatizo mbalimbali yanayowakumba wanawake wa kiafrika na vikwazo wanavyokabiliana navyo katika kutafuta ukombozi wa kweli.

**Kifani:** Mwandishi ametumia lugha rahisi inayoeleweka ya kishairi mafumbo rahisi na nyimbo zinazosababisha hivyo kufanya mchezo usichoshe. Pia inawajenga wahusika wake vizuri kwa kuwafanya waonekane wenye uhalisia na hivyo kubeba mawazo yanayosaidia hali halisi katika jamii.

· **KUTOKUFAULU**

**Kimaudhui**: Ameshindwa kuonyesha hatima ya wanawake wa Patata na jamii nzima baada ya kushindwa kuinua NGUZO MAMA.

**Kifani**: Kuna matumizi ya lugha ya matusi kwa mujibu wa maadili ya jamii yetu, lugha hii ni lugha isiyofaa.

**UHAKIKI WA DIWANI**

**"CHUNGU TAMU"**

Mwandishi T. Mvungi

Wachapishaji TPH

Mwaka 1985

**UTANGULIZI**

Diwani hii inajadili masuala mbalimbali ya kimaisha yaliyopo Tanzania, Kama vile utetezi wa haki umuhimu wa kazi na kuwajibika, mapenzi, maana ya maisha, suala la uongozi, usaliti, matabaka, suala la demokrasia athari za ukoloni na vita katika jamii, nafasi ya mwanamke na thamani ya mwanaume katika jamii.

· **DHAMIRA KUU**

1. **UJENZI WA JAMII MPYA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Harakati za ujenzi wa jamii mpya zilianza baada ya kupata uhuru na hisia baada ya azimio la Arusha. Azimio hili lilikusudia kujenga jamii yenye kufuata misingi ya haki na utu, yenye demokrasia ya kweli isiyokuwa na dhuluma, matabaka yenye viongozi waadilifu na wawajibikaji jamii isiyokuwa na aina yoyote ya unyonyaji, jamii ambayo hatamu za uongozi zingekuwa mikononi mwa wakulima na wafanyakazi. Kwa mujibu wa mwandishi jamii imeshindwa kufanikisha kueleza malengo ya kujenga jamii mpya. Ameonyesha vikwazo mbalimbali vilivyokwamisha ujenzi wa jamii mpya na kupendekeza mbinu mbadala ambazo zitakapotumiwa na jamii tutaweza kujenga jamii mpya. Mbinu hizo ni kamavile:-

**a. <u>Kufanya kazi kwa bidii – uvivu</u>**

Ameonesha tumeshindwa kujenga jamii mpya kutokana na uzembe na kutokuwajibika. Tunaviongozi wazembe wasio wajibika na wananchi wasiojua wajibu wao. Anaitaka jamii ifahamu kuwa kazi na kuwajibuka ni msingi wa maendeleo. Anaelezea juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Mfano:-katika mashairi ya "daktari" ,"Askari" ,"chanzo mwenye kauli", " wimbo wake hotubani", "wabaki Taabani."

Shairi la "Daktari" "Askari" linaonyesha jinsi Waganga wanavyojua kuwajibika katika kazi yao ya utabibu. Ameonesha jinsi walivyohudhuria majeruhi kwa bidii wakati wa vita. Jamii inatakiwa kuwajibika ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Katika shairi la "Chanzo ni wewe kauli"ameonesha jinsi utekelezaji mbovu wa mipango ya maendeleo na kutokuwajibika kwa viongozi kunasababisha rushwa, magendo na ulanguzi. Anaonesha uzembe unaofanywa na vyombo vya dola kwamba ndiyo umechangia uwajibikaji mbovu.

Shairi la wimbo wake hotubani, mwandishi anaonyesha utekelezaji mzuri na maazimio mbalimbali yanavyochangia kuleta maendeleo. Anaomba viongozi wetu wanaopenda kukaa ofisini hawatembelei maeneo ya kazi, wanatumia madaraka vibaya, wanatoa maagizo midomoni pasipo utekelezaji, wanakunywa na kulewa kila siku. Utekelezaji wao uko kwenye hotuba tu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Shairi la" wengine wabaki Taabuni "mwandishi anaonyesha jinsi uzembe kazini kutowajibika ipasavyo usaliti pamoja na rushwa vinavyorudisha nyuma utekelezaji wa maazimio mbalimbali tunayojiwekea, mfano mwandishi anaonesha vyombo vya dola huwaacha watu waadilifu kwa kuchukua rushwa,

Ulanguzi twaondoa

Adha hii ya udhia

Yaani tunaichukia

Adha isiyo rudia

Wote twataka kujua

Chanzo cha hii tabia.

Ni wazi kuwa endapo jamii itatambua umuhimu wa kuwajibika na kazi ndipo tutaweza kujenga jamii mpya.

**b. <u>Kuwa na uongozi mzuri – uongozi mbaya</u>**

Mfano shairi la "wimbo wake Hotubani "linajadili na kuonesha jinsi uongozi mbaya unavyozorotesha demokrasia na kusababisha utekelezaji mbaya wa mipango ya maendeleo. Pia mwandishi anaonesha viongozi wetu hawana uwezo wa kuendesha taifa hili kwa kukosa hekima. "Stahiki katika shauri la wimbo wake hotubani"

"Cheo kiko mikononi

Agizo li mdomoni

Kila siku yu pombeni

Mchana hotuba ndotoni

Wimbo wake hotubani

Raia kazi fanyeni"

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**c. Kuwepo kwa demokrasia ya kweli**

Kwa kutumia shairi la kademokrasia katoweka, mwandishi anapiga vita uongozi wa mabavu. Afrika demokrasia inapokosekana husababisha kuota mizizi na ni vigumu kuuzwa.mwisho hupelekea machafuko na vita vile vile unaonesha kuwa ili kumlinda dikteta, mabavu hutumika ili asing'oke madarakani hutumika kuwafaidisha wao. mwandishi anasema:-

Udikteta huelimisha

Kwa sumu ya nyoka na mabaka

Ibilisi asiye Baraka

Haki zatupiwa kwenye vichaka

Huku ni kustaarabika

Hivyo ili jenga jamii mpya hatuna budi kudumisha demokrasia ya kweli.

**d. Kupinga dhuluma**

Katika shauri la "Wengine wabaki Taabuni" Mwandishi anajadili juu ya dhuluma wanavyoendesha wakubwa nchini dhidi ya watu wa tabaka la chini. Ameonesha kuwa majambazi wanayo idhini ya kufanya lolote dhidi ya wanyonge, Ameonyesha dhuluma inavyotumiwa na majambazi nchini. Pia kwa viongozi wanatabia ya kujibembeleza mali bila kujali watu wenye kipato cha chini.

"Wale wafaao kitanzini

Ndo wamejaa madarakani

Mtu ajaza mali tumboni

Au ndege yawaka kichwani

Halafu wengine wasikieni"

· **DHAMIRA NDOGO NDOGO**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

## 2. SUALA LA MAPENZI

**Mwandishi amejadili aina mbalimbali za mapenzi:-**

**-Aina ya kwanza ni ile ya mtu na nchi yake.**

Katika shairi la "Daktari Askari" wakati wa vita ya Uganda na Tanzania raia wanajeshi, madaktari, manesi walijitolea kwa moyo wa dhati kwenda kupigana kuikomboa nchi yao. Haya ni mapenzi ya kweli na dhati.

Mapenzi kama ya Idd Amini si ya kweli ndiyo maana alitumia mabavu kuiongoza nchi yake.

Pia shairi la" ngulu wapaona" lazungumzia mapenzi ya mtu kwa nchi yake. Mshairi

anaonesha umuhimu wa kuwa na mapenzi na kwenu hata kama ni porini. Anamtaka kila mtu kuthamini kwao hata kama kuna karaha.

"Mbali kuwa vipi,

Wazo huona pafupi

Hufika kwa sumaku

Hata ukiwa ulaya

Kwani hukana ngulu

Nguli wapaona

Kwa raha na karaha"

**-Pia mapenzi kati ya mwanamke na mwanaume:-**

**<u>Mapenzi ya dhati:-</u>**

Mapenzi kati ya Thomas na Dotto yalikuwa ya dhati bila kujali rangi na taifa. Mapenzi ya dhati huzaa matunda mema katika ndoa, Huzaa ndoa za kudumu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

zisizojali rangi, utajiri, utaifa au hali ya mtu, Ndoa ya uaminifu ni kama ile ya mashaka na dorothy.

“Ahadi zikawatoka

Wakasabai wanayakiuka

Kati yetu ndoa tutaiweka

Wote walitamka

Mapenzi hayana mipaka

Ndipo ilipotokea.

Mapenzi ya udanganyifu

Mapenzi ya udanganyifu huzaa ndoa za udanganyifu na mara nyingi hazidumu. Shauri la “Fikira za waungwana” linadhihirishwa wazi jinsi mapenzi ya udanganyifu yanavyosababisha ndoa za ulaghai, Mwandishi anasema,

“Mume wangu nakupenda, Josefu amenikuna

Nimekula nae tunda nampendelea sana

Ila usifanye inda mimi ni wako kimwana

Nitaishi kwa mpango, kwako na kwake Josefu”

Kwa upande mwingine katika shairi la “usiwe mwonja asali”mwandishi anaonesha jinsi tabia ya kujamiiana, inavyopelekea mapenzi ya udanganyifu, Inapasa kutunza heshima mpaka mtakapooana,

“Basi umwitae mwali

Yaani umwache mbali

Umwambie kwa kauli

Ukishamjua hali

Sahau kwamba ni mwali

Usiwe mwonja asali”

## 3. NAFASI YA MWANAMKE NA UMUHIMU WAKE

Mwanamke kama mwanamapinduzi na jasiri. Katika shiri la “Daktari Askari” mwanamke anaoneshwa akifanya kazi za kimapinduzi sawa na mwanaume. Kwani mwanamke anapigana vita ili kuikomboa nchi yake.

## 4. UMUHIMU WA KUTOA WOSIA

Mwandishi pia anashauri jamii kutoa wasio kwa familia zao kabla ya mauti kuwafika. Kupitia shauri la “Wasia” msanii anatilia mkazo kuwa siku yako ikifika ni muhimu kutoa wasia kwa familia yako kuhusu mambo ungependa wafanyeje baada ya kifo chako.

“Kwisha kuniweka chini

Udongo kishafukia

Na nyimbo niimbieni

Kwa mungu kuniombea

Katoliki yangu dini

Halafu nawaambia

Sherehe kazifanyeni

Kawaida ya tanzia”

· **UJUMBE**

- Ni lazima tujitoe mhanga ili kutetea wanyonge
- Mgawaniko wa watu kimatabaka husababisha utengano

- Dhuruma uongozi mbaya, ukosefu wa demokrasia ni baadhi ya vikwazo vya ujenzi wa jamii mpya

Suala la mapenzi waachiwe wawili wapendanao

· **FALSAFA**

Mwandishi anaamini katika kuwatetea wanyonge na kuleta haki na usawa kwa kila mtu vilevile uhuru katika mapenzi na ndoa.

**FANI**

Muundo- Mwandishi ametumia muundo changamano ametumia sana tarbia na sabilia.

Mtindo- Mwandishi ametumia mitindo changamano yaani kimapokeo na kisasa. Vilevile ametumia masimulizi.

Matumizi ya lugha- Lugha iliyotumika ni sanifu iliyosheheni misemo,nahau na methali na tamathali za semi

Misemo, Nahau na Methali, Mfano:-

- Sasa mwaleta shari (msemo)
- Umoja ni nguvu (methali)
- Kuvaa masulupwete (msemo)

Tamathali za semi:

- Tashibiha: Mfano: Kichwa chake kama cha kifutu
  - Shaba kama maji
- Tashihisi, Mfano: Kicheche pia ameapa
  - Jiji lasema hali ngumu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mioto ikapasua anga

- Sitiari: Mfano; Utoto ni kito

  Umaskini ni mzigo

- Tafsida, Mfano; Usiwe mwonja asali

  Dora ana kitu tumboni

  Nimekula nae tunda

- Tabaini: Mfano; Kuwaza na kuwazua

**MBINU NYINGINE ZA KISANAA**

- Takriri: Mfano: Adam, Adamu, Machozi

  Mama dora akaasa akaasa

- Nidaa: Mfano: Umeshituka! Ati mie mzee!

- Ono matopeo: Mfano: Lo! Looo!

Lugha ya kiingereza

- Movement order

- But this is was sir

Mandhari: Mwandishi amesadifu Tanzania na Uganda kipindi cha miaka ya 1980 pia kinazungumzia maudhui ya wakati huu wa sasa hususani nchi za ulimwengu wa tatu.

Jina la kitabu: Linasadifu yaliyomo ndani ya kitabu kwamba ukikutana na "chungu", pambana nayo ili kupata "Tamu"

Kufaulu kwa mwandishi

Kimaudhui; ameweza kuonyesha matatizo yaliyopo katika jamii tuliyonayo pia na kutoa mbinu za kutatua matatizo hayo.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kifani; Amefaulu kutumia miundo changamano pamoja na ujenzi wa taswira.

Kutofaulu kwa mwandishi

Lugha imejaa taswira sana na lugha ya kiingereza kiasi kwamba msomaji wa kawaida hawezi kuelewa zaidi ya walengwa.

· **UJENZI WA TASWIRA**

- Chatu” lnawakilisha wazulumaji (wakoloni)

Kuku ataga mayai

Chatu yake ataga

Kuku panya akimkuta

Panya anamkonyeza

Chatu apata kitoweo”

- **“Kuku**” inawakilisha wadhulumiwa (waafrika)
- “**Vifaranga”** inawakilisha malighafi

“Babu akaendelea

Akasema “namalizia”

Paku vifarana aliangua

Wengi chatu walijienea

Wachache wakabakia

Akiba chatu wajiwekea”

**“Ngulu”** inawakirisha vijijini sehemu isiyo na maendeleo,

Sehemu iliyosahaulika

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

"Mbali kuwe vipi

Wazo huona pafupi

Hufika kwa sumaku

Hata kuwe ulaya

Kwenu kukawa ngulu

Ngulu wapona

Kwa raha na karaha"

- **"Zabibu"** inawakilisha mwanamke au msichana
- "**Punda na ngamia"** wanawakilisha wananchi wanaoteswa na kunyanyaswa

"Punda na Yule ngamia

Wanajua kuvumilia

Hata njaa ya siku mia

Lakini siku zikiwadia

Vituko watavijua"

UHAKIKI-USHAIRI
JINA LA KITABU- KIMBUNGA
MWANDISHI- HAJI GORA HAJI
MCHAPISHAJI-TUKI
MWAKA – 1995

UTANGULIZI
Kimbunga ni diwani inayozungumzia juu ya mawaidha mbalimbali katika maisha pamoja na suala zima la ujenzi wa jamii mpya.Katika diwani hii,

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

mwandishi ametoa maadili na maonyo mbalimbali ya kufuata ili kufanikisha suala la ujenzi wa jamii hapa nchini.

**Maudhui**
Dhamira kuu- kuna dhamira kuu mbili katika diwani hii.

1.maonyo na maadili mema katika maisha

2. Ujenzi wa jamii mpya

**1. Maonyo na maadili mema katika maisha**
Mashairi mengi katika diwani hii yanazungumzia suala hili.Mwandishi amekuwa Mwalimu mzuri wa walimwengu kuhusiana na harakati mbalimbali za maisha.Mawaidha aliyoyatoa mwandishi ni kielelezo kizuri kinachofuatwa na kizazi hiki.Maadili na maonyo haya ni ya muhimu sana katika maisha.Maadili hayo ni kama vile:

**(a) Umuhimu wa malezi bora**
Malezi bora katika jamii ni njia pekee ya kuiweka jamii katika msingi bora wa maisha, katika shairi la "Vijana wa Zanzibar" (UK25) mwandishi ameonesha kuwa matendo ambayo vijana wa siku hizi huyatenda si mazuri ni ya kusikitisha .Anasema vijana wa siku hizi hawana utii, ni wajeuri,wadanganyifu, majambazi na pia hudharau mila na desturi zetu za asili na kukimbilia tamaduni kigeni.Rejea ubeti wa 2:

*"mwawacha yenu ya hapa,ambayo yako mazuri*
*Kutii na kuogopa mwaona haina heri*
*Mwayavamia kwa pupa, kwa hedi na ujeuri*
*Mila zetu za fakhari wacheni kuzipotosha."*

Kulingana na ubeti huu,mwandishi anaonesha kuwa suala la malezi bora ni muhimu sana katika jamii ili kuwaanda vijana wetu kuendana na mazingira wanamoishi.

Katika shairi la ``si vyema``(uk20) Mwandishi anajadili juu ya malezi bora kwa watoto na vijana ili wawaheshimu wakubwa wao Mwandishi anasisitiza umuhimu wa heshima katika suala zima mla maisha. Ni dhahiri kuwa vijana ambao hwakupata malezi bora tangu utoto wao wakiwa wakubwa hwawi na heshima wala nidhamu.

Kwa ujumla, katika suala la malezi mwandishi anafundisha jamii kuwa samaki mkunje angali mbichi.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**(b) Umuhimu wa kuwathamini wazazi**
Mwandishi ameonesha kuwa kuna umuhimu wa kuwaheshimu na kuwathamini wazazi.katika shairi la *"wazazi"* (uk.19) ameonyesha wazazi ndio ngao ya mtoto; mtoto hatakiwi kuwakasirikia,kuwaudhi wala kuwachukiza bali anatakiwa kuwa na mapenzi nao.Wajibu wa wazazi kwa mtoto ni kumpa chakula, mavazi malezi mema pamoja na elimu.Rejea ubeti wa 4:

*"Wakatafuta walimu, kukupatia ujuzi,*
*Wakakufunza elimu, pamoja na matumizi,*
*Sasa ni mtu timamu, waendelea na kazi,*
*Usiwaudhi wazazi, hiyo ndio yako ngao."*

Katika shairi la ``ulezi kazi``(uk22-23) Mwandishi ameonesha jinsi mama ( wazazi) wanavyohangaika kubeba mimba hatimaye kuzaa na kuanza kazi ya ulezi wa mtoto hadi anapofikia umri wa kujitegemea.Anaonesha kuwa wazazi
kupata taabu na shida mbalimbali katika ulezi wao.Hivyo mwandishi anashauri wazazi wathaminiwe na wapewe heshima zao.

**( c) Kuepukana na umbea:**
Umbea ni ile tabia ya kutoa maneno au habari kutumwa. Au ni ile hali ya uchongeaji au kilimilimi. Mwandishi anaona tabia hii si nzuri kwani huweza kutenganisha marafiki au ndugu kwa njia ya uchonganishi.
Katika shairi la *"wacha Hayo"* ( uk25) mwandishi anashauri jamii iepukane na umbea na badala yake ijishughulishe katika shughuli za uzalishaji mali.Madhara ya umbea ni kama vile majungu,uchochezi ubaguzi, kuvunja mafanikio,. umbea pia husababisha utengano ubeti wa 1 mwandishi anasema:

*"Wacha kupika majungu, na kuleta uchochezi,*
*Kuwajaza walimwengu,kasumba zile na hizi,*
*Hicho kimoja kifungu, kuletesha ubaguzi,*
*Tuacheni ubaguzi, huvunja mafanikio."*

Katika shairi la *"Hayafai Mitaani"* (uk.41) mwandishi anaonya jamii kwa si jambo la busara au zuri kusambaza taarifa au habari ya jambo Fulani sehemu ambayo haihusiki .Anaona kuwa busara sana endapo jambo Fulani limeafanyikia sehemu isiyohusika. Si tabia nzuri kulipeleka mitaani kwa watu wasiohusika Ubeti wa 2 anasema:

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

*"Yanayosemwa kunini, huko huwa yamekwishwa,*
*Haifai asilani, mitaani kufikisha,*
*Kwa siri ya mwituni, si vyema kuelewesha,*
*Ya kunini huishia kunini."*

Hapa mwandishi anatushauri kuwa jambo kuwa jambo moja likitendeka katika sehemu moja ni bora liishie katika sehemu hiyo na hakuna haja ya kupeleka katika sehemu nyingine.

**(d)Kuepukana na udokozi (tabia ya wizi)**
Udokozi ni ile hali ya kunyemelea vitu visivyo vyako kwa lengo la kuiba au kunyang`anya .Mwandishi anakemea tabia hii kwani anaiona si nzuri Tabia hii ipo miongoni mwa wanajamii mwandishi anaonya kuwa tabia uhatarisha maisha ya wahusika wenye tabia hii.
Mwandishi amemtumia paka kuwakilisha watu wenye tabia hiyo. Aidha mwandishi anaendelea kufafanua kuwa tabia hii husababisha uchokozi, hatari pamoja na chuki katika maisha .Shairi la *"paka"* (uk.12) linadhihirisha haya.

**(e) Kuendesha magari kwa uangalifu**
Mwandishi anawaonya madereva kuwa wanatakiwa waache tabia ya kuendesha magari kwa mwendo kasi unahatarisha maisha ya watu. Hivyo anawataka madereva kuzingatia umuhimu wa kuendesha magari mwendo unaofaa (usiowa kasi) Wa natakiwa wafikirie sehemu zenye mashimo , kona na milima vuilevile anawataka madereva wawe waangalifu katika mapishano ya magari barabarani .Pia wawe waangalifu wanapopishana na waendesha baiskeli , wapitao kwa miguu, viziwa, vipofu, vikongwe pamoja na wazee.Haya anayajadili katika shairi la "madereva" ( Uk. 43).

**(f) Umuhimu wa shukrani katika maisha**
Mwandishi anaidilia jamii umuhimu wa kutoa pale mtu anapofanyiwa hisani na mtu mwingine.katika shairi "*Punda*" ( uk 21) mwandishi ameonesha jinsi baadhi ya watu wasivyo kuwa na shukrani katika maisha . Ameonesha kuwa mwanadamu asiye kuwa na shukrani hata umfanyie wema kiasi gani hawezi kutoa shukrani .Ameelezea kuwa mtu asiye na shukrani ni wakuachana naye au kumtenga (kutengana naye) kabisa.
Anasema:

*"Punda hakumbuki wema, hata kwa mchunga wake,*
*Humpa mwingi mtama, na maji anufaike,*
*Katu hawi salama, shukrani zake mateke,*
*Ndiyo tabia ya punda, kurusharusha mateke,*
*Kuchunga akikushinda, mwache awende zake."*

Katika ubeti huu mwandishi anasisitiza umuhimu wa kutoa shukrani pale unapofanyiwa fadhila.

**(g) Umuhimu wa kulipa deni**
Mwandishi anawaonya wale watu wenye tabia kutolipa deni.Anawaona kuwa ni wadanganyifu , waongo , walaghai.wanafiki na wajanja .Mwandishi anawashauri wale wote madeni kulipa madeni hayo kwa hiari na anawaonya wasijifanye wajuaji kwani wakigundulika watapata hasara .Anaendelea kuwaambia kuwa kulipa deni ni wajibu wa kila mwenye deni .vile anaonesha kuwa . kukwepa deni si haki Anayesema haya katika shairi lan "Dawa ya deni ni kulipa" (uk.32) ubeti wa 3 anasema:

*"Ulipofikwa na dhiki, la kufanya hukujua,*
*Kukopa ukaafiki, kwa shida kuiondoa,*
*Kukwepa deni si haki, utakuja athiriwa,*
*Huwezi kuaminiwa, kama hutojiamini."*

Mwandishi amefafanua kuwa mtu anayeshindwa kulipa deni hawi tena mwaminifu katika jamii.Na matokeo yake kushindwa pa kukopa pindi apatapo shida.

**(h) Faida ya kujiwekea akiba**
Katika shairi la *"usimalize"* (uk. 27) mwandishi anafafanua umuhimu wa kujiwekea akiba .Ubeti 4 anasema:-

*"Akiba ni yako ngao, dhiki inapokunasa,*
*Si wajinga wawekao, hukataa kujitesa,*
*Hutambuwi uchao,lipi litalokugusa,*
*Akiba haichakai."*

Katika ubeti huu mwandishi anasisitiza umuhimu wa kujiwekea akiba kwani hutusaidia sana wakati wa dhiki.

2. Ujenzi wa jamii mpya
Pia mwandishi amejadili dhamira ya ujenzi wa jamii mpya katika kazi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

yake.Katika diwani hii mwandishi ameonesha vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha ujenzi wa jamii mpya hapa nchini .Vikwazo hivyo ni kama vile uongozi mbaya ,rushwa tamaa ukosefu wa elimu ukoloni mamboleo n.k
Katika kujadili dhamira hii mwandishi ameonesha mbinu mbalimbali ambazo zinatumiwa na jamii hii kufanikisha zoezi zima la ujenzi wa jamii mpya nchini. Mbinu hizo ni pamoja na:

**(a) Uongozi mzuri**
Uongozi mzuri unahitajika kwa jamii yoyote ile ili kuleta ufanisi mzuri. Uongozi mbaya unasababisha kushindwa kufikia ufanisi mzuri.Kutokana na uongozi mbaya ndiyo maana jamii hufikia kufanya mapinduzi.

Katika shairi la *"kimbunga"* (uk. 1) mwandishi anaongelea juu ya mapinduzi yanayofanywa na tabaka la chini dhidi ya tabaka tawala. Anatumia mji wa *siyu* kuwa kielelzo kizuri kwa jamii yoyote inayotaka kufanya mapinduzi ili kuondoa viongozi wabovu na kuleta viongozi bora.Katika mapinduzi hayo mwandishi amefafanua kuwa wengi ndio wanaoathirika na wachache hunusurika.

Shairi la *"madanganyo"* (uk.6) linazungumzia jinsi uongozi mbaya unavyowadanganya wananchi , unavyowaadhiri na kuwakera wananchi.Wananchi hushiriki katika uzalishaji mali (miradi mbalimbali) lakini matunda ya jasho lao hufaidiwa na wachache.Wachache hao husahau wale waliosulubika katika uzalishaji ubeti wa 6 mwandishi anasema.

*"Mlitupigia mbiu, tulimeni ushika,*
*Tukakatana miguu, kwa mapanga na mashoka,*
*Manufaa kwa wakuu, wadogo yetu mashaka,*
*Wezeni kutukumbuka, mjue nasi wenzenu."*

Shairi la *"Wenye Navyo Watubana"* (uk. 8) mwandishi amejadili juu ya wenye utajiri au vitu jinsi wanavyowagadamiza kuwanyonya na kuwabana wale wasio na chochote .Mwandishi anawaomba viongozi wawatetee ili kuepukana na hali hii.Hii ni kutokana uongozi mbaya ndio maana hali kama hii ipo nchini lakini viongozi hawachukui tahadhari.

Ubeti wa 7 mwandishi anasema:

*"Maji yamezidi unga, kwa lochi wa darajani,*
*Kujitolea mhanga, kwa bei haiwezekani,*
*Mvao wake wa kanga, ni shilingi elifu."*
*Wakubwa tuteteeni wenye vyao watubana"*

Shairi la "*kimbwangai*" (uk9-11) linajadili dhana ya viongozi wetu kwa wananchi wanaowaongoza.Mwandishi ameonesha jinsi wananchi wanavyowachagua viongozi wao lakini viongozi wao wakishapata madaraka huwageuka na kuwasaliti wananchi Anasema hayo kwenye ubeti wa 7:

*"Kimbwangai alipoona, ni mtu kukamlika,*
*Akaanza kujivuna, na dharau kuzidiya,*
*Wala hakujali tena, wenzake walimwambiya"*
*Akahisi hawi nyani, umbo lile litadumu."*

Shairi hili, limejengwa kitaswira -Hapa *kimbwangai* ametumia kuwakilisha viongozi wasaliti na *nyani* kuwakilisha wananchi wanaowaongoza na akina kimbwangai.

Katika shairi hili la "*Hili Mnatutakiya* "(uk.18-19) mwandishi anaonesha jinsi vyombo vya dola vinavyoshindwa kuteleza wajibu wake wa kuwalinda raia na kuwashughuikia wahalifu.Mwandishi ameonesha kuwa vyombo hivyo vinawalinda wezi.

Katika diwani hii mwandishi anaonesha kuwa uongozi mbaya ni kikwazo cha ujenzi wa jamii mpya na ili tujenge jamii mpya lazima tuwe na uongozi bora.

**(b) Kupiga vita rushwa**

Rushwa ni kikwazo kingine kinachokwamisha ujenzi wa jamii mpya kutokana na kukithiri kwa rushwa katika jamii haki hupotea, wachache wanafaidi na wengine wanaendelea kuumia shairi la "*Rushwa"* (uk.12) linadhihirisha kauli hii kama asemavyo mwandishi.

*"Rushwa kajenga kambi, na kuondoka hataki,*
*Afanya kila vitimbi, mkaidi hashindiki,*
*Tumzushie wimbi, isiwe kutahiliki,*
*Tumechimbia handaki, rushwa tukamzikeni."*

Katika ubeti huu mwandishi anatuonesha kuwa lazima jamii yetu itupilie mbali rushwa ili haki na usawa vitawale.Kupiga vita rushwa ili mbinu ya ujenzi wa jamii mpya ambayo mwandishi ameipendekeza.

(c ) Umuhimu wa Elimu
Ili tuweze kufanikisha zoezi la ujenzi wa jamii ni lazima watu wapate elimu bila kujali umri. Mwandishi ana wa himiza wazee kujiunga na kisomo cha manufaa ili wafute ujinga wa kutokujua kusoma na kuandika.Haya mwandishi anayasema katika shairi a *"kisomo cha Manufaa"* (uk.2-3) na katika shairi hili mwandishi anawahimiza wazee wajiunge na elimu ya watu wazima kwa sababu wakishaelimika watakuwa na uwezo kupanga mipango yao ya maendeleo .Mwandishi anaonesha kuwa elimu ni silaha madhubuti katika kufanikisha zoezi zima la ujenzi wa jamii mpya. Pasipokuwa na wasomi katika jamii hii yetu zoezi la ujenzi wa jamii mpya litakwama.

(d) Kupiga vita ukoloni mamboleo.
Ukoloni mamboleo ni kikwazo kikubwa kinachokwamisha maendeleo ya uchumi hapa nchini.Na ili tuweze kufanikisha ujenzi wa jamii mpya hapa nchini,katika shairi *"Chuwi"* mwandishi anaonesha jinsi ukoloni mambo leo unawaathiri sana watu tabaka la chini la wasio na chochote na kuwasetiri matajiri au tabaka la juu katika ubeti 6 mwandishi anasema:

*"Ambao ni matajiri, kwao anapowafikiriya,*
*Huwezi kujisetiri, salama kujipatiya,*
*Walokuwa mafakiri, huzidi kuwaoneya,*
*Huyu ndiye chuwi gani?"*

Mwandishi amefafanua kuwa ukoloni mamboleo huingia kwa njia mbalimbal kwa nchi zinazoendelea.Hivyo mwandishi anatahadhalisha kuwa tuepukane na mbiu (njia) hizo ndipo tutaweza kujenga jamii mpya.

**(e) Umuhimu wa kujitawala**
Ili tuweze kujenga jamii mpya ni lazima tujitawale katika fani zote za kifikra, kisiasa, kiutamaduni pamoja kiuchumi. Katika shairi la ``Afrika `` ( uk1-2) mwandishi amefafanua kuwa ili tuweze kujitawala ni laziam tuepukane na unafiki, vibaraka, wasaliti, mahusuda tusikate tama, vile vile tudumishe amani. Mwandishi anaonesha hayo katika ubeti 3:

*"Wasaliti wazikishe, wasio wenye kuzuzuka,*
*Tamaa mwakilishe, yasiwe unayotaka,*
*Katu wasiwawezeshe, wabakie kuzuzuka,*
*Katu washidike mahusuda, wasiopenda bara letu."*

Katika shairi la "*kujitawala*" ( uk. 7-8) mwandishi amefafanua umuhimu wa kujitawala kwa jamii yoyote ile . Na mwandishi anaonesha kuwa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kujitawala kwa jamii yoyote ile. Na mwandishi anaonesha kuwa kujitawala ni pale umma unapoamua mambo yao wenyewe bila kuingiliwa kuwekewa vikwazo vyovyote mwandishi anasema:

*"Kujitawala ni kwema, kulikoni kutawaliwa,*
*Kujitawala ni umma, kila yao kuamua…"*

Katika shairi hili la kujitawala mwandishi anaonesha faida mbalimbali za kujitawala kama vile demokrasia,kuwepo umoja na ushirikiano kuwepo haki na usawa amani hudumishwa.Hivyo mwandishi anatuonesha kuwa ili tujenge jamii mpya ni lazima tujitawala kisiasa kiuchumi kuitamaduni kifikra.

**(f ) umuhimu wa kazi na kuwajibika**

Kazi ni nyenzo muhimu sana ya ujenzi wa jamii mpya .Mwandishi amesisistiza umuhimu wa kazi na uwajibikaji katika shairi la `` kazi`` (uk 17) Mwandishi anatuonesha kuwa kazi ndio msingi wa maendeleo .Anasisitiza umuhimu wa kufanya bidii na tuepukane na uvivu .Ubeti wa 1 mwandishi anasema. *"Pesa huleta kazi ni njia zipiitiayo,…"*

Katika shairi la *"Uokolewe"* mwandishi anasisitiza umuhimu wa kudumisha umoja mshikamano ili kuinua uchumi wetu Anasisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii katika rasilimali zetu za kuinulia uchumi wetu . Rasilimali hizo ni pamoja ukulima , uvuvi , utalii na viwanda.

Katika shairi la "Mkarafuu" (Uk. 29-30), mwandishi anafafanua umuhimu wa zao la mkarafuu katika uchumi wa Zanzibar .Anasisitiza kuwa ni muhimu ila mtu alithamini zao hili.

Katika shairi la *"Dumizi"* (uk. 41) mwandishi anakemea ile tabia ya baadhi ya watu kukaa bila kazi (uvivu) na kuanza maisha ya kunyonya .Hivyo mwandishi anapiga vita unyonyaji wa watu waishio kwa jasho la wenzao.

Kutokana na maelezo haya yote , dhahiri kuwa kazi ni msingi wa maendeleo na ili tuweze kujenga jamii mpya ni lazima tujue umuhimu wa kazi na kuwajibika.

**Dhamira nyinginezo ( Ndogonodgo)**

(1) Mapenzi na ndoa

Katika diwani hii, mwandishi ameonesha kuwa mapenzi yameganyika katika pande kuu mbili kuna mapenzi ya kweli na mapenzi ya udanganyifu .

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Katika shairi la "Usimpige Mkeo" (uk.12) mwandishi anasema kuwa haifai mwanamume kumpiga mke wake na vilevile wnamume hatakiwi kumwekea mke wake masharti magumu .

Shairi la "Hongera" (Uk.16-17) mwandishi anaendelea kujadili suala la mapenzi na ndoa katika jamii zetu .Anawaonya bibi na bwana wasiwe na tabia kufukuzana wawapo nyumbani .Amewapa m kila mmoja maadili yake kwa mwenzake. ubeti za (4-5) mwandishi anasema:

4- *"Bi harusi yangu shika, uyatie akilini.*
*Mumeo akifika, anapotoka kazini,*
*Mpe mema mamlaka, aliwazike moyo,*
*Hongera"*

5- *Bwana harusi sikia, ukiwa kwako nyumbani,*
*Maneno ya kutupia, hayafai asilani,*
*Kauli njema tumia, na lugha iwe laini,*
*Hongera"*

Katika shairi "*Sifa ya Mke"* (uk.40) mwandishi anaonesha kuwa sifa kubwa ya mwanamke ni tabia wala si sura . Sifa ya tabia njema humpa mwanamke taadhima , huruma ,utiifu na hata uhodari .Anafafanua sifa za mwanamke kuwa awe mtulivu kiruka njia asiwe na ufedhuri wa aina yeyote ya uovu. N.k

Katika shairi la *"sitaki"* (uk44-45) mwandishi anakemea mapenzi ya udanganyifu yaliyoshamiri katika jamii zetu kwa wakati huu. Anasema:

*"Rabi simpe mapenzi, hakuna wa kuamini,*
*Wapendwa wenye ujuzi, ni wachache duniani,*
*Mapenzi yamepotea, sasa ni adimu sana"*

Ni kweli mapenzi ya siku hizi hutawaliwa na pesa na yamejaa ulaghai wa kila aina pamoja na udanganyifu.

**(ii) Maradhi ya hatari**

Mwandishi amejadili maradhi mbalimbali yanayozikumba jamii zetu na ameonesha njia zianazosababisha maradhi hayo na njia za kuepukana na maradhi haya.

Katika shari la "*Vielezo"* (uk. 3-4) mwandishi amejadili juu ya ugonjwa wa UKIMWI (AIDS), ameonesha kuwa ugonjwan huu huambukizwa kwa njia

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

zifuatazo: uasherati juongezewa damu isiyojunguzwa kudungwa sindano zisizochemshwa mbinu anayoipendekeza ya kuondokana na (kuepukana) na ugonjwa huu ni kuacha tabia ya uzinzi na uasherati.

Shairi la *"Usafi"* (uk 13) mwandishi amejadilii juu ya ugonjwa wa kipindupindu Ameonesha kuwa hakuna umaarufu wowote bali ni kumaliza ugonjwa husababishwa na uchafu wa mazingira . mbinu ya kuepukana na ugonjwa huu husabishwa kudumisha usafi wa mazingira yetu.

Katika shairi la "Mnapata kitu Gani" (uk.26-27) mwandishi anaiadilia jamii juu ya madhara ya kuvuta sigara amesema kuwa uvutaji sigara Anasema kuwa kuvuta sigara pesa bure Ugonjwa wa kansa hutokana na madhara ya sigara na ili kuepukana na ugonjwa huu hatuna budi kuepukana na uvutaji wa wa sigara.

**Ujumbe**

- Dhana potofu ya kudhani bila kuwa uhakika wa mambo haifai katika jamii kwa sababu hupotosha ukweli wa mambo.
- Mapenzi na ndoa ya dhati ni muhimu katika jamiii zetu.
- Ukoloni mamboleo uongozi mbaya , rushwa ukosefu wa elimu ni baadhi ya vikwazo vya ujenzi wa jamii hapa nchini.
- Maadili mema na maonyo ni njia pekee ya kuiweka jamii katika misingi ya haki na usawa
- Baadhi ya maradhi tunayojitakia sisi wenyeywe.

Falsafa

Mwandishi anaelekea kuamini kuwa maadili mema na maonyo ni njia pekee ya kuiweka jamiii katika msimamo wa mwenendo bora wa maisha . Pia mwandishi anatetea misingi ya haki na utu katika jamii.

Msimamo

Msimamo wa mwandishi una hali ya udhanifu pia kuwa na misingi ya kisayansi,Udhanifu wa mwandishi unadhihirisha kwenye *kipaji cha lugha ya kiswahili hali katika maisha pamoja na bahati.*

Fani

a) Muundo

Ametumia muundo wa tarbia (mistari 4) kwa kiasi kikubwa. Ametumia muundo wa tathlitha (mistari 3) katika shair la "*kujitawala"* (Uk.7-8) pia

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ametumia muundo wa takhimisa (sabilia) mistari 5 na kuendelea katika shairi la "*Punda*" (Uk.21-22), shairi la "Bahati" (Uk.36).

b)Mtindo
Mtindo uliotumika ni ule unaofuata kanuni za mapokeo za urari wa vina na mizani pamoja na mpangilio wa beti.karibu mashairi yote yana vina vya kati na mwisho isipokuwa mashairi ya *"kimbunga"* (uk. 1) "*Dumuzi"* (uk41) "*Madereva"* (uk.43) "chuwi" (Uk. 42) yana nusu mstari katika kituo.

c) Matumizi ya lugha
Mwandishi ametumia lugha rahisi iliyoshehenezwa lahaja ya kiunguja yenye mafumbo na taswira mbalimbali na tamathali za semi kidogo na misemo kwa kiasi.

**Tamathali za semi**

**Tashibiha :**

- Kwenye shairi la "*Sifa ya Mke"* - ( Uk.40)
- Ufedhuli na uovu kama yake mazoea.
- Awe kama malaika kupindukiya.

**Tafsida**
Mwandishi ametumia mbinu ya kufumba kwa kusema maneno makali, machafu, matusi kwa kutumia tafsida. Mfano shairi la "*Nyang'au"* (uk.44) linahusu tamaa "*Paka*" (uk. 22) linahusu wizi shairi la "*Dumuzi*" (uk.41) linakemea uvivu n.k.

**Mbinu nyingine za kisanaa**

*Takriri*: ili kuweka msisitizo mfano shairi la "kujitawala" neno kujitawala limerudiwarudiwa.

**Matumizi ya taswira**
Taswira nyingi zimetumika.

Mfano: Kimbunga- (Uk.1) - Kuashiria mapinduzi
kimbwangai (Uk.9) - Kuashiria viongozi wasaliti

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Nyani (Uk.9) -kuashiria wananchi wasalitiwa
Chuwi (Uk.42) - kuashiria ukoloni mamboleo n.k

**Jina la kitabu**
Jina la kitabu *kimbunga* halisadifu yale yaliyomo ndani ya kitabu kwa sababu hatuyaoni mageuzi yoyote ambayo anayajadili katika kitabu hiki zaidi ya mashairi ya maadili mema na maonyo ya kimaisha aslimia kubwa ya mashairi katika diwani hii yamejadili juu ya maonyo na maadili katika maisha.

**Kufaulu kwa mwandishi**

**Kimaudhui**

- Kutoa maadili mema na maonyo katika jamii.
- Kujadili dhamira ya ujenzi wa jamii mpya.
- Ameonesha mbinu mbalimbali za kufuata ili tufanikiwe katika ujenzi wa jamii mpya.

**Kifani**
-Ametumia lugha rahisi, mafumbo,taswira n.k.

**Kutofaulu kwa mwandishi**

*Kimaudhui*

- Baadhi ya maadili aliyoyajadili katika kitabu hiki ameyajadili kidhanifu, ni sawa na yale tunayoyapata makanisani ambayo yana nafasi ndogo sana katika ujenzi jamii mpya.
- Vilevile amejadili masuala mbalimbali kidhanifu hasa anapomhusisha Mungu.Kama maswala ya kipaji ( uk 38-39) bahati ( uk 36) umasikini ( uk35)*Kifani*
- Kutumia lahaja ya unguja badala ya Kiswahili sanifu.
- Diwani hii ni hali ya chini sana katika muundo, mtindo na baadhi ya vipengele vingine vya
kisanaa.

**TAMTHILIYA YA "KWENYE UKINGO WA THIM"**

**MWANDISHI: I. HUSSEIN**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

**MCHAPISHAJI: OXFORD UNIVERSITY PRESS**

**MWAKA: 1998**

## UTANGULIZI

Tamthiliya hii inaonesha na kuibua mgogoro uliopo katika mila na yale ya kisasa yaani ukale na usasa, Pia tamthiliya hii inaonesha uonevu uliopo dhidi ya wanawake na jinsi mwanaume anavyo pendelewa katika sheria za taasisi za utamaduni wa mwafrika.Kwa upande mwingine mwandishi ameonesha jinsi mvutano huo unavyoleta athari kubwa kwa jamii.

## A. MAUDHUI

· **DHAMIRA KUU**

1. **UKOMBOZI WA KIUTAMDUNI**

Mwindishi ameonesha kasoro mbalimbali zinazojitokeza katika utamaduni wa mwafrika kama anavyosema katika utangulizi wake.

“katika kutumia na kufasiri kipengele cha utamaduni wa mwafrika kama nilivyofanya mimi katika mchezo huu ,nimehisi kuna walakini.”

Walakini anazoziona mwandishi zinaathari mbaya kwa jamii kwani ndizo zinazo sababisha mvutano kati ya ukale na usasa ambao ndiyo kiini cha tamthiliya hii,

Ndoa ya Hebert na Martha ambao walioana kutoka makabila tofauti ndiyo yaliyo changia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mvutano huu wa kale na usasa katika tamthiliya hii. Jamii nyingi za kiafrika mila na desturi zake haziruhusu mwanamke kuolewa au mwanaume kuoa nje ya kabila lake. Kutokana na mila hii kushikiliwa na baadhi ya jamii za kiafrika, inazua mvutano kati ya vijana na wazee, vijana hawaoni sababu ya kuzuiwa kuoa au kuolewa na mtu asiye wa kabila lake wakati wao wanapendana.

Kwa upande mwingine mvutano huu unachangiwa na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kitamaduni kwasababu matatizo hayo hayajawakumba wazee wanaong’ang’ania mila na desturi hizo ambazo zimepitwa na wakati. Wakati vijana wanaona mabadiliko hayo ni ukombozi kwa upande wao kama lidya anavyosema

“ndiyo ukweli wenyewe siku hizi mambo ya kisasa ,kila kitu cha kisasa, mtazame Hebert au Martha.hii habari ya kuoa kabila moja imekwisha kila unaemuona hivyohivyo hata chris.”

Kutokana na dondoo hii mwandishi anasisitiza kuoa ili jamii iweze kujikomboa kiutamaduni, ni lazima itupilie mbali mila na desturi zote zilizopitwa na wakati kwani hazina nafasi katika kizazi cha sasa. Masuala ya ndoa yanapaswa yaamuliwe na wapendanao na si mila na desturi katika jamii.

Athari hii ya kung'ang'ania ukale kwa upande mwingine ipo hata kwa wasomi. Kwa mfano Ben ambae ni kaka yake Martha msomi na mwalimu wa chuo kikuu anaamini mke wa kweli ni lazima atoke kataka kabila lake. Mwandishi amedhihirisha hayo kati ya mazungumzo ya Hebert na Ben wakati wakizungumza kuhusu ndoa ya Hebert na Martha.

(uk.11)

"BEN: toka huyo mwanamke ameolewa na wewe, mimi simjui kama dada yangu labda ni bibi yako tu.

"HERBERT: wewe huoni haya kuwa mkabila namna hii..................siwezi kuelewa wasomi chukua mtu kama wewe umesoma alafu unasomesha chuo kikuu na bado ni mkabila wa kutupwa."

Ukabila unapokithiri na kuota mizizi katika jamii huwa una madhara yake. Mfano unaweza kupelekea watu kuuana ovyo kama ilivyo tokea Burundi na Rwanda. Kutokana na ukabila huo huo kikatokea kifo cha Hebert.

Kwa upande mwingine mwandishi ameonesha kuwa utamaduni wa kiafrika una mgandamiza na kumwonea mwanamke. Mila na desturi za utamaduni wa kiafrika zina mnyima mwanamke haki ya kuamua badala yake mambo yake mengi yanaamuliwa na mwanaume.

Mwanamke ananyimwa haki ya kurithi mali alizochuma na mume wake pindi anapo kufa.

Mwandishi pia anaonesha kuwa mila na desturi za utamaduni wa kiafrka zinamwonea mwanamke na kumpendelea mwanaume.

Vilevile mwandishi anaonesha kuwa baadhi ya watu hasa wasomi waliobahatika kuhamia mjini wana kawaida ya kusahau kwao, kwa mfano Hebert ambaye alikuwa msomi ambaye alipata kazi mjini alipasahau kabisa kijijini kwao hata kujenga kibanda cha kujisitiri alishindwa, tabia hii si ya Hebert tu katika jamii kuna watu waliotawaliwa na anasa za mjini na kusahau kijijini kwao.

- **DHAMIRA NDOGONDOGO**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

## 2. NAFASI YA MWANAMKE

Katika tamthiliya hii mwandishi amemwonesha mwanamke katika pande kuu mbili,

- Kama mwanamapinduzi kwa kushiriki vita vya msituni vya mau mau sambamba na wanaume,dhidi ya ukoloni wa kiingereza.(martha)

- Mwanamke kama kiumbe duni. Mwandishi ameonesha jinsi utamaduni wa mwafrika unavyomwonea na kumgandamiza mwanamke. Mila na desturi zina mnyima mwanamke haki zake kama vile ambavyo mwanaume anavyozipata.mwandishi ameonesha jinsi mwanamke anavyoonewa na mwanaume kupendelewa

> "Mwanamke utakuwa na pesa ulizozipata kwenye kibarua, Utafunga ndoa, na kuanzisha familia lakini huko ni kubahatisha tu.ukipatana na mumeo basi hiyo ni bahati yako, La hamkupatana ndio umepata maisha yako (martha)"

Hapa mwandishi anaonesha kuwa mwanamke ananyang'anywa hata kile kidogo alichochuma na mume wake, jambo hili lipo kwenye jamii nyingi za kiafrika ambapo wanawake wengi hawamiliki chochote isipokuwa yeye anamilikiwa na mwanaume.

Mwandishi pia anaonesha wanaume wanavyopendelewa wana uhuru wa kufanya chochote bila kipingamizi chochote. Wana uwezo wa kutafuta mke mwingine, kwenda kilabuni na kukaa na wenzao bila kipingamizi. Lakini mwanamke hana uhuru wa kufanya vitu hivyo.

Mwanamke anaonesha jinsi mwanamke anavyonyimwa uhuru wa kufanya mambo anayotaka, hii ndo hali halisi katika jamii nyingi za kiafrika.

Vilevile anaonesha jinsi mwanamke anavyonyimwa haki ya kurithi mali aliyochuma na mumewe alipokuwa hai. Martha alinyang'anywa kila kitu baada ya kifo cha mumewe Kwanza anampoteza mumewake, pili ananyang'anywa mali na kila kitu na familia ya mume wake.

Mwandishi katika kutahadharisha vitu kama hivi ni lazima waandike wasia kabla hawajafa ilikuepusha migogoro.

Mwanamke ananyimwa uhuru wa kumzika mumewe pindi anapokufa, Mfano Martha alipo nyimwa kumzika mumewe.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mwandishi anaonesha kuwa ili tuweze kujikomboa kiutamaduni ni lazima tutupilie mbali baadhi ya mila na desturi zinazomnyanyasa, zinazomwonea na kumgandamiza mwanamke ambazo bado zipo katika jamii yetu.

## 3. MALEZI

Ni moja kati ya dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya hii Mwandishi kaonesha kuwa malezi mabaya huwa na athari mbaya kwa watu husika hapo baadae katika tamthiliya hii mwandishi ameonesha malezi aliyopewa chris na wazazi wake ya kuishi kuambiwa baba yake halisi ni kinyume na malezi bora kwa watoto. Martha na Hebert hawakumwambia ukweli chris kuwa Hebert hakuwa baba halisi wa chris mpaka alipokuja kugundua ukweli mwenyewe pale Hebert alipokufa. Jambo hili lilizua utata mkubwa kati ya Chris na mama yake.

Vilevile kitendo baba na mama kucheza kwa kukumbatiana mbele ya watoto ni kinyume cha utamaduni wa kiafrika. Huu ndio utamaduni wa mwigo kutoka katika utamaduni wa kigeni.

Mwandishi anatahadharisha kuwa tabia hii ina athari kubwa katika jamii kwa sababu tuna wafundisha watoto utamaduni wa kigeni ambao hauendani na mazingira yetu.

## 4. NDOA

Katika kujadili dhamira hii mwandishi anaonesha wazi jinsi utamaduni wa kiafrika unavyoathiri ndoa nyingi katika jamii. Vijana wengine wanashindwa kuoana kutokana na sheria mbalimbali zinazokumbatiwa na utamaduni wetu. Mfano ndoa ya Hebert na Martha ambao walioana kutoka makabila tofauti wametengwa kwa madai ya kukiuka taratibu za makabila.

“jamaa zangu damu moja, wamenitenga siku ya ndoa. Ben peke yake ndo alikuwa na mimi, Jamaa wa mume wangu nao walimtenga siku hiyohiyo.”

Kutokana na dondoo hii mwandishi anaonesha kuwa baadhi ya tamaduni zetu zina wanyima vijana uwezo wa kuamua nani awe mke wake au mume wake. Jambo hili lina athari kubwa kwa jamii.kwani husababisha mvutano kati ya watoto na wazazi wao.

## 5. UKABILA

Dhamira hii inajitokeza pia katika kitabu hiki ingawa tatizo hili linaonekana kubebwa na mila na desturi za utamaduni wetu. Hubert alikatazwa na ndugu zake kumuoa Martha kwa kuwa Martha alikuwa mkikuyu na yeye ni mjaluo. Na hata baada ya Hebert na Martha kuoana kwa kulazimisha ndugu zao waliwatenga.kutokana

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

uhasama mkubwa uliopo kati ya makabila haya ya kikuyu na ujaluo unasababisha matatizo makubwa katika ndoa ya Hebert na Martha.

Kwa upande mwingine katika nchi ya Kenya ambapo makabila haya yanatokea kumekuwa na hali ya kuhasimiana na mapigano ya hapa na pale kati ya makabila haya mawili. Kwa ujumla ukabila unapozidi huwa na madhara makubwa kuliko faida.

## 6. DHANA POTOFU

Mwandishi anaonesha kuwa kuna baaadhi ya watu wana imani potofu kwa uonevu na unyanyasaji wa mwanamke katika jamii unatokana na maamuzi ya mungu. Mwandishi anasema;

“huwezi kujua la kufanya mwachie mungu”.

Pastor anaamini kuonewa na kunyanyaswa kwa mwanamke ni mipango ya mungu na mwanamke kamwe hawezi kutafuta suluhu bali amwachie mungu.

Kwa upande mwingine pia pastor anaamini kuwa tajiri au maskini ni mipango ya mungu. Pastor anaonesha kuwa utajiri wa Martha na Hebert walipewa na mungu. Na hata baada ya Martha kunyang’anywa kila kitu na George na Umma klan anaona kuwa ni kazi ya mwenyezi mungu.

“unakumbuka uliponunua nyumba hii,.......

bustani hizi ulijiona umefika.

Sasa aliyekupa vyote hivyo amevichukua vyote...

hii ni kazi ya mungu na kazi ya mungu haina makosa.”

Mawazo haya ni potofu na hayana ukweli kwani utajiri au umaskini hautokani na mpango wa mtu bali mfumo wa jamii unaotawala ndiyo unaotabiri utajiri au umaskini wa mtu.

## 7. UTEKELEZAJI MBOVU WA MIPANGO YA MAENDELEO

Mwandishi amejadili dhamira ya uamuzi mbaya wa mipango ya maendeleo ya taifa. Anaonesha jinsi viongozi wanavyopingana wao wenyewe katika utekelezaji wa maamuzi yanayohusu ujenzi wa taifa letu. Mwandishi anaonesha kuwa kiongozi Fulani na kuwaagiza wananchi wayatekeleze lakini anakuja kiongozi mwingine wa juu na kuwakataza wananchi wasitekeleze maamuzi hayo na wananchi wanapoacha kutekeleza anapokuja kiongozi mwingine anawahimiza wafanye tena. Hali hii

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

inasababisha utata kwa wananchi katika kutekeleza mipango ya maendeleo kwa sababu wanashindwa kuelewa washike la nani waache la nani. Kutokana na hali hii wananchi wanakua na mchangamano wa mawazo ambao kwanamna moja au nyingine yanakwamisha swala la ujenzi wa jamii mpya.

## 8. NAFASI YA MWANAUME KATIKA JAMII.

Mwandishi amemchora mwanaume katika nafasi mbalimbali,

- Kama mwanamapinduzi anaye hitaji mabadiliko katika mila na desturi za utamaduni wetu. Mfano Hebert aliyekubali kutengwa na familia yake ili aweze kumuoa Martha ambaye ni mtu wa kabila tofauti na lake.

- Kama mtu anaependelewa na mila na desturi za utamaduni wa mwafrika. Ana uhuru wa kuoa mke zaidi ya mmoja, kwenda atakako, kurithi mali n.k.

- Mtu katili na asiye na huruma. Mfano George ambaye alikuwa shemeji yake Martha. Alimnyang'anya Martha mali na kila kitu akimnyima hata haki ya kumzika mumewe.

## B.MIGOGORO

**Katika tamthiliya hii kumejitokeza migogoro kadhaa kama ifuatavyo;**

1. Mgogoro kati ya ukale na usasa. Mgogoro huu chanzo chake ni baadhi ya watu kuendelea kung'ang'ania mila na desturi ambazo zimepitwa na wakati katika jamii na hivyo kukwamisha ustawi wa jamii kwa namna moja au nyingine. Wakati watu wengine (vijana) wanaona kuwa ni lazima yafanyike mabadiliko katika mila na desturi hizo ili kuweza kuendana na mabadiliko na wakati huu wa sasa. Suluhisho ni kwamba inabidi yafanyike mabadiliko katika mila na desturi zinazoonekana kupitwa na wakati, Kwa mfano sio lazima mke/mume atoke kwenye kabila lako. Ni lazima kuwe na haki sawa kati ya wanawake na wanaume.

2. Mgogoro kati ya Chris na Martha. Chanzo chake ni Martha, mamake mzazi Chris kutomwambia chris kuwa Hebert hakuwa baba yake mzazi bali ni baba mlezi. Martha alikaa kmya hakumwambia Chris ukweli ingawa haikuwa sahihi kufanya hivyo.

3. Mgogoro kati ya Hebert na George. Chanzo ni Hebert kukataa kwenda kijijini kwenye harusi. Suluhisho ni Hebert kutokwenda kabisa nyumbani kwao.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

4. Martha na George na umma klan. Chanzo cha mgogoro ni Martha kudhulumiwa kila kitu baada ya kifo cha Hebert pamoja na kunyimwa haki ya kwenda kumzika mumewe. Aliamua kutafuta ushauri lakini hakupewa ushauri wa maana.

5. Mgogoro kati ya ben na Hebert. Ben hakukubaliana na Hebert kumuoa dada yake. Suluhisho ni kwamba ben na Hebert waliingia katika ugomvi/kutokuelewana na baadae kusababisha kifo cha Hebert.

**C: UJUMBE**

1. Mipango mizuri ya maendeleo na utekelezaji wake mzuri ni kichochezi cha maendeleo katika jamii.

2. Baadhi ya mila na desturi za utamaduni wetu zimepitwa na wakati hivyo jamii haina budi kuzitupilia mbali mila na desturi hizo

3. Ukombozi wa mwanamke katika jamii ni jambo la muhimu sana kwani mwanamke akijikomboa atathaminiwa na kupewa haki zote.

4. Swala la ndoa ni jukumu la wawili wapendanao na lisiwe swala la kulazimisha kwa lengo la kukidhi kanuni na taratibu za mila na desturi zetu haswa zile zinazopitwa na wakati.

5. Mabadiliko ya kiutamaduni ni lazima mabadiliko hayo yaendane sambamba na mabadiliko yanayotokea kisiasa, kiuchumi na kifikra.

**B. FANI**

- **MUUNDO**

Mwandishi ametuma muundo wa moja kwa moja. Ameugawa mchezo katika maonesho manne na kila mchezo katika kichwa cha habari onesho la

**I.**NYUMBA **II.** NYUMBANI **III.** CHIRA **IV.** MSINGI ULIOBOMOKA

Mchezo unaanza kwa kuonesha ndoa ya Hebert na Martha ambao ndio wahusika wakuu.maisha yao ya ndoa na hatimaye vifo vya wote wawili na matokeo ya vifo hivyo.

- MTINDO

Kwa kiasi kikubwa mwandishi ametumia mtindo wa daolojia kutoka mwanzo hadi mwisho, Pia ametumia nafsi zote tatu katika mchezo huu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- MATUMIZI YA LUGHA

Mwandishi ametumia lugha ya kawaida yenye sentensi fupifupi, mbinu mbalimbali za kisanaa pamoja na tamathali za semi.

**Tamathali za semi**

Mwandishi ametumia tamathali mbalimbali kama vile:

i. **Tafsida**

Mfano: “wakati walipomzika marehemu Martha alikuwa hayupo duniani alikua ameshafariki”.

ii. **Tashihisi**:

Mfano: “vyura jana vilisema mvua inayokuja ni mvua ya rehema.”

**Vipengele vingine :**

i. Mdokezo

Mfano: “vilivyoshikamana vitakuwa vinapo.....”.

ii. **Lugha ya kishairi**:

Mwandishi ametumia lugha ya kishairi kwa kiasi Fulani.

Mfano: “unaona

Nti mwamvuli

Mwengine

Na mwengine

Na mwengine tena”

iii. **Matumizi ya vilugha** mwandishi ametumia Kiswahili kisichokuwa sanifu chenye athari ya kilugha

Mfano: “tumekuja kutengenesa barabara”.

“wapi ile daraja mbofu”

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

"sasa mutu hii tabu sana. Maiti itasikwa nyumbani. Moja anasema tujitegemee mwingine anasema hapana."

iv. **Mjalizo**

Mfano: "nataka pesa za ndoo mbili, ufagio, chumvi, mbao"

"kila kitu nyumba ,viwanja, gari, fanicha, kila kitu."

v. **Takriri:**

Mfano: "si rahisi pasta! Si rahisi kwa mwanamke, Si rahisi hata kidogo."

vi. **Matumizi ya kiingereza**

Mfano: "headquaters"

"a very happy man"

vii. **Matumizi ya taswira**

Mwandishi ametumia baadhi ya taswira katika mchezo huu ambazo ni:-

- **Jina la kitabu** , neno "thim" ni neno la kijaluo lenye maana ya **mwitu** kwahiyo kwenye ukingo wa thim maana yake ni baadhi ya mila na desturi zipo ukingoni kuisha.
- Chira

Taswira hii ina maana ya bahati mbaya.

- Kichwa cha tembo

Maana ya taswira hii ni kuachwa bila ya kitu chochote

- Tegemea mti ,mti utaanguka

Mwandishi anatuasa tusiwe tegemezi

- **WAHUSIKA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Wahusika wakuu ni Hebert na Martha ambao maudhui yanawahusu kwa kiasi kikubwa. Hawa ni mke na mume ambao kuona kwao kulisababisha watengwe na familia zao kwa kuwa walioana kutoka makabila tofauti.

Hebert ni msomi anaefanya kazi mjini ambae ameathiriwa na utamaduni wa mjini kiasi kwamba anasahau kwao kijijini, anashindwa hata kuwatembelea ndugu zake kijijini

Martha ni mke wa Hebert na mama yake chris, alishiriki kupigana vita vya maumau. Baada ya kufiwa na mumewe alinyang'anywa kila kitu kwakuwa yeye ni mwanamke, hivyo hakufaa kurithi chochote katika jamii.

Hawa ni wahusika mfano wa watu wengi wanaotaka mabadiliko katika mila na desturi za utamaduni wetu. Pia ni vielelezo vya watu wanaopinga ukabila katika jamii na hivyo wanafaa kuigwa katika jamii.

- **WAHUSIKA WADOGO**

- **Chris**

Mtoto wa Martha na mtoto wa kando wa Hebert anayesoma Colombia, amerika ya kusini. Ndiye aliyetegemewa kuwa mrithi wa mali za Hebert, lakini kwakuwa alikuwa mwanaharamu alikosa urithi huo.ni kielelezo cha kijana anaetaka mabadiliko na anafaa kuigwa.

- **George**

Huyu ni ndugu yake Hebert anayeishi kijijini ni kielelezo cha watu wanao ng'ang'ania mila na desturi zilizopitwa na wakati na pia ni kielelezo cha wanaoendeleza mfumo dume. Anamdhulumu Martha mali yote sio mfano wa kuigwa katika jamii.

- **Ben**

Huyu ni mwalimu wa chuo kikuu, kaka yake Martha, ni mkabila anaeshikilia mila na desturi zilizopitwa na wakati, Amesababisha kifo cha shemeji yake hafai kuigwa.

- **WAHUSIKA WENGINE**

Lidya, Stella, Jean hawa ni kielelezo cha vijana wakike walio mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko katika jamii hasa katika utamaduni.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Wapo mstari wa mbele kufuta mila na desturizinazomkandamiza mwanamke hivyo wanafaa kuigwa.

Pasta, mwenyekiti, mfanyakazi wa II na I, Sauti, Kizuizui, Ps, Mzee Mchimba, DC, Pc n.k.

- **MANDHARI**

Mandhari ni katika nchi ya Kenya na uthibitisho ni vita vya maumau ambavyo vilipiganwa Kenya. Pia makabila ya wajaluo na wakikuyu ambayo yanapatikana Kenya. Pia kwa kiasi kikubwa suala la ukabila lililojitokeza limekithiri nchini Kenya.

- **JINA LA KITABU**

"**kwenye ukingo wa thim**" jina hili linasadifu vizuri yaliyomo ndani ya kitabu. Neno "**thim**" ni neno la kijaluo lenye maana ya **mwitu.** Kwa hiyo **kwenye ukingo wa thim ,** ni taswira inayoonesha baadhi ya mila na desturi za zamani ,zinazoonekana kupitwa na wakati na hivyo ziko ukingoni kuisha. Kitabu hiki kinajadili mila na desturi za zamani zinazoonekana kupitwa na wakati kama vile watu kuoana katika kabila moja, kuchaguliwa wachumba, wanawake kutorithi mali, watoto wa kambo kutorithi pia, wanawake kunyimwa haki ya kuzika waume zao.

---

# TAFSIRI NA UKALIMANI

**DHANA YA TAFSIRI**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Profesa Mwansako (1961) "Kitangulizi cha Tafsiri" anafasili tafsiri kuwa ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja kwenda nyingine

Pia TUKI toleo la pili (2004) inaeleza kuwa "Tafsiri ni maana ya maneno kutoka katika matini iliyoandikwa katika lugha moja kwenda lugha nyingine."

**HITIMISHO**

Tafsiri ni kubainisha maneno kutoka lugha asilia na kuyaweka katika lugha lengwa kwa maandishi bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana. Kazi ya kutafsiri hujihusisha zaidi na maandi

**MBINU ZITUMIKAZO KATIKA KUTAFSIRI**
**AINA ZA TAFSIRI**

**Kuna aina nyingi zinazotumiwa katika kazi ya kutafsiri:-**

(i) TAFSIRI YA NENO KWA NENO
(ii) TAFSIRI YA SISISI
(iii) TAFSIRI YA KISEMANTIKI
(iv) TAFSIRI YA KIMAWASILIANO

1. **TAFSIRI YA KISEMANTIKI**

Ni tafsiri ambayo huzingatia maana iliyotolewa na mwandishi wa lugha asilia na hairuhusiwi kufanya marekebisho katika lugha asilia ili kukidhi matakwa ya lugha lengwa. Mtafsiri anatakiwa kutafsiri kila kipengele katika matini ya lugha asilia ili kupata maana iliyokusudiwa katika lugha asilia kwa kufuata sarufi ya lugha lengwa.

***Mfano:*** CHANZI***:*** Mwalimu Juma alimaliza shule ya msingi mwaka 1982 na alijiunga

na shule ya Sekondari Mzumbe 1983.

***LENGWA:*** Juma the teacher completed his Primary school Education in

1982 and joined Mzumbe Secondary School in 1983.

**UBORA:-**

1. Ina uwezo mkubwa wa kuendeleza lugha lengwa kwa kuingiza miundo na misemo kutoka lugha asilia.

***Mfano: CHANZI***: Wasalimie wote nyumbani

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***LENGWA:*** Greet all at home

2. Kusaidia katika kunukuu maneno ya mtu mwingine kwani kila neno hutakiwa litafsiriwe jinsi lilivyo pasipo kupoteza maana hata kipengele kimoja.

**UDHAIFU:**

Tafsiri ya kisemantiki hautilii maanani nahau na misemo maalum inayohusiana na

utamaduni wa lugha lengwa.

***Mfano: CHANZI*** (Kiingereza) Anna married John.

***LENGWA*** (Kiswahili) Anna amemuoa John

**II. TAFSIRI YA KIMAWASILIANO**

Hii ni tafsiri ambayo huwa inazingatia hadhara ya matini ya lugha lengwa kwa kumjali sana msomaji wa matini hiyo. Hii ni tafsiri huru inayompa ubavu mfasiri kuongea au kupunguza maneno ya matini ya lugha asilia wakati wa kufasili. Jambo la kuzingatia ni kwamba ujumbe uwafikie walengwa kwa namna ile ile bila kupoteza wazo la matini ya lugha asilia Mfasiri anauhuru wa kutumia maneno yanayolingana na misemo, methali, nahau, utamaduni na mazingira ya lugha lengwa.

**UBORA**

1. Njia hii hufuata kanuni, taratibu na sheria za lugha lengwa kwa kuzingatia mwelekeo wa utamaduni wake, historia, mazingira na hadhira lengwa.

***Mfano: CHANZI*** (Kiingereza): Anna married John.

***LENGWA*** (Kiswahili):John amemuoa Anna.

2. Tafsiri ya kimawasiliano husaidia hadhira lengwa kuelewa kwa urahisi. Tafsiri hii ni rahisi kwa kuwa uhusisha kile wanachosoma na hali halisi katika mazingira yao.

Tafsiri hii uhusu mabadiliko kulingana na historia, itikadi na mazingira ya hadhira ya lugha lengwa.

3. Huweza kuboresha au kusahihisha kifikiriwacho kuwa kilipotoshwa na matini ya lugha asilia ili kiweze kueleweka vizuri katika matini ya lugha lengwa.

**UDHAIFU:-**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. Haina uwezo wa kuendeleza, kuingiza miundo au misemo kutoka katika lugha asili kwenda lugha lengwa kwa sababu haizingatii wazo la jumla la kiutamaduni kwa lugha lengwa.

2. Kitendo cha mfasiri kuegemea sana kwenye mawazo, historia, utamaduni, mazingira na itikadi ya lugha lengwa inaweza kupotosha.

***Mfano:*** Wakati wa ugomvi wa Marekani na Iraq vyombo vya habari vya Iraq

Vilimuita Rais Sadam Hussein Mheshimiwa. Sentensi hizo hizi

zilitafsiriwa na vyombo vya habari ya Marekani kuwa " Gaidi Rais

Saadam Hussein".

**TAFSIRI YA NENO KWA NENO**

Hii ni tafsiri ambayo mofimu na maneno hufasiliwa yakiwa pwekepweke kwa kuzingatia maana zake za msingi bila kujali muktadha. Mpangilio wa mofimu na maneno wa lugha chanzi hubakia vilevile. Maneno yanayofunga maana na utamaduni hufasiriwa kisisisi. Matini ya tafsiri yaani matini ya lugha lengwa huandikwa chini ya matini chanzi.

***Mfano:*** ***CHANZI:*** Alikwenda mpaka nyumbani kwake.

***LENGWA:*** He/ passed /go/until/at/house/his

**UBORA:**

1. Husaidia kuelewa jinsi lugha chanzi inavyofanya kazi na jinsi muundo na maumbo yake yalivyo.

2. Husaidia katika kuainisha muundo na maumbo ya semi za lugha ngeni zinazofanyiwa uchunguzi

**UDHAIFU:**

Tafsiri hii haitoi kwa uwazi maana inayokusudiwa kwa sababu nahau na misemo inayohusiana na utamaduni hufasiriwa kisisisi.

1. **TAFSIRI SISISI**

Ni aina ya tafsiri ambayo maneno hufasiriwa ya kuwa pwekepweke kwa kuzingatia maana zake za msingi katika lugha chanzi bila kujali sana muktadha. Lakini hufasiriwa kufuatana na mfumo wa kisarufi, hususani sintaksia ya lugha lengwa.

**Mfano:** ***CHANZI:*** He was taken to the central police station

***LENGWA:*** Alipelekwa kituo cha kati cha polisi

(Neno "kituo cha kati cha polisi"limetumika badala ya kituo kikuu cha polisi)

**MCHAKATO WA KUTAFSIRI.**

Kwa ujumla mfasiri kabla ya kufanya mchakato wa kutafsiri anapaswa kuainisha matini kabla ya kuanza hatua ya kwanza ambayo ni maandalizi, kuainisha matini ni kitendo cha kuzigawa matini katika aina mbalimbali kutokana na mahitaji yanayotofautiana ya kifasiri kwa kila aina ya matini. Uainishaji huu wa matini hujikita katika mikabala mitatu:-

(i) Matini zinaweza kuainishwa kwa kufuata matumizi ya istilahi katika matini.

(ii) Kwa kufuata mada

(iii) Kwa kufuata dhima kuu za lugha

1. ***Maandalizi:*** Humuhitaji mfasiri kufahamu vizuri maudhui ya matini chanzi. Mfasiri huisoma matini nzima ya lugha chanzi ili kubaini ujumbe, mtindo na kuweka alama maalumu sehemu zenye utata au ugumu. Pia mfasiri hubaini utamaduni wa mwandishi wa wasomaji wa matini chanzi.

2. ***Uchambuzi:*** Mfasiri huchunguza maneno pamoja na maelezo muhimu ya matini chanzi yaliyoandikwa katika hatua ya maandalizi. Zoezi hili hufanywa kwa kutumia maendeleo mbalimbali kama vile kamusi na istihadi za vitabu mbalimbali.

3. **Kuhamisha matini chanzi kwenda matini lengwa**: (Uhamishaji) Mfasiri huhamisha mawazo, maana na ujumbe kutoka matini asilia kwenda matini lengwa. Mfasiri hufanya maamuzi juu ya zana za kisarufi zinaweza kutumiwa katika matini lengwa zitakazoelezea maana za matini asilia kwa usahihi zaidi.

4. **Rasimu ya kwanza**, Baada ya kubainisha maneno, tunapata rasimu ya kwanza ya tafsiri. Mfasiri hupata nafasi ya kufanya marekebisho kwa kuzingatia umbo la matini lengwa na kila lengo asilia.

5. **Udhalisuwa rasimu ya kwanza**: Katika hatua hii, mfasiri anapata nafasi ya kwanza ya kusahihisha matini iliyokwisha tafsiriwa. Mfasiri anapaswa aisome rasimu nzima kwa sauti kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Kusahihisha makosa ya kisarufi na miundo ya tungo isiyoeleweka vizuri.

(b) Kunyoosha sehemu zenye tafsiri ya mzunguko na zenye matumizi ya visa yasiyo ya lazima

(c) Kurekebisha sehemu zenye miunganisho inayozuia mtiririko mzuri wa matini.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(d) Kubaini iwapo mada au ujumbe mkuu wa matini unajitosheleza waziwazi katika tafsiri.

(e) Kuona kuwa lugha inayotumika ina uasili unaokubalika kulingana na mada na umbo la matini lengwa.

(f) Kubaini iwapo lugha inayotumika inazingatia utamaduni wa hadhira lengwa.

6. **Kusomwa kwa rasimu ya kwanza na mtu mwingine.** Mfasiri humpatia mtu mwingine matini lengwa ili aisome kuona kama inaeleweka na ina mtiririko mzuri wa mawazo. Dhima ya msomaji wa pili ni kuona kama tafsiri ipo sahihi, inaeleweka na ina mtiririko mzuri unaokubalika. Pia msomaji wa pili hutoa mapendekezo ya marekebisho yanayohitajika.

7. **Usawidi wa rasimu ya mwisho.** Mfasiri akishapata maoni ya msomaji wa pili, huyatunza maoni hayo kusahihisha tena rasimu yake na hatimaye hutoa rasimu ya mwisho. Hii ndiyo itakuwa matini lengwa

**B UKALIMANI**

Tuki (2004) anasema "Mkalimani ni mtu anayefasiri mazungumzo papo kwa papo kutoka lugha nyingne kwenda nyingine". Hivyo twaweza sema ukalimani ni kitendo cha kuhamisha maneno kutoka lugha moja kwenda nyingine kwa kuongea au mazungumzo. katika ukalimani mawazo au jambo lazima liwe katika mazungumzo na sio maandishi.

**AINA ZA UKALIMANI**

**I) Ukalimani wa papo kwa papo**, mkalimani anatafsiri papo kwa papo kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa.
mfano:- katika mikutano ya kidini, mihadhara n.k

**II)Ukalimani wa maandalizi,**

hapa mkalimani na mtoa mda hukaa pamoja na kuongea nini cha kufanya. mfano hutoba za kisiasa, mkalimani hukaa na mtoa hotuba ili kuwekeana mpaka katika kuongea.

**Mambo ya kuzingatia kwa mtoa mada/ hotuba**

- Ufasaha na usanifu wa lugha

- mpangilo mzuri wa wazo

- Ukweli na uwazi katika kujieleza

**Mambo ya kuzingatia kwa Mkalimani**

-Kuwa msikivu, Mtulivu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

-Aweze kuweka akili yake kwa yale yanayozungumzwa / Aweze kufahamu yanayozungumzwa

-umakini, ili awaze kufasiri kinachozungumzwa

-kujua matamshi ya mzungumzaji.

-Kuwa makini na kile kinachozungumza

**SIFA ZA MKALIMANI BORA**

**1:** Awe mtu anayezielewa lugha chanzi na lugha lengwa vizuri.

2: Awe ni mtu ambaye pande zote za lugha anazozikalimani ili kuelewa mila na desturi za watumiaji wa lugha hizo.

3: Awe standi wa ukalimani hapa anatakiwa awe hodari wa kukalimani, kuzungumza vizuri maneno kusika awe na uwezo wa kukalimani neno kwa neno au sentensi kwa sentensi .

4: Muadrifu ambaye awezi kupotosha au kubadili maana ya kinachozungumzwa.

5: Asiwe mbaguzi hii ina maana asibague kijinsia ,dini, umri au kisiasa bali afikishe kinachokusudiwa.

6: Awe makini kusikiliza kinachozungumzwa ili kuto changanya maana ya ujumbe unaokusudiwa kuifikia jamii.

**umuhimu wa tafsiri na ukalimani**

**-**Msamiati wa lugha lengwa hukua mfano baadhi ya maneno ya lugha ya kigeni hukua uchukuliwa na kuwekwa katika lugha lengwa.

-Kupanua uelewa wa kufahamu mambo kwa msomaji na msikilizaji.

-Kukua na kuenea kwa tamaduni mbalimbali.
mfano : Baadhi ya tamaduni za kigeni zimeingia katika Tanzania na pia Tamaduni za kitanzania zimesambaa duniani.

-Husaidia kupashana habari, kuwasiliana. Mfano Wasioelewa lugha ya kigeni huweza kupata habari kupitia kufasiriwa

**Matatizo ya tafsiri na ukalimani**

- Masuala ya itikadi na uelekeo, kutofautiana katika itikadi kunaweza sababisha kutoeleweka . mfano:- kingereza, irak walitangaza " Honourable peresident Sadam Hussein."

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Marekani walitangaza" Gaidi Raisi Sadam Hussen."

- Tofauti za kimazingira

| mfano:- Kingereza | Kiswahili |
| --- | --- |
| Autumn | Vuli |
| Winter | Kipupwe |
| Summer | Kiangazi |

-Tofauti za misemo, Nahau na methali.

-Kupuuzwa kwa ukalimani na tafsiri hapa Tanzania hivyo kupelekea kukosa wakalimani mahiri**.**

---

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/